# TATHMINI YA MAIGIZO YA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA KWENYE RUNINGA YA CITIZEN NCHINI KENYA

**(EVALUATION OF CHARACTERS WITH DISABILITIES IN THE SULTANA SHOW ON CITIZEN TV IN KENYA)**

**CAROLINE KEMUNTO GETATE**

**C50/OL/CTY/32347/2016**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA SHULE YA SHERIA, SANAA NA SAYANSI ZA KIJAMII ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**SEPTEMBA, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa popote kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

Sahihi.................. ...................Tarehe 29/09/2025

**Caroline Kemunto Getate**

**Msimamizi**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi..................................Tarehe.. 29/9/2025

**Profesa Richard Makhanu Wafula**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Kenyatta**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuniongoza hadi nikafika kiwango hiki cha elimu. Kwa wazazi wangu Bw.Getate Victor na Bi. Chepkorir Esther, ndugu zangu Dominic, Maria, Josea na Robina, mume wangu Jeremiah na wanangu Osborn, Joy na Precious.

## SHUKRANI

Namshukuru Mola kwa kunipa nguvu na uwezo wa kufika kiwango hiki cha elimu. Namshukuru kwa dhati msimamizi wangu Prof. Richard Wafula kwa kukubali kuniongoza katika safari hii ya masomo ya uzamili. Shukrani zangu ziwaendee wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Kenyatta, nao ni mwenyekiti wa Idara Prof. Peter Githinji na wahadhiri wengine wakiwemo Prof. Pamela Ngugi, Prof.Chacha Mwita, Dkt.Edwin Masinde, Dkt. Beth Mutugu na Dkt. Jessee Muriithi, kwa kunielekeza na kunitia moyo tangu shahada ya kwanza hadi sasa. Mungu awabariki nyote. Sitawasahau ndugu zangu kwa mchango wao wa hali na mali na kunihimiza kuendelea na masomo yangu. Mwisho, ninawashukuru watoto wangu kwa kuvumilia kutokuwepo kwangu na shauku yao ya kutaka kuona hatima ya kazi hii.

## IKISIRI

Kipindi cha Sultana kilipeperushwa kwenye runinga ya Citizen nchini Kenya kuanzia Machi, 2022 hadi Julai, 2023. Kipindi hicho kilihusisha wahusika mbalimbali wakiwemo walemavu. Tafiti za awali zimechunguza usawiri wa wahusika walemavu katika njia hasi. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza usawiri wa wahusika walemavu kwenye vipindi vya televisheni kwa njia chanya. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kuchunguza maigizo ya wahusika walemavu kwenye kipindi hicho. Suala la utafiti lilikuwa kutathmini maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana katika runinga ya Citizen nchini Kenya. Malengo ya utafiti huu yalikuwa; kujadili maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen, pili, kubainisha sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen na kufafanua mbinu za maigizo zinazotumika na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Maigizo (Turner, 1969) inayosisitiza umuhimu wa kudhihirisha mitagusano ya wanajamii kwenye maisha yao halisi kupitia matendo yao kwenye jukwaa. Aidha, nadharia hii inaonyesha manufaa ya hadhira katika kuchunguza vitendo vya waigizaji kwenye jukwaa. Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Maktabani mtafiti alidurusu vitabu, majarida, tasnifu na miswada mbalimbali kuhusu uigizaji, mbinu za utafiti na nadharia ya Maigizo. Utafiti wa nyanjani ulihusu ukusanyaji wa data kwa kuhusisha mahojiano na kurekodi. Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa ni simu ya rununu, tarakilishi na mwongozo wa mahojiano. Jumuiya ya utafiti ilikua waigizaji walemavu wa viungo na wa tabia wa kipindi cha Sultana cha runinga ya Citizen. Sampuli ya utafiti iliteuliwa kimaksudi ili mtafiti aweze kupata data ya malengo ya utafiti. Data ilikusanywa kwa kutazama, kusikiliza na kunukuu majibu ya maswali kutoka kipindi kiteule. Data ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia nadharia ya Maigizo, maswali na malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kimaelezo. Utafiti ulibaini kuwa wahusika walemavu wa viungo na wa tabia wanawasilisha maudhui mbalimbali. Wahusika walemavu wanawasilisha maudhui ya bidii, mapenzi, ujasiri na unyanyapaa ilhali wale wa tabia wanawasilisha maudhui ya ukatili, mauaji, tamaa na utabaka. Utafiti pia umeonyesha kuwa wahusika walemavu wana sifa mbalimbali wanazotumia kuwasilisha maudhui. Wahusika walemavu wa viungo wanadhihirisha kuwa na ukakamavu, hasira, ubinafsi, upweke, uvumilivu na hekima ilhali wale wa tabia wanadhihirisha kuwa na taasubi ya kiume, ukatili, udanganyifu, tamaa, ukaidi na uchochezi. Aidha, mbinu mbalimbali zilitumiwa na wahusika walemavu. Mbinu hizi ni pamoja na kufananisha, ishara za mwili, mazungumzo na hisia na mielekeo ya wahusika. Utafiti huu utasaidia kuongeza data muhimu katika taaluma ya fasihi. Pia, utawafaa watafiti watakaotumia nadharia ya Maigizo kwa kurejelea mihimili yake ambayo mtafiti amejadili kwa kina.

## ABSTRACT

Sultana was a drama series that was showcased by Citizen Television in Kenya between March 2022 and July 2023. The programme had different characters including those with disabilities. Earlier studies have investigated the negative portrayal of characters with disabilities, thus creating a gap. This study aimed to fill this gap by examining the positive portrayal of characters with disabilities on TV drama programs. Therefore, the study aimed to investigate the performances of characters with disabilities in the Sultana series of Citizen Television in Kenya. The objectives of this research were: to discuss the themes presented by characters with disabilities in the Sultana series of Citizen TV; secondly, to identify the character traits of the characters with disabilities in the Sultana series of Citizen TV, and to explain the dramatic techniques employed by characters with disabilities in the Sultana series of Citizen TV. This research was guided by the theory of Drama (Turner, 1969), which emphasizes the importance of showing the interactions of people in their real lives through stage actions. This theory also shows the role of the audience in evaluating the actors as they continue with their acting on stage. This study utilized data from both the library and the field. In the library, the researcher reviewed books, magazines, theses, and various manuscripts about acting, research methods, and the theory of Drama. Field research involved data collection through interviews and recording. The research tools that were used are a mobile phone, a laptop and an interview guide. The research population was the actors with physical and behavioural disabilities from the Sultana series of Citizen TV. The research sample was chosen purposefully so that the researcher could get the data for the research objectives. Data was collected by watching, listening, and getting answers to questions from the Sultana series. The data was analyzed descriptively based on the theory of drama, research questions, and research objectives. The results of the research were presented descriptively. The study established that characters with disabilities presented different themes. Characters with physical disabilities presented themes like hard work, love, bravery, and stigma. Characters with behavioural disabilities presented themes such as brutality, murder, greed, and classism. Characters with disabilities showcased different character traits. Those with physical disabilities showcased traits such as tenacity, anger, caring about others, selfishness, loneliness, patience, and wisdom. Characters with behavioral disabilities exhibited traits such as male chauvinism, cruelty, deceit, greed, stubbornness, and agitation. Also, it was established that disabled characters used different dramatic techniques to present different themes. Such techniques include imitation, body signs, dialogue, as well as sentiment and perception. This study will add important data to the Television drama. Additionally, it will be useful to researchers who refer to the Theory of Drama, as the researcher has discussed its tenets in detail.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **KBC:** | Kenya Broadcasting Corporation |
| **k.t:** | Keshatajwa |
| **KTN:** | Kenya Television Network |
| **NACOSTI:** | National Commission for Science, Technology and Innovation |
| **NTV:** | Nation Television |
| **TV:** | Televisheni |

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Maigizo:** Kutenda mambo kama yanavyotendwa na mwingine ama kumuiga mtu mwingine.

**Ulemavu**: Hali inayoashiria upungufu fulani wa mtu unaodhihirishwa na tabia yake, mwonekano wake au kupungukiwa kiuamilifu

**Ulemavu wa Viungo**: Hali inayodhihirisha binadamu kupungukiwa kiuamilifu na kimaumbile katika kiungo fulani kwenye mwili wake.

**Ulemavu wa Tabia:** Hali inayoonyesha ukosefu wa maadili inayojitokeza kupitia tabia za binadamu iliyo kinyume na matarajio ya jamii.

**Wahusika**: Viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ili wawe wasemaji wake katika kuufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

## YALIYOMO

**UNGAMO** .... ii
**TABARUKU** .... iii
**SHUKRANI** .... iv
**IKISIRI** .... v
**ABSTRACT** .... vi
**ORODHA YA VIFUPISHO** .... vii
**UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU** .... viii
**YALIYOMO** .... ix
**SURA YA KWANZA** .... 1
1.1 Utangulizi .... 1
1.2 Usuli wa Mada .... 1
1.3 Maelezo ya Dhana ya Maigizo .... 3
1.4 Majukumu ya Maigizo na Fasihi kwa Ujumla .... 4
1.5 Suala la Utafiti .... 5
1.6 Malengo ya Utafiti .... 6
1.7 Maswali ya Utafiti .... 6
1.8 Sababu za Kuchagua Mada .... 7
1.9 Upeo na Mipaka .... 8
1.10 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .... 9
1.10.1 Masuala ya Ulemavu kwa Jumla .... 9
1.10.2 Masuala Kuhusu Walemavu Katika Vyombo vya Habari .... 12
1.11 Misingi ya Nadharia .... 16
1.12 Mbinu za Utafiti .... 17
1.12.1 Muundo wa Utafiti .... 18
1.12.2 Mahali pa Utafiti .... 18
1.12.3 Uteuzi wa Sampuli .... 19
1.13 Vifaa vya Utafiti .... 20
1.13.1 Ukusanyaji wa Data .... 20
1.13.2 Uchanganuzi wa Data .... 21
1.13.3 Uwasilishaji wa Matokeo .... 21
1.13.4 Maadili ya Utafiti .... 22
1.14 Hitimisho .... 22

**SURA YA PILI** ........ 23
**MAUDHUI YANAYOWASILISHWA NA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA** ........ 23
2.1 Utangulizi ........ 23
2.2 Usuli wa Kipindi cha Sultana ........ 23
2.3 Dhana ya Maudhui ........ 27
2.4 Maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana ........ 28
2.4.1 Maudhui Yanayotokana na Wahusika wa Viungo ........ 28
2.4.1.1 Bidii ........ 28
2.4.1.2 Mapenzi ........ 30
2.4.1.3 Ujasiri ........ 31
2.4.1.4 Unyanyapaa ........ 33
2.4.2 Maudhui Yanayowasilishwa na Walemavu wa Tabia ........ 36
2.4.2.1 Ukatili ........ 36
2.4.2.2 Mauaji ........ 38
2.4.2.3 Tamaa ........ 40
2.4.2.4 Utabaka ........ 42
2.5 Hitimisho ........ 45
**SURA YA TATU** ........ 46
**SIFA ZA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA** ........ 46
3.1 Utangulizi ........ 46
3.2 Sifa za Wahusika Walemavu wa Viungo katika Kipindi cha Sultana ........ 46
3.2.1 Sifa za Mhusika Sultana ........ 47
3.2.1.1 Mkakamavu ........ 47
3.2.1.2 Mwepesi wa Hasira ........ 49
3.2.1.3 Muwajibikaji ........ 51
3.2.2 Sifa za Mhusika Kokani ........ 54
3.2.2.1 Mbinafsi ........ 54
3.2.2.2 Mpweke ........ 55
3.2.3 Sifa za Mhusika Buya ........ 57
3.2.3.1 Mvumilivu ........ 58
3.3 Sifa za Walemavu wa Tabia ........ 60
3.3.1 Sifa za Meja Jabali ........ 60
3.3.1.1 Mwenye Taasubi ya Kiume ........ 60

3.3.1.2 Katili.......... 62
3.3.2 Sifa za Mhusika Fatima .......... 64
3.3.2.1 Mdanganyifu .......... 64
3.3.2.2 Mwenye Tamaa .......... 65
3.3.3 Sifa za Mhusika Kaka .......... 67
3.3.3.1 Mkaidi .......... 67
3.3.3.2 Mchochezi .......... 68
3.3.4 Tathmini ya Sifa za Wahusika .......... 69
3.4 Hitimisho .......... 70
**SURA YA NNE** .......... 71
**MBINU ZA MAIGIZO ZINAZOTUMIWA NA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA** .......... 71
4.1 Utangulizi .......... 71
4.2 Mbinu za Maigizo .......... 71
4.2.1 Kufananisha .......... 72
4.2.2 Ishara za Mwili .......... 77
4.2.3 Mazungumzo .......... 81
4.2.4 Hisia na Mielekeo ya Wahusika .......... 85
4.2.4.1 Hisia na Mielekeo ya Wahusika Walemavu wa Viungo .......... 86
4.2.4.2 Mielekeo ya Wahusika Walemavu wa Tabia .......... 87
4.3 Hitimisho .......... 90
**SURA YA TANO** .......... 91
**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI** .......... 91
5.1 Utangulizi .......... 91
5.2 Muhtasari wa Utafiti .......... 91
5.3 Matokeo ya Utafiti .......... 92
5.4 Changamoto za Utafiti .......... 95
5.5 Mchango wa Utafiti .......... 96
5.6 Mapendekezo ya Utafiti .......... 96
5.6.1 Mapendekezo kwa Wadau Mbalimbali .......... 96
5.6.2 Mapendekezo kwa Tafiti za Baadaye .......... 97
5.7 Hitimisho .......... 98
**MAREJELEO** .......... 99
**VIAMBATISHO** .......... 105

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Tasnifu hii imeshughulikia maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen nchini Kenya. Sura hii ya kwanza imeweka msingi wa utafiti kwa kuangazia vipengele mbalimbali kama vile usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Aidha, sura hii imeshughulikia sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia na mbinu za utafiti.

## 1.2 Usuli wa Mada

Maigizo ni masimulizi yanayoambatana na matendo kwenye jukwaa mbele ya hadhira (Wanjala, 2011). Maigizo huwa na wahusika ambao hutumiwa kuwasilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii fulani. Katika jamii, matendo ya kawaida ya kila siku yaliigizwa (Matti, 1996). Matendo haya yanahusu shughuli kama vile: upashaji tohara, mazishi na kupewa jina kwa mtoto. Utendaji huu uliazimia kuathiri na kubadili mwelekeo wa jamii kuhusu masuala fulani (Schechner, 2013).

Vivyo hivyo, kazi za kifasihi ambazo hubeba dhima ya kijamii huchukuliwa pia kama aina ya maigizo kwa kuwa zinawasilisha masimulizi yanayowiana na uhalisia wa maisha ya binadamu. Kuna mifano mingi ya kuonyesha kuwa fasihi imetumika kubadilisha mielekeo ya jamii kupitia maigizo haya ya kifasihi. Kazi za kijamii kama vile *Kiza katika Nuru (1976)* na *Dunia Mti Mkavu* (1980) za Said Ahmed Mohamed zinapatikana katika mkabala huu kwa kuonyesha changamoto na mabadiliko katika jamii. Kazi za kifeministi kama vile *Tumaini* (2006) na *Nakuruto* (2007) za Clara Momanyi zina lengo la kubadilisha fikra na mtazamo wa jamii kuhusu jinsia ya kike. Katika ulingo wa kimataifa,

waandishi kama vile Ngugi wa Thiong'o ameandika vitabu kama *Petals of Blood* (1977) na *The Wizard of the Crow* (2006), ambavyo vyote vinajumuisha uanaharakati na maigizo ya kifasihi. Vilevile, mwandishi wa Marekani Harriet Stowe katika kitabu chake *Uncle Tom's Cabin* (1852) aliandika kazi ambayo iliigizwa na kupokewa kama tamthilia yenye hamasa ya kijamii, na hivyo kuhamasisha watu kupinga dhuluma dhidi ya weusi Marekani. Kwa hivyo, fasihi na maigizo vinashirikiana kama nyenzo za uanaharakati wa kijamii kwa kuwa fasihi mara nyingi hutumia mikondo ya kimaigizo ili kuathiri mielekeo ya jamii, ingawa si kila uanaharakati unaweza kuhesabiwa kuwa fasihi.

Ulemavu huashiria upungufu fulani wa binadamu unaojitokeza kutokana na tabia yake, mwonekano wake na uamilifu wake (Mutugu, 2019). Upungufu huu hubainika kutokana na waja kutokuwa na uwezo wa kuongea, kuona, kusikia, kutembea sawa na watu wengine na ukosefu wa kimaadili. Kulingana na Shirika la Afya Ulimwenguni (2024), inakisiwa kuwa zaidi ya watu bilioni moja nukta tatu duniani kote wana ulemavu. Hii ni takriban asilimia kumi na sita ya watu wote duniani. Aidha, asilimia themanini ya watu hawa wanapatikana kwenye mataifa yanayoendelea.

Kutokana na ugunduzi wa Shirika la Afya Ulimwenguni (k.t) kuhusu idadi ya walemavu duniani, mtafiti alichochewa kutafiti masuala ya walemavu katika vipindi vya runinga kama vile Sultana. Kutokana na uchunguzi wa awali wa mtafiti, tafiti chache zimeshughulikia maigizo ya wahusika walemavu kwa kina kwenye runinga zinazopeperushwa kwa lugha ya kiswahili nchini Kenya. Kauli hii inatupeleka katika maelezo ya maigizo.

### 1.3 Maelezo ya Dhana ya Maigizo

Dhana ya maigizo inaweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali. Maana ya dhana hii hutofautiana kutegema muktadha na tamaduni mbalimbali. Hii inamaanisha kwamba kile kinachoitwa maigizo katika jamii moja kinaweza kuwa na maana tofauti katika jamii nyingine kutokana na jinsi jamii hiyo inavyoifasili dhana hii.

Kulingana na Schechner (1988), kuigiza ni kumithilisha, ambapo mwigizaji hufanya vitendo vinavyofanana na yale ya mtu mwingine. Hii inamaanisha kwamba anayeigiza anaweza kuiga maneno, tabia au hata vitendo vya wengine ili kuifanya ionekane kama utekelezaji wa kweli wa kile kinachoigizwa. Kwa kuwa umithilishaji unahusisha vitendo, maigizo yanachukuliwa pia kama aina ya Sanaa tendaji.

Kulingana na Bauman (1992), maigizo mara nyingi yanahusisha njia ya kuwasiliana na hadhira kupitia jukwaa kwa njia inayovutia na inayochochea hisia. Aidha, Bauman anasema kwamba maigizo yote yanatokea na kuthaminiwa kulingana na muktadha wa kijamii unaohusika. Anaongezea kuwa kupitia maigizo, tunaweza kugundua vitengo vya kijamii, kitamaduni na vya kiujumi vya tukio la mawasiliano.

Bauman anaeleza kuwa miongoni mwa maigizo yanayothaminiwa ni maigizo ya kitamaduni na haya huwa na sifa maalum kama ifuatavyo:

(i) Matukio haya huandaliwa mapema kabla ya wakati wa kuigizwa.

(ii) Yana mwanzo na mwisho maalumu au yanayoweza kutambulika.

(iii) Hutekelezwa katika eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya tukio hilo. Eneo hili linaweza kuwa la muda mfupi au la kudumu, kama ukumbi wa maonyesho, uwanja wa sherehe au eneo lisilo rasmi lililoheshimiwa.

(iv) Huwa na ratiba maalumu inayoonyesha mfuatano wa matukio.

Maigizo haya huwa ni matukio ya hadhara yaliyopangwa na yanayotazamwa na hadhira, pia hutoa fursa kwa washiriki kukutana na kudhihirisha vipawa vyao.

Kulingana na Wamitila katika Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia (2003), uigizaji ni ufundi na ustadi wa kuwasilisha au kutekeleza kazi za sanaa kwa kuiga vitendo fulani na kuvionyesha mbele ya hadhira. Kamusi hiyo pia inafasili maigizo kama dhana inayotumiwa kuelezea utanzu mojawapo wa fasihi simulizi. Maigizo huhusisha uwasilishaji wa tungo mbele ya hadhira na huambatana na utendaji au uigizaji.

King'ei (2005) anaeleza kuwa maigizo ni ile hali ya kuiga maneno au vitendo vya wengine, ni mchakato wa kufanya na kusema kwa namna inayofanana na ile ya mtu mwingine, ambapo matendo yanapewa uzito mkubwa. Katika utafiti huu, neno maigizo linatumika kueleza jinsi mhusika anavyotoa ujumbe wake kupitia maneno yanayoambatana na vitendo.

## 1.4 Majukumu ya Maigizo na Fasihi kwa Ujumla

Maigizo yana majukumu kadha wa kadha kwa hadhira inayolengwa. Kupitia maigizo, dhamira na maudhui ya mtunzi huwasilishwa. Baadhi ya majukumu ya maigizo ni kama yafuatayo:

Goodland (1971) anaeleza kuwa maigizo yana mchango mkubwa kwa jamii, kwani husaidia kukuza utamaduni, kudumisha mifumo ya kijamii na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala mbalimbali.

Kwa mujibu wa Traore (1972), maigizo ni vitendo vinavyotokana na uzoefu wa binadamu katika kukabiliana na maisha na vinavyoonyesha uhalisia wa maisha yaliyojaa chanagamoto na migogoro. Hali hizi halisi humpa mwigizaji fursa ya kutoa mchango wake katika kuwakilisha matatizo yanayoikabili jamii. Aidha, mwigizaji anaweza kutumia uigizaji kama njia ya kukosoa jamii yake, hasa inapokuwa na vitendo vinavyoonyesha athari mbaya.

Robinson (1980) anasema kuwa hakuna aina ya uigizaji unaofanywa bila nia ya kuwasiliana au kuathiri hisia za hadhira. Mafanikio ya uigizaji hupimwa kwa jinsi mawasiliano yanavyofanyika.

Ngugi wa Thiong'o (1986) anasema maigizo hayakuwa shughuli iliyojitenga, yalikuwa kiungo mojawapo cha maisha ya kila siku yaliyofuata mkondo wa majira katika jamii. Mbali na kuwa aina ya burudani, yalikuwa njia ya kufunzia na pia shughuli iliyochukuliwa kwa dhati kama njia mojawapo ya kuyaendeleza maisha ya jamii.

Matti (1996) anaelezea kwamba maigizo mazuri ni yale yanayowakilisha ufanisi wa utamaduni katika kuonyesha mabadiliko katika maisha ya binadamu. Hii inatokana na dhana kwamba fasihi ni kioo cha jamii na hivyo maigizo, kama sehemu ya fasihi, yanapaswa kuakisi mabadiliko ya kitamaduni yanayojitokeza katika maisha ya kila siku.

### 1.5 Suala la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen kwa nia ya kuonyesha kwamba katika kipindi cha Sultana, wahusika walemavu wanasawiriwa kwa njia inayoafiki wahusika wa kawaida wasiokuwa walemavu. Wahusika hao wanaonyesha upungufu na uchanya bila kupigwa chuku na

hivyo, kusitisha unyanyapaa ambao huhusishwa na walemavu. Tafiti za awali kama vile: Wright (2006) na Mutugu (2019) zimejiegemeza katika wahusika walemavu wanaojitokeza katika kazi za fasihi andishi kama vile riwaya na tamthilia. Isitoshe, tafiti nyingine kama vile za Mathooko na Wengine (2012), Njoroge (2018), Gao na Njeri (2020) zinaangazia nafasi ya walemavu katika vyombo vya habari. Maigizo ya wahusika walemavu katika vipindi vya runinga vinavyopeperushwa kwa lugha ya Kiswahili kama vile *Neema,Selina,Maria na Mali* nchini Kenya, hayajachanganuliwa kwa kina. Utafiti huu ulinuia kuziba pengo hili kwa kuchunguza taswira ya ulemavu kupitia maigizo katika kipindi cha Sultana.

**1.6 Malengo ya Utafiti**

i. Kujadili maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen.
ii. Kubainisha sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen.
iii. Kufafanua mbinu za maigizo zinazotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen.

**1.7 Maswali ya Utafiti**

i. Maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen ni yapi?
ii. Sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen ni zipi?

iii. Ni mbinu zipi za maigizo zinazotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen?

**1.8 Sababu za Kuchagua Mada**

Sababu ya kwanza ya kuchagua mada hii ni kuwa utafiti wa awali haujashughilikia maigizo ya wahusika walemavu kwenye runinga zinazopeperusha kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya, hasa kipindi cha Sultana. Kama ilivyo kazi yoyote ya Sanaa, maigizo haya yana sifa mahsusi ambazo hazina budi kuchunguzwa. Ulemavu ni hali inayotukabili kila wakati na hatuwezi kuepukana nayo na hivyo usomi juu yake ni muhimu.

Pili, tuliamua kuchanganua maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu, sifa zao na mbinu za maigizo wanazotumia katika kipindi cha Sultana kwa sababu ndivyo vigezo vinavyofaa zaidi kutathminia upeo wa sanaa katika fasihi. Hii ni kwa madhumuni ya kuweka wazi majukumu muhimu yanayofanywa na wahusika walemavu katika sanaa ya maonyesho kwa lengo la kubadilisha mielekeo ya kijamii kuhusu ulemavu. Wahusika hutumiwa kuwakilisha hali halisi ya maisha ya watu katika jamii inayohusika na kuwakilisha mawazo mbalimbali ya dhana katika kazi za fasihi (Msokile, 1992).

Tatu, utafiti huu ulidhamiria kuchangia katika uwanja wa uchanganuzi kimaudhui na kimtindo katika kipindi cha Sultana kama kielelezo na utafiti huu utachochea tafiti fuatilizi za maigizo katika vyombo vya habari hasa kwenye runinga. Tafiti kama hizi zitawapa watu walio na ulemavu wa aina yoyote ari na shime ya kushiriki katika maendeleo ya kijamii kama vile sanaa na elimu.

Nne, tulichagua mada hii ili kuongeza data muhimu katika maigizo ya wahusika walemavu katika vipindi vya runinga vinavyopeperushwa kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Mawasiliano ya runinga ni muhimu kwa kuwa hugusa hisia za watu wanapotazama matendo ya wahusika ikilinganishwa na kusoma kwenye maandishi. Sababu hizi zinatuongoza kwenye upeo na mipaka ya utafiti.

### 1.9 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen, nchini Kenya. Utafiti huu ulichagua kipindi cha Sultana kilichopeperushwa kati ya saa moja na nusu jioni na saa mbili kamili usiku kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na kurudiwa Jumamosi kuanzia saa kumi jioni. Utafiti huu ulijikita katika filamu wala si katika fani nyingine yoyote ya fasihi.

Ingawa kuna vipindi vingine vya runinga vinavyopeperushwa kwa lugha ya Kiswahili na vyenye maigizo ya wahusika walemavu kama vile *Neema*, *Selina, Maria na Mali* tulichagua kipindi cha Sultana kwa sababu utafiti wa awali ulithibitisha kuwa nafasi ya wahusika walemavu inajitokeza zaidi katika kipindi hiki ikilinganishwa na vipindi vingine. Katika kipindi cha Sultana, walemavu wamepatiwa majukumu muhimu ikilinganishwa na vipindi vingine vilivyohusisha walemavu. Wahusika walemavu wamepewa majukumu ya kuwasilisha hali halisi ya maisha ya binadamu kupitia mbinu za maigizo.Wahusika hawa wamepewa sifa maalum kulingana na lengo la mwandishi la kupitisha dhamira na maudhui kwa hadhira lengwa, kama asemavyo Rono (2013), wahusika wa kazi za sanaa huwa na sifa tofauti kati yao kulingana na dhamira ya

mwandishi na utanzu husika wa kazi ya fasihi na kwa hivyo mwandishi huwasawiri kwa njia tofauti.

Wahusika lengwa ni walemavu wa viungo na wa tabia pekee. Mutugu (2019) anasema kuwa ulemavu wa viungo unarejelea hali ambapo binadamu anaonyesha upungufu wa kimaumbile katika kiungo fulani cha mwili wake. Anaendelea kusema kuwa ulemavu wa tabia ni hali ambapo mtu anaonyesha tabia zisizofaa kulingana na matarajio ya jamii.

Ili kufanikisha utafiti huu, data iliyolengwa ni ile inayohusiana moja kwa moja na maigizo yanayosawiri ulemavu kwenye kipindi cha Sultana. Maudhui, sifa za wahusika na mbinu za maigizo zilichunguzwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia matukio katika kipindi kiteule, kauli na matendo ya wahusika mbalimbali. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Maigizo (Turner, 1969) inayosisitiza uhalisia na uhusiano kati ya mwigizaji na hadhira katika maigizo.

## 1.10 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu suala la walemavu duniani. Utafiti ulidurusu tafiti hizi ili kuzilinganisha na kuzilinganua na utafiti lengwa. Aidha, mchango wa tahakiki hizi katika utafiti huu ulibainika wazi. Yaliyoandikwa kuhusu mada yamegawanywa katika sehemu mbili kuu. Nazo ni tafiti kuhusu masuala ya ulemavu kwa jumla na tafiti kuhusu masuala ya ulemavu katika vyombo vya habari.

### 1.10.1 Masuala ya Ulemavu kwa Jumla

Devileger (1999) alichunguza miktadha ya kimaisha na kimaana inayojitokeza kwenye methali hamsini na tano zinazohusu ulemavu. Katika uhakiki wake amezingatia lugha kutoka mataifa ya Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Zambia,

Zimbwabwe na Senegali. Anatambua kuwa ulemavu ni tukio zito unaohusisha taashira nzito. Kwa upande mmoja, mlemavu anadhihirisha taashira ya maisha iliyo na ubunifu, maadili na matumaini na kwa upande mwingine unahusishwa na uovu ambao sharti chimbuko lake lichunguzwe. Utafiti huu ulitufaa kwa kutupa kiini cha ulemavu. Tofauti kati ya utafiti huu na wetu ni kuwa utafiti wa Deliveger unahusu methali na huu unahakiki maigizo ya runinga.

Wright (2006) alichunguza juu ya "maadili ya wahusika wenye ulemavu katika kazi iliyoandikwa na Lawrence *Lady Chatterly's Lover*. Anabainisha kuwa wahusika wengi walemavu wanakumbana na dhiki nyingi katika kupigania nafasi zao kwenye jamii. Wao hupitia changamoto wanapojaribu kujitambua na kujitathmini. Anatambua ulemavu wa wahusika kama picha inayotumika kwenye kazi za kifasihi kuwasilisha maudhui. Kwa msingi huo, tuliweza kuchanganua maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Utafiti huu unazingatia hali ya kisaikolojia ya wahusika walemavu ilhali utafiti wetu ni wa kudhihirisha nafasi ya wahusika walemavu katika maigizo ya runinga.

Mahenge (2017) katika makala yake iitwayo *Msigano wa Majina ya Walemavu Katika Jamii ya Wazungumzaji Kiswahili*, amegundua kuwa maana ya ulemavu hutofautiana baina ya watu walio na ulemavu na wale wasio na ulemavu. Isitoshe, utafiti wake umebaini kuwa walemavu hupewa majina yanayowakebehi katika jamii na kamusi. Mahenge (k.t) anahimiza wanajamii kubadili namna wanavyowaita walemavu katika jamii. Makala haya yalitupa mwanga zaidi kuhusu dhuluma za kisaikolojia wanazopitia walemavu kutokana na majina wanayopewa na waja. Utafiti wa Mahenge ulitufaa katika

kutambua sifa za wahusika walemavu ambao wameathiriwa na hali hii. Hata hivyo, utafiti wa Mahenge uliangazia walemavu kijumla ilhali utafiti huu ulijikita kwenye walemavu wa viungo na wa tabia.

Mutugu (2019) alitafitia kuhusu "taswira za ulemavu kama mtindo katika riwaya teule za Said Ahmed na Euphrase Kezilahabi." Aliangazia taswira za walemavu wa akili, wa tabia na wa viungo kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya waandishi. Utafiti wa Mutugu ulithibitisha kuwa taswira za ulemavu zilitumiwa na watunzi wa kazi hizo kama mtindo wa kuwasilisha maudhui. Utafiti wake ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa ulijengea msingi utafiti huu haswa kwa kubainisha na kueleza dhana na aina za wahusika walemavu. Utafiti wake unatofautiana na utafiti lengwa kwa kuwa mtafiti alichunguza maigizo ya wahusika walemavu kwenye kipindi cha runinga ilhali yeye alijikita kwenye uchanganuzi wa riwaya teule.

Karimi (2022) alitafiti kuhusu nafasi ya wahusika wendawazimu katika riwaya za *Kidagaa Kimemwozea* na *Mkamandume*. Akitumikiza mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Nafsia, alibainisha namna wahusika wendawazimu hufanikisha maudhui, huendeleza mbinu za uandishi na kufaulisha dhamira katika riwaya teule. Utafiti wa Karimi (k.t) ulitupa mwanga zaidi kuhusu nafasi ya walemavu katika fasihi na jamii kwa ujumla. Hata hivyo, tofauti naye, utafiti huu ulijikita kwa walemavu wa viungo na wa tabia wala sio walemavu wa kiakili. Pia utafiti wa Karimi umejiegemeza katika riwaya teule ilhali huu wetu ulijikita katika maigizo ya runinga.

Mchepange na Mahenge (2022) wameandika makala kuhusu methali za Kiswahili zihusuzo ulemavu. Wamebaini kuwa methali hubeba mitazamo hasi na chanya kuhusu

ulemavu na walemavu katika jamii. Utafiti huu ulitupa mwanga zaidi kuhusu sifa za wahusika walemavu wa viungo na wa tabia ambao wameathiriwa na mitazamo hasi au chanya kuhusu walemavu katika jamii, kwenye kipindi cha Sultana. Hata hivyo, utafiti wa Mchepange na Mahenge (k.t) ulilenga methali ilhali utafiti huu ulijikita katika utanzu wa maigizo.

Muguche (2022) alitafiti kuhusu "ulinganishaji wa ujifunzaji stadi za Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika kaunti za Nakuru na Kisumu." Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho hukumbwa na changamoto nyingi kwenye shule teule kwa sababu ya tofauti za kimazingira katika shule hizo. Utafiti huu ulikua na manufaa kwa utafiti wetu kwa vile ulitupa uelewa wa walemavu wa macho tulipokua tunashughulikia walemavu wa viungo. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa utafiti wa Muguche uliangazia tofauti ya kimazingira katika kujifunza stadi za Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho, ilhali utafiti wetu ni wa maigizo ya wahusika walemavu katika maigizo ya runinga.

### 1.10.2 Masuala Kuhusu Walemavu Katika Vyombo vya Habari

Barnes (1992) alichunguza "matumizi ya tamathali za usemi zinazolemaza katika vyombo vya habari." Alijikita katika imani za kiasilia ambazo hazina msingi wowote kimantiki kuhusu watu walemavu kwenye vyombo vya habari. Aliangazia majarida, filamu, runinga na redio. Utafiti wa Barnes ulitambua kuwa mambo mengi yaliyojitokeza kwenye vyombo vya habari kuhusu ulemavu yalikuwa hasi sana. Walemavu wanaonekana kama wanyonge na wategemezi. Tofauti kati ya utafiti wa Barnes na huu

ni kuwa yeye alichunguza usawiri wa watu walemavu kwenye vyombo vya habari na namna usawiri huo unavyowalemaza watu hao. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu ulitupa mtazamo unaopatikana katika jamii kuhusu watu wenye ulemavu.

Mathooko na wengine (2012) walishughulikia nafasi ya watu walemavu kwenye vyombo vya habari. Utafiti wao ulizingatia hadithi kuhusu ulemavu na watu walemavu na picha zinazofuatana na hadithi hizo. Wanasema picha na hadithi zipatikanazo kwenye vyombo vya habari zina athari katika fikira za watu. Utafiti huu ulitufaa kwa kutazama jinsi vyombo vya habari kwa ujumla vinavyowakilisha watu wenye ulemavu. Maoni haya yalinufaisha utafiti huu kutambua wahusika walemavu wanaodhihirisha sifa kama hizi. Utafiti wa Mathooko na wengine (k.t) ni tofauti na huu kwa kuwa unaangazia nafasi ya watu walemavu kwenye vyombo vya habari kwa ujumla ilhali tuliangazia wahusika wenye ulemavu katika runinga pekee.

Shule (2017) aliangazia jinsi waigizaji wenye ulemavu wanavyoathiriwa na mitazamo ya kijamii na tasnia ya filamu nchini Tanzania. Matokeo yalionyesha kuwa shida kubwa ya waigizaji hawa ni upatikanaji wa fursa za kutosha za uigizaji kwa waigizaji wenye ulemavu. Utafiti lengwa uliziba pengo katika muktadha wa Kenya, kwa kutathmini iwapo wahusika walemavu wanapewa fursa inayotosha katika uigizaji. Utafiti wa Shule (k.t) ni tofauti na utafiti lengwa kwa sababu uliangazia muktadha wa nchi ya Tanzania ilhali utafiti huu ulikuwa wa muktadha wa Kenya.

Njoroge (2018) alihakiki juu ya uwakilishi wa walemavu katika televisheni za Kiafrika na kugundua kuwa uwakilishi wa wahusika hawa katika vipindi vya televisheni unaweza kuwa na matokeo mchanganyiko. Wahusika wenye ulemavu mara nyingine wanaweza

kuonyeshwa kama wenye uwezo na wenye nguvu, wakati mwingine wanaweza kuonekana kama wenye utegemezi. Hii inaweza kusababisha mitazamo tofauti ya umma kuhusu ulemavu. Manufaa ya utafiti huu ni kwamba, kutokana na mitazamo anayopeana, mtafiti tuliweza kuangalia mitazamo hiyo kwa mukadha wa kipindi cha Sultana.Tofauti kati ya utafiti huu na lengwa ni kwamba, Njoroge (k.t) amechanganua kuhusu uwakilishi wa wahusika walemavu katika vipindi vya televisheni kwa ujumla ilhali utafiti lengwa uliangalia uwakilishi wa wahusika walemavu katika kipindi kiteule cha Sultana.

Smith (2019) alifanya uchambuzi wa jinsi walemavu wanavyowakilishwa katika uigizaji wa runinga na kugundua kuwa walemavu mara nyingi wanawakilishwa katika majukumu ya chini na wahitaji. Hii inaashiria ukosefu wa uwiano na uwakilishaji mzuri wa ulemavu katika tasnia ya burudani. Utafiti huu ulitupa msingi wa kuangalia iwapo waigizaji walemavu wamepewa nafasi sawa na wenzao katika kipindi cha Sultana. Tofauti kati ya utafiti wa Smith na huu ni kuwa, utafiti wake unahusu uwakilishi wa wahusika katika runinga kwa ujumla ilhali utafiti wetu ulijikita katika kipindi kiteule cha Sultana cha runinga ya Citizen.

Gao na Njeri (2020) walichunguza juu ya jukumu la shirika la walemavu katika televisheni. Walibaini kuwa walemavu wanakutana na upinzani katika kufikia majukumu ya uigizaji kutokana na ukosefu wa ufahamu na ubaguzi wa aina mbalimbali. Changamoto hizi zinaweza kuzuia walemavu kuchukua nafasi za uigizaji za kisasa na kusababisha uwakilishaji duni. Utafiti huu ulitupa msingi wa utafiti wa jinsi wahusika hawa wanavyowakilishwa katika kipindi cha Sultana. Tofauti ya utafiti huu na utafiti lengwa ni kuwa wao wanapochambua changamoto za wahusika walemavu, sisi

tuliangazia nafasi za wahusika walemavu katika kipindi kiteule katika kuendeleza maudhui na dhamira kwa hadhira lengwa.

Mawira (2020) alitafitia juu ya kutengwa kwa walemavu katika vyombo vya habari. Anasema kuwa ulemavu ni hali inayojumuisha vizuizi vya mwili au kisaikolojia ambavyo vinaweza kumfanya mtu awe na uwezo mdogo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii au kazi. Hii inamaanisha kuwa mtu mwenye ulemavu ananyimwa nafasi ya kutekeleza majukumu fulani akilinganishwa na mtu wa kawaida. Utafiti huu ni faafu kwa kuwa, ulimsaidia mtafiti alipokuwa akishughulikia sifa za wahusika walemavu wanapoendeleza shughuli zao za kila siku. Tofauti ni kuwa utafiti lengwa ulizingatia maigizo ya wahusika walemavu katika runinga.

Dimbu (2021) alitafiti kuhusu hali ya kijamii na uchumi na athari zake kwa waigizaji walemavu katika vyombo vya habari vya Afrika Mashariki. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa tabaka la kijamii linaweza kuathiri tajriba za waigizaji. Utafiti huo unajumuisha nchi za Afrika Mashariki na umeangazia sehemu pana. Hata hivyo, utafiti wa Dimbu ulitoa ufahamu muhimu wa athari za kijamii na uchumi kwa waigizaji walemavu katika runinga.

Kutokana na tafiti ambazo zimeelezwa, ni wazi kwamba tafiti chache za ulemavu katika vipindi zimefanywa japo sio kwa kina. Hivyo basi, mtafiti alinuia kuchunguza tathmini ya maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen nchini Kenya. Maandishi haya kuhusu mada ya utafiti yatatupeleka kwenye nadharia iliyotumika katika utafiti huu

## 1.11 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Maigizo iliyoasisiwa na Turner (1969) na kuendelezwa na Schechner (1988), Fine (1994) na Foley (1995). Turner (k.t) alichunguza kwa undani suala la matambiko na maigizo. Alibaini kuwa uigizaji wa matambiko hutumia ishara zinazowakilisha utamaduni wa jamii. Ishara hizi hubadilika kutoka jamii moja hadi nyingine. Kwa mujibu wa Schechner (k.t) maigizo huwa njia ya kuelewa mtagusano wa kijamii kwani mwigizaji hutathminiwa na hadhira. Mutegi (2010) anaeleza kuwa maigizo huwa na maana tofautitofauti kutegemea jinsi yanavyochukuliwa na hadhira. Isitoshe, Yovo (2021) anaeleza kuwa kwa kupitia maneno utendaji wa wahusika hubainika.

Fine (1994) na Foley (1995) wanaorodhesha vigezo vinavyotambulisha nadharia ya maigizo kama vile: jukwaa, ujumi kwenye mawasiliano, tukio, sajili, mila na utamaduni zinazohusika na iktisadi ya mawasiliano. Kupitia kauli zao mihimili ifuatayo imeorodheshwa ili kufaa utafiti huu:

1. Uigizaji unafaa kusawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi kiasi kuwa hadhira itaelewa kinachozungumziwa. Mwigizaji sharti aige hali tofauti maishani inayowakabili hadhira. Mhimili huu ulituwezesha kutambua maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana.
2. Uigizaji unaomshirikisha mtendaji hai una ufanisi mkubwa kwa kuwa mtendaji huyo ana uwezo wa kufaragua vitendo vyake kwa ajili ya kutosheleza matakwa ya hadhira yake. Mhimili huu ni muhimu kwenye utafiti huu kwa kuwa ulituwezesha kubainisha wahusika walemavu na sifa zao kupitia vitendo vyao.

3. Maigizo sharti yafanywe kwa ubunifu kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuvutia hadhira. Kila uigizaji unafaa kuishawishi hadhira kuuzingatia na ni kwa njia hiyo pekee utakavyoweza kufanikisha mawasiliano. Mhimili huu ulitufaa katika kuangazia mbinu mbalimbali za maigizo zinazotumiwa katika kipindi cha Sultana ili kuvutia hadhira, ikiwemo lugha ya kuvutia, ishara za uso, mikono, miondoko ya mwili, taharuki na nyimbo.
4. Kupitia maigizo sharti mila na tamaduni za jamii zibainike na kuendelezwa. Kwa njia hii hadhira itahudumiwa kwa kufahamishwa masuala mbalimbali. Kupitia mhimili huu athari ya mila na tamaduni katika sifa za mhusika mlemavu wa kipindi cha Sultana zilibainishwa. Maudhui yanayohusiana na mila na utamaduni yalichunguzwa pia kupitia mhimili huu.
5. Jukwaa linalotumiwa na waigizaji sharti liwakilishe uhalisia. Kupitia mhimili huu athari ya mandhari kwa mhusika mlemavu ilibainishwa na jinsi mandhari ya mhusika mlemavu inaathiri mwenendo wake.

## 1.12 Mbinu za Utafiti

Kothari (2004) anasema kuwa mbinu za utafiti ni seti ya taratibu na njia zinazotumika kukusanya, kuchambua, na kuelewa data kwa lengo la kupata ufahamu wa kina kuhusu suala fulani la utafiti. Kila mbinu inatekelezwa kulingana na muktadha wa utafiti na malengo ya mwandishi. Uchaguzi sahihi wa mbinu za utafiti unaweza kuwa msingi wa mafanikio ya utafiti, kutoa ufahamu wa kipekee, na kuchangia kwenye uelewa wa jamii na sayansi. Uchaguzi wa mbinu unategemea sana malengo ya utafiti na aina ya data inayotarajiwa kupatikana.

### 1.12.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitekelezwa kwa njia ya kimaelezo. Utafiti wa Hakim (1982), unaashiria kuwa mbinu ya kimaelezo hueleza jinsi mambo yalivyo bali haielezi sababu ya mambo kuwa hivyo. Hii itatufaa katika kujibu maswali ya utafiti. McCombes (2019) anasema kuwa, utafiti wa kimaelezo ni chaguo mwafaka wakati lengo la utafiti ni kubainisha sifa, masafa, mienendo na kategoria ya mambo. Mbinu hii iliwezesha upatikanaji wa habari kamili katika kubainisha na kufafanua maudhui, sifa za wahusika na mbinu za maigizo za wahusika walemavu kulingana na malengo na mihimili ya nadharia ya Maigizo. Kwanza kabisa, mtafiti alitazama kipindi cha Sultana kuanzia mwanzo hadi mwisho ili kubaini iwapo kutapatikana data inayotosha kujibu maswalili ya utafiti.

### 1.12.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti lengwa ulifanywa maktabani na nyanjani. Tromp (2006) anaeleza kuwa dhima kuu ya kufanya utafiti maktabani ni kumpatia mtafiti data chasili itakayomwongoza kwa upana kwenye suala analolitafiti kupitia ukusanyaji wa data kwa njia ya usomaji. Maktabani, mtafiti alisoma vitabu, majarida, makala, ripoti maalum, tasnifu, magazeti na habari zozote zinazowiana na mada na malengo ya utafiti. Lengo la kudurusu maandishi tofauti tofauti ni kuangalia yaliyoandikwa hapo awali na inahusiana na mada ili kubaini ni pengo lipi mtafiti ataziba. Pia, mtafiti alisakura mtandao wa kijamii haswa kwa lengo la kupata data ya malengo ya utafiti. Kipindi cha Sultana kilitazamwa kwenye mitandao ya *Youtube na Viusasa*. Aidha, mtafiti alimhoji mtayarishaji na baadhi ya wahusika walemavu wa kipindi cha Sultana nyanjani.

### 1.12.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli yetu ilichaguliwa kwa mbinu ya kimaksudi. Utafiti huu una aina tatu za sampuli. Sampuli ya; vituo vya runinga, watayarishaji wa vipindi na wahusika. Utafiti lengwa ulitumia sampuli ya kimaksudi. Kulingana na Kombo na Tromp (2006), uteuzi kusudi wa data huhusisha data iliyo na sifa zinazolengwa moja kwa moja na utafiti lengwa.

Nchini Kenya kuna vituo mbalimbali vya runinga kama vile; Citizen, KBC, NTV, K24, KTN, TV47 miongoni mwa vituo vinginevyo. Hata hivyo, utafiti lengwa haukuhusisha vituo vyote ila kituo cha runinga ya Citizen. Runinga ya Citizen iliteuliwa tofauti na vituo vinginevyo vya runinga kwa sababu ina mashabiki wengi nchini Kenya kulingana na Baraza la Vyombo vya Habari Nchini Kenya (2024). Aidha, runinga ya Citizen ina umaarufu kwa kuwa, inapeperusha masuala yanayohusu maisha ya kila siku ya binadamu katika vipindi tofauti. Hata hivyo, utafiti lengwa haukuhusisha vipindi vyote vinavyopeperushwa na runinga ya Citizen. Mtafiti aliteua kimaksudi kipindi cha Sultana kilichopeperushwa kati ya saa moja na nusu jioni na saa mbili kamili usiku kila siku ya Jumatatu hadi siku ya Ijumaa na kurudiwa Jumamosi kuanzia saa kumi jioni, kwa sababu utafiti wa awali ulionyesha kuwa wahusika wenye ulemavu wamepewa nafasi muhimu katika kipindi hiki ikilinganishwa na vipindi vingine. Kipindi hicho kilipeperushwa kwa takribani mwaka mmoja na miezi minne kutoka mwezi wa Machi 2022 hadi mwezi wa Julai 2023.

Aidha, mtafiti alimhoji mtayarishaji wa kipindi cha Sultana ili kupata maoni yake kuhusu historia fupi ya kipindi cha Sultana, dhamira ya kipindi kwa watazamaji na mbinu za

maigizo zinazotumika na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen.

Mwisho, mtafiti aliwateua kimaksudi wahusika katika kipindi cha Sultana kwa kuzingatia majukumu waliyopewa katika kipindi hicho. Katika kipindi cha Sultana kuna aina mbalimbali ya wahusika. Hata hivyo, sio wahusika wote waliohusishwa kwenye utafiti lengwa. Wahusika waliotumikizwa katika utafiti huu ni walemavu wa viungo na wa tabia.

## 1.13 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya kukusanya data ni muhimu ili kuhakikisha usahihi na ufanisi wa utafiti. Matumizi ya vifaa sahihi husaidia kuimarisha uhalisi wa matokeo na kuongeza uaminikaji wa utafiti (Babbie, 2016). Data ilikusanywa kwa kutumia vifaa tofauti. Vifaa hivyo ni pamoja na matumizi ya simu ya rununu, tarakilishi, na mwongozo wa mahojiano.

### 1.13.1 Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Kothari (2004) ni muhimu kuchagua njia sahihi za ukusanyaji wa data kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti huu ulizingatia mbinu ya kukusanya data iliyofungamana moja kwa moja na suala, malengo na nadharia ya utafiti. Ili kupata data ya utafiti huu, mtafiti alitazama kipindi cha Sultana kisha akateua na kuorodhesha maneno na matendo ya wahusika walemavu katika kipindi. Vilevile, mtafiti alimhoji mtayarishaji na baadhi ya wahusika walemavu wa kipindi cha Sultana ili kupata data zaidi. Mtafiti alinakili majibu kutoka kwa mtayarishaji na baadhi ya wahusika walemavu wa kipindi cha Sultana wakati wa kujibu maswali. Mwisho, data zilizokusanywa zilinakiliwa, kusomwa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti.

### 1.13.2 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data huwa ni wa aina mbalimbali kutegemea utafiti unaohusika (Buliba na wengine, 2014). Utafiti huu ni wa kimaelezo na hivyo ulijikita katika kuchanganua hoja za utafiti. Data ilikusanywa nyanjani na kisha kuchanganuliwa kwa kurejelea malengo, maswali na nadharia husika. Majibu kutoka kwa mahojiano na mtayarishaji wa kipindi na baadhi ya wahusika walemavu wa kipindi cha Sultana yalinakiliwa, kupangwa kulingana na mwongozo wa maswali haya.

Awamu tatu zilizingatiwa wakati wa uchanganuzi wa data. Kwanza, data iliyokusanywa maktabani na nyanjani ilisomwa na kisha kuchanganuliwa kwa mbinu ya kimaelezo. Data hiyo ilihusisha kujadili maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Katika hatua ya pili, mtafiti alibainisha sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Aidha, katika hatua ya tatu mtafiti alifafanua mbinu za maigizo zinazotumika na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen.

### 1.13.3 Uwasilishaji wa Matokeo

Kwa mujibu wa Creswell (2013) ni muhimu kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa usahihi na kuyaweka wazi ili kuhakikisha yanaeleweka na kufahamiwa. Uwasilishaji wa matokeo ipasavyo utawawezesha wasomaji kuelewa muktadha wa utafiti na kufanya uchambuzi wao wenyewe. Matokeo yaliyotokana na uchanganuzi wa data yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa mujibu wa malengo na misingi ya nadharia. Uwasilishaji huu ulihusu maelezo ya vipengele ambavyo vilijitokeza katika kipindi cha Sultana katika runinga ya Citizen.

### 1.13.4 Maadili ya Utafiti

Utafiti wa Cohen na wengine (2007) ni msingi wa kuelewa maadili ya utafiti. Wanasema kuwa inafaa mtafiti aweke maslahi na haki za washiriki mbele. Hii itahakikisha kwamba utafiti unafanyika kwa njia inayofuata viwango vya maadili. Pia italeta usalama kwa washiriki na kutoa msingi imara kwa matokeo ya utafiti. Uchunguzi huu ulizingatia maadili mbalimbali. Kwanza kabisa mtafiti aliomba barua ya utambulisho kutoka Shule ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Kenyatta, kisha kibali kiliombwa kutoka kwa Baraza la Kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Vibali hivi vilikuwa vya kutujulisha kwa washirika katika utafiti. Barua ya kujitambulisha kwa watafitiwa ilitayarishwa na mtafiti. Mtafiti pia alihakikisha ameweka haki za watafitiwa kwa kuweka siri zao.

## 1.14 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia: usuli wa mada, suala, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka. Aidha, sura imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi na mihimili ya nadharia ya Maigizo na kueleza mbinu zilizotumika kwenye utafiti. Aidha, maadili ya utafiti yameelezwa. Sura inayofuata imeangazia maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana.

# SURA YA PILI

# MAUDHUI YANAYOWASILISHWA NA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA

## 2.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia iliangazia msingi wa utafiti huu. Katika kuangazia msingi wa utafiti, sura hiyo ilibainisha malengo ya utafiti na yaliyoandikwa kuhusu mada. Aidha, mihimili ya nadharia ya Maigizo ambayo iliongoza utafiti huu pia ilibainishwa. Sura hii inachambua lengo la kwanza la utafiti ambalo ni kujadili maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Ili kufanikisha kujadili maudhui, sura hii iliongozwa na mhimili wa nadharia ya Maigizo kuwa uigizaji unafaa kusawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi kiasi kuwa hadhira itaelewa kinachozungumziwa. Aidha, mawazo ya wataalam mbalimbali yametumika kushadidia matokeo ya utafiti. Sehemu ifuatayo inajadili maudhui yanayowasilishwa na wahusika katika kipindi cha Sultana. Pia, mwelekeo wa kipindi hiki kuhusu ulemavu umechanganuliwa. Kabla ya kufanya hivyo, mtafiti alidokeza usuli wa kipindi hiki na kueleza dhana ya maudhui. Usuli wa kipindi cha Sultana ni muhimu katika kukiweka katika mkabala wake. Maelezo kuhusu dhana ya maudhui ni muhimu katika kuielewa na kujenga msingi wa kuelewa namna maudhui yanavyojitokeza katika kipindi cha Sultana. Usuli na dhana zimeelezwa katika sehemu zifuatazo.

## 2.2 Usuli wa Kipindi cha Sultana

Kabla ya kuzama kwenye maudhui haya, ni muhimu kufafanua usuli wa kipindi cha Sultana ili wasomaji wakifahamu kwa mapana. Kwa mujibu wa data ya nyanjani

iliyopatikana kupitia mahojiano na mtayarishaji wa kipindi na baadhi ya wahusika wa kipindi hiki, asili ya kipindi hiki ni taifa la Mexico lililo katika bara la Amerika Kusini. Kipindi hiki kilikuwa kimepeperushwa kupitia kituo kimoja cha runinga katika taifa hilo kabla ya kusimilishwa na kupeperushwa kupitia runinga ya Citizen nchini Kenya. Mtayarishaji wa kipindi hiki alidokeza kuwa alivutiwa na dhamira ya kipindi hicho ya kuwapa shime na ari watu walio na ulemavu kujiona kama watu wengine, jambo lililomfanya kuandaa mikakati ya kukisimilisha kwa muktadha wa Pwani ya Kenya. Hasa, alivutiwa na jinsi mtayarishaji wa kipindi hicho alivyowatumia wahusika walemavu katika kuwasilisha maudhui. Uhalisia wa matukio mbalimbali katika jamii pia yalipewa kipaumbele.

Kupitia mahojiano na mtayarishaji wa kipindi, mikakati ya kukisimilisha kipindi cha Sultana ilianza mwezi wa Aprili mwaka wa 2020, miaka miwili kabla ya kipindi hicho kuanza kupeperushwa kwenye runinga ya Citizen. Mwanzo, mtayarishaji wa kipindi alikitazama kipindi hicho kilichoandaliwa katika mazingira ya taifa la Mexico. Kisha alishirikiana na wataalamu mbalimbali wenye ujuzi katika taaluma ya maigizo ili kupanga mikakati ya kukisimilisha kipindi hicho. Alitafuta waigizaji mbalimbali ili wachukue majukumu tofauti kwenye kipindi.

Katika mahojiano na baadhi ya wahusika wa kipindi hiki, ilibainika kuwa kabla ya kuteuliwa kama waigizaji, wahusika hao walikaguliwa ili kutathmini vipaji vyao vya uigizaji ili kutimiza dhamira ya mtayarishaji wa kipindi. Waigizaji hao walijulishwa kuwa walitakikana kuwa na vipaji vya hali ya juu kwa ajili ya kuwasilisha maudhui

ipasavyo. Hivyo basi, waigizaji waliteuliwa kulingana na vipaji vyao katika kazi ya uigizaji.

Aidha, mtayarishaji wa kipindi hiki alidokeza kuwa alikumbana na changamoto mbalimbali katika harakati za kutayarisha kipindi hiki. Kwanza, halikuwa jambo rahisi kuwapata wahusika wenye vipaji vya viwango vilivyokuwa vinahitajika katika kipindi hiki. Hali hii ngumu ilitokana na kuwa baadhi ya wahusika katika kipindi hiki ni walemavu, hivyo basi, walioteuliwa walitakikana kuigiza kama walemavu, japo kimaumbile si walemavu. Ilimchukua mtayarishaji wa kipindi muda mwingi katika kuwatayarisha waigizaji kuchukua majukumu yao mbalimbali, hasa wahusika walemavu. Waliochukua majukumu ya kuigiza kama walemavu wa viungo hawakuwa walemavu wa kihalisia hivyo basi, walichukua muda mwingi kujifunza kuigiza kama walemavu. Kwa mujibu wa Senkoro (1982), tabia za wahusika katika kazi za sanaa huibua dhamira. Hivyo basi, mtayarishaji wa kipindi alitilia maanani vipaji vya waigizaji ili atimize lengo lake ipasavyo.

Aidha, changamoto nyingine ilikuwa ni gharama ya juu kutokana na uwepo wa wahusika walemavu. Wahusika walemavu walihitaji vifaa vya kipekee vya kuigiza ambavyo ni vya gharama ya juu. Kwa mfano, mhusika Sultana ambaye aliigiza kama mlemavu wa macho alinunua vifaa kama vile fimbo maalum vilivyomsawiri kama mlemavu wa macho. Vilevile, mhusika Buya alinununua miguu bandia ya gurudumu kumwonyesha kama mlemavu wa miguu. Naye Kokani alinunua kifaa kilichofanya ngozi yake kuonekana kama iliyo na ulemavu.

Kupitia maigizo, mila na tamaduni za jamii zilibainika na kuendelezwa. Mandhari ya Kipindi cha Sultana ni pwani ya Kenya. Kwanza, hili lilichochewa na hali ya kuwa matukio mengi katika kipindi hiki yanaakisi hali halisi ya mazingira na utamaduni wa pwani. Kwa mfano jamaa kuishi pamoja, mavazi na vyakula vya Kimombasa yalidhihirika wazi kwenye kipindi. Pili, mazingira ya pwani yalisheheni utamaduni wa Waswahili. Kipindi cha Sultana kimesheheni utamaduni wa Waswahili ambao wanapatikana katika maeneo ya pwani. Hivyo basi, kwa kuchukua mazingira ya pwani, mtayarishaji wa kipindi alikipa kipindi uhalisia wa kimazingira wa Waswahili. Hii inaendana na mhimili wa nadharia ya maigizo kuwa, kupitia maigizo sharti mila na tamaduni za jamii zibainike na kuendelezwa. Kwa njia hii hadhira itahudumiwa kwa kufahamishwa masuala mbalimbali.

Kipindi cha Sultana kilipokelewa vizuri sana na watazamaji na ikapata umaarufu zaidi katika nchi za Afrika Mashariki. Kulingana na mtayarishaji wa kipindi hiki, walemavu halisi walikipokea vyema kipindi hiki kwa sababu mhusika mkuu, Sultana, ni mlemavu wa macho. Watazamaji walemavu walikiona kipindi hiki kama kilichokuwa na dhamira ya kutetea nafasi ya walemavu katika jamii na kupigania haki zao. Kwa kawaida katika jamii hasa nchini Kenya, walemavu hukumbana na changamoto nyingi hasa za unyanyapaa katika maisha yao. Walemavu aghalabu hubaguliwa katika masomo, nafasi za ajira, uongozi miongoni mwa masuala mengine muhimu katika jamii. Aidha, wakaaji wa Pwani pia walikipokea kipindi hicho vyema kwa sababu kilitumia mandhari ya eneo lao. Kwao, kipindi hicho kilisheheni uhalisia wa kimaisha wa wakaazi wa eneo lao. Vilevile, baadaye kipindi hiki kilipokelewa vyema katika maeneo mengine ya Kenya na nchi jirani kama vile Tanzania, Rwanda na Uganda. Zaidi ya hayo, kipindi hicho

kilisheheni mafunzo mbalimbali kwa wanajamii kama vile kusuta maovu yanayofanyika katika jamii na kusifia mambo mema.

**2.3 Dhana ya Maudhui**

Senkoro (1982) anaeleza kuwa maudhui katika kazi ya fasihi ama sanaa ni mafunzo ama mawazo yanayomsukuma msanii au mtunzi kutunga kazi ya sanaa. Senkoro anaendelea kufafanua kuwa maudhui katika fasihi ya Kiswahili yanajumuisha vipengele mbalimbali kama vile dhamira, falsafa, mgogoro, msimamo na ujumbe. Naye Mbarouk (1998) anaeleza kuwa maudhui ni kati ya mambo yanayokamilisha kazi ya sanaa. Jambo jingine linalokamilisha kazi ya sanaa ni fani. Maudhui ni ujumbe wa jumla unaodhihirika kutokana na kitu, tukio au wahusika kwenye kazi za kifasihi (Njogu na Chimerah, 1999). Maudhui ni muhimu katika kudhihirisha dhamira katika sanaa ya uigizaji. Kulingana na Kimani na Chimera, kazi ya fahisi haitungwi katika ombwe tupu bali kuna ujumbe, falsafa, mgogoro, dhamira au msimamo fulani unaozungumziwa na mtunzi na kufanikishwa na hadhira yake.

Senkoro (k.t) anaeleza kuwa dhamira ndio sehemu kuu ya maudhui. Katika kazi ya sanaa inayotumia lugha, dhamira huwa ni wazo kuu au jumla ya maana inayowasilishwa na mtunzi wa kazi hiyo na pia jumla ya maana inayopokelewa na hadhira. Kwa upande mwingine, falsafa ni wazo au mawazo ya kipekee yanayotambulisha kazi ya msanii fulani. Falsafa hubainika katika kazi mbalimbali za msanii. Senkoro (k.t) anaeleza mgogoro kama dhana inayotumiwa kurejelea mvutano kati ya wahusika mbalimbali au baina ya wahusika na nguvu nyingine za nje kwenye kazi za kifasihi. Kulingana na Senkoro, bila mgogoro basi kazi ya fasihi hukosa mtiririko unaofaa. Sehemu nyingine ya

maudhui inayoelezwa na Senkoro ni mtazamo wa msanii. Watunzi wa kazi za fasihi huwa na mitazamo isiyofanana kuhusu masuala mbalimbali katika jamii. Hivyo basi, ni rahisi kutofautisha mitazamo ya wasanii wawili kuhusu masuala mbalimbali ya jamii kupitia kazi zao.

## 2.4 Maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana

Sehemu hii imejadili maudhui mbalimbali yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Kuna aina mbili ya wahusika walemavu katika kipindi hiki: walemavu wa viungo na wa tabia. Wahusika walemavu wa viungo ni Sultana aliye na ulemavu wa macho, Kokani aliye na ulemavu wa ngozi na Buya aliye na ulemavu wa miguu. Wahusika walio na ulemavu wa tabia ni Fatima na Meja Jabali.

### 2.4.1 Maudhui Yanayotokana na Wahusika wa Viungo

Maudhui mbalimbali yanawasilishwa na wahusika wa viungo katika kipindi cha Sultana. Maudhui yanayowasilishwa na wahusika hawa ni maudhui ya bidii, mapenzi, ujasiri na unyanyapaa.

#### 2.4.1.1 Bidii

Maudhui ya bidii katika kipindi cha Sultana yanadhihirishwa na wahusika mbalimbali ambao ni walemavu wa viungo. Kwanza, bidii inadhihirishwa na mhusika mkuu katika kipindi hiki anayejulikana kama Sultana. Mhusika huyu alizaliwa na ulemavu wa macho. Hata hivyo, Sultana anaonekana kutia bidii katika shughuli zake ili aweze kujitegemea. Kwa mfano, Sultana hategemei msaada kutoka kwa mtu yeyote katika kufanya usafi wa kibinafsi kama vile kufua nguo. Aidha, Sultana anaonekana akitekeleza majukumu yake

ya nyumbani kama vile kuosha vyombo na kupika. Ili kujikimu kimaisha, Sultana anajihusisha na shughuli ya kuuza makombe anayookota kando ya bahari.

Mhusika mwingine mlemavu katika kipindi cha Sultana anayeonekana kuwa na bidii ni Buya. Mhusika huyu aliumia mguu baada ya kuvamiwa na majambazi, jambo lililomfanya alazimike kutumia miguu bandia iliyotengenezwa na magurudumu ya gari. Hata hivyo, Buya anaonekana akitoka nyumbani kwake kila asubuhi kuelekea kazini ili kukimu mahitaji yake na yale ya familia yake. Mhusika Kokani pia anaonyesha kuwa na bidii. Kokani ni mlemavu wa ngozi. Hata hivyo, hali yake ya ulemavu haikumfanya kuwa goigoi. Kokani anaonekana kuwa mwenye bidii nyingi katika masomo yake. Bidii yake ilimfanya kuhitimu vyema katika shule ya msingi na kujiunga na shule ya upili. Aidha, alitia fora katika shule ya upili na kujiunga na chuo kikuu ambapo alisomea taaluma ya udaktari. Kisha anahitimu katika taaluma yake na kuanza kuhudumia umma kama daktari.

Wahusika hawa watatu yaani Sultana, Buya na Kokani wanadhihirisha maudhui ya bidii katika kipindi cha Sultana. Kwa kurejelea nadharia ya Maigizo, uigizaji unafaa kusawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi kiasi kuwa hadhira itaelewa kinachozungumziwa. Ulemavu wa viungo upo katika jamii na kwa hivyo ni suala halisi linaloangaziwa katika kipindi cha Sultana. Hata hivyo, ulemavu wa viungo katika jamii aghalabu huhusishwa na uzembe (Wright, 2006). Katika kipindi cha Sultana, wahusika walemavu wamesawiriwa kama wenye bidii. Hali zao za ulemavu hazijawazuia kutia bidii kama binadamu wengine ili kukimu hali zao za maisha kifedha, kielimu, kikazi miongoni mwa hali nyinginezo.

Kwa mujibu wa Wright (2006), wahusika walemavu hukumbana na changamoto nyingi na ngumu wakilinganishwa na wahusika wa kawaida. Wahusika hawa sharti wakabiliane na changamoto hizi na kupigania nafasi zao katika jamii. Hivyo basi, ni rahisi jamii kuhusisha ulemavu na uzembe au kutojiweza. Mtazamo wa mtunzi wa kipindi hiki pia unabainika kuwa ulemavu haufai kuwa kisingizio cha kutokuwa na bidii na kufanikiwa maishani.

### 2.4.1.2 Mapenzi

Maudhui ya mapenzi yanaendelezwa na wahusika mbalimbali katika kipindi cha Sultana. Mhusika mkuu katika kipindi hiki ambaye pia ni mlemavu wa macho anaonekana kumpenda Jabali Junior ambaye ni mhusika asiye na ulemavu. Hali ya ulemavu inayomkumba Sultana haikumzuia Jabali Junior kumpenda. Mapenzi yao yanafikia kileleni pale wanapopanga na kufanya harusi kubwa. Wawili hao wanaoana na kuonekana kuishi maisha ya furaha. Aidha, tunaona pia Kokani akitaka uhusiano wa kimapenzi na Sultana. Licha ya kuwa Sultana hakumpenda Kokani, Kokani anaonekana kumjali Sultana kiasi kuwa hataki lolote baya limpate. Hili linadhihirika pale ambapo Kokani anamsomea vikali Kaka kwa kumpeleka Sultana katika shughuli za matembezi. Vilevile, Kokani anamwahidi Sultana kuwa angempa chochote alichotaka mradi tu akubali kuwa mke wake.

Katika upande mwingine, Buya ambaye ni mhusika mlemavu wa miguu anamwonya mwanawe anayejulikana kama Dida dhidi ya kuingia katika ndoa ya kulazimishwa. Hili linajitokeza pale ambapo Buya anaingilia kati mipango ya ndoa ya lazima kati ya Dida na Jabali Junior. Mkewe Buya ambaye ni Fatima anataka Dida aolewe na Jabali Junior.

Fatima na Meja Jabali ambaye ni baba wa kambo wa Jabali Junior walikuwa wamewapangia ndoa watoto wao. Buya anapinga ndoa hiyo vikali na kumjulisha mwanawe Dida kuwa hatakuwa na amani iwapo atalazimishwa kuolewa na mtu ambaye hampendi. Dida anaonekana kutilia maanani mawaidha ya babake kisirisiri. Jabali Junior naye hampendi Dida licha ya kuwa baba yake anampangia ndoa ya lazima na binti huyo.

Tukio hili linaonyesha utekelezaji wa mhimili wa nadharia ya Maigizo kwa kuwa uigizaji huu unasawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi kiasi kwamba hadhira inauhusisha moja kwa moja na changamoto za ndoa za lazima ambazo zinapatikana katika jamii. Mwigizaji Buya anaiga hali halisi inayokabili familia nyingi, ambapo wazazi hutaka kuwalazimisha watoto wao kuingia katika ndoa zisizo za hiari. Hivyo basi, uigizaji huu unawawezesha watazamaji kuelewa kinachozungumziwa kwa urahisi, na kuibua tafakari kuhusu madhara ya ndoa za kulazimishwa.

**2.4.1.3 Ujasiri**

Wahusika mbalimbali walemavu wanadhihirisha maudhui ya ujasiri katika kipindi cha Sultana. Kwa mfano, licha ya kuwa mlemavu wa ngozi, Kokani anaonekana kupinga maovu yanayofanyika katika jamii. Mwanakijiji mmoja tajiri kwa jina Meja Jabali alionekana akiwadhulumu watu wanyonge wakiwemo walemavu wa viungo. Meja Jabali anaonekana akiwanyang'anya wakulima wadogo mashamba na mifugo wao. Meja Jabali pia hakutaka upinzani wowote wa kibiashara kijijini. Alitaka awe mfanyibiashara wa kipekee katika uuzaji wa maziwa na mayai katika Kijiji chote. Kokani alijiunga na kundi la vijana lililokuwa likipingana na dhuluma hii. Hali yake ya ulemavu haikumzuia kutetea haki za wanyonge katika jamii.

Mhusika Sultana anatafuta majibu kuhusu asili na waliko wazazi wake kutoka kwa Bi. Salama. Bi. Salama alikuwa mkunga aliyemsaidia mamake Sultana wakati alipokuwa akijifungua nyumbani kwake. Bi. Salama alihusika katika kitendo kiovu cha kuwabadilisha Sultana na Jabali Junior wakati walipozaliwa na kuwakabidhi wazazi tofauti. Bi. Salama aliiweka siri hii kwa miaka mingi. Sultana anaonyesha ujasiri kwa kutafuta majibu haya licha ya kuelewa kuwa ni vigumu sana kuyapata. Aidha, Sultana ambaye ana ulemavu wa macho anaonyesha ujasiri wakati anapoelekea baharini akiwa peke yake. Kwa kawaida, Sultana angekuwa na msaidizi wa kumwelekeza ikizingatiwa kuwa baharini kuna hatari ya kusombwa na maji. Vilevile, Sultana anaonyesha kuwa ni jasiri kwani anatembea kijijini peke yake bila kuitisha msaada wowote. Anaonekana kujua njia zote kijijini. Haogopi kupotea njia au kudhulumiwa.

Mhusika Buya pia anaonyesha ujasiri. Baada ya kuvumilia kukaa kwenye ndoa ya msukosuko na Fatima, anachukua hatua ya kuitisha talaka. Fatima alikuwa amejaribu kumuua mumewe Buya mara ya kwanza lakini hakufaulu. Buya anaonekana kila mara akimwambia Fatima atie sahihi stakabadhi za talaka kati yao. Baada ya Fatima kutaka kumuua kwa mara ya pili, Buya anaamua kumfungulia kesi ili apatane na mkono wa sheria. Fatima anatiwa nguvuni na polisi siku ya harusi yake na Meja Jabali kwa jaribio la kutaka kumuua Buya. Buya anaapa kufanya lolote ili kuhakikisha amekomesha ukatili wa Fatima.

Kwa mujibu wa Njoroge (2018), wahusika walemavu husawiriwa kama walio na uwezo ama wenye utegemezi. Wahusika Sultana, Kokani na Buya wanaonyeshwa kama wahusika wenye uwezo, yaani hali zao za ulemavu hazijawazuia wao kudhihirisha ujasiri.

Kwa kawaida, wahusika walemavu husawiriwa kama wanyonge na wategemezi kwenye filamu au televisheni (Barnes, 1992). Hata hivyo, usawiri huo unaonekana kubadilika katika kipindi cha Sultana ambapo wahusika walemavu wa viungo wamepatiwa majukumu ambayo kwa kawaida hupewa wahusika wasio walemavu.

Hali hii pia inalingana na mhimili wa nadharia ya Maigizo ambapo uigizaji unalenga kusawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi ili hadhira iweze kuelewa kinachozungumziwa. Katika hali hii, Buya anaiiga kwa usahihi hali inayowakabili watu wengi maishani, yaani ndoa zenye misukosuko, ukatili wa kifamilia, na ujasiri wa kusimama kidete kudai haki kupitia vyombo vya sheria. Kwa njia hii, hadhira hutambua changamoto na suluhisho linalowezekana katika maisha halisi, hivyo kufanya ujumbe wa kipindi kueleweka kwa urahisi na kuakisi uhalisia wa kijamii.

#### 2.4.1.4 Unyanyapaa

Wahusika walemavu wa viungo katika kipindi cha Sultana wanakumbana na changamoto za unyanyapaa katika shughuli zao za kila siku. Mhusika mkuu katika kipindi hiki cha Sultana anakumbana na changamoto kwa kuwa ni mlemavu wa macho. Mfano wa unyanyapaa anaokumbana nao ni akiwa katika shughuli zake za kujitafutia riziki baharini. Akiwa katika harakati hizo, Sultana anakutana na watoto pale baharini wanaomkosea heshima na adabu kwa kumchokoza na kumcheka kwa kuwa hawaoni watoto hao. Watoto hao wanaonekana kumfanyia utani na kumwita majina mbalimbali ya kumdhalilisha. Aidha, Sultana anapokea majina ya masimango kutoka kwa wahusika wengine katika kipindi wanaoonekana kuwa na chuki na yeye. Kwa mfano, Fatima anamwita kipofu huku naye Meja Jabali akimwita kinyangarika. Jina kipofu ni la kumdhalilisha kwa

sababu ya hali yake ya ulemavu. Vilevile, jina kinyangarika ni la kumdharau kwa sababu ya hali yake. Fatima anasema Sultana anafaa afungiwe kwa sababu, kwa muonekano wake, anakaa mjuaji sana. Hii ni baada ya Sultana kugonga na kutawanyisha keki kimakosa kwenye sherehe. Salama anashikwa na kiwewe wakati Sultana anapoondoka katika sherehe hiyo na kukaa kwa muda mrefu bila kurudi nyumbani. Anamtafuta kwa kuwa anajua maisha yake yanaweza kuwa hatarini na huenda akaumizwa kwa sababu ya ulemavu wake wa kutoona.

Aidha, maudhui ya unyanyapaa yanadhihirika wakati jamaa wa Sultana wanaonekana kutaka kuchukua usukani wa shughuli za maisha yake. Sultana analalamikia hali ya jamaa zake kumpangia maisha yake. Kwa mfano, wanampangia jinsi anafaa kuishi, mambo anayofaa kutenda na mahali anafaa kuenda. Jamaa zake wanamwona kama mtu asiye na uwezo wa kujifanyia maamuzi bora kwa sababu ya hali yake ya kuwa mlemavu wa macho. Aidha, Fatima anamwona mumewe Buya kama mtu asiyefaa kupendwa kwa sababu ya hali yake ya kulemaa mguu.

Mhusika Kokani ambaye ni mlemavu wa ngozi anaonekana akitorokwa na watu ambao hawajazoea kuuona ulemavu wake. Ana kovu kubwa usoni mwake linaloonekana kuwa la kutisha. Kovu hili lilisababishwa na mkasa wa moto. Katika kazi yake ya udaktari, baadhi ya wagonjwa anaowahudumia pia wanaonekana kumwogopa na hata kumtoroka na kutafuta matibabu kwingine. Baada ya kugundua kuwa watu wanamwogopa na kumtoroka kwa sababu ya ulemavu alio nao, Kokani anaamua kutowapa wahudumu wenzake kama vile nesi nafasi ya kufanya kazi na yeye pale hospitalini. Anachukua hatua hiyo ili kuficha hali yake. Mara nyingi hulazimika kuvaa fulana yenye kofia

inayomfunika hadi usoni ili kuficha kovu hilo. Mtayarishaji wa kipindi cha Sultana alikuwa na haya ya kusema kupitia mahojiano kwenye dondoo lifuatalo:

> Baadhi ya wahusika katika kipindi hiki wanaigiza ulemavu kama vile Sultana ambaye pia ni mhusika mkuu katika kipindi hiki. Kutumia wahusika walemavu kama wahusika wakuu lilikuwa jambo la makusudi ili kuonyesha kuwa walemavu pia wana nafasi na uwezo sawa na watu wasio walemavu katika jamii. Licha ya hali zao zinazowafanya kuchukuliwa kama watu wasiojiweza, walemavu wana uwezo wa kushiriki katika masuala muhimu katika jamii na hata kujipatia riziki bila kutegemea msaada wa watu wengine (Data ya nyanjani, 2025).

Kwa kurejelea nadharia ya Maigizo, uigizaji unafaa kusawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi kiasi kuwa hadhira itaelewa kinachozungumziwa. Unyanyapaa dhidi ya watu walemavu ni suala linaloendelea kushuhudiwa katika jamii tofauti nchini Kenya. Mahenge (2017) alibaini kuwa watu walio na ulemavu hupewa majina ya kuwakebehi katika dunia halisi na katika utunzi wa kazi mbalimbali za kisanaa kama vile uigizaji. Mahenge anaeleza hivi:

> Kuna msigano wa majina wanayoitwa watu wenye ulemavu katika jamii, majina hayo kwa mujibu wa maelezo yao, yanaonekana kuwadhalilisha. Majina haya ni kama vile kiwete, kilema, kipofu, zeruzeru na taahira… (Mahenge, 2017, uk. 82).

Jambo hili pia linajitokeza katika kipindi cha Sultana ambapo wahusika walemavu wanaitwa majina ya kuwakebehi. Kwa mfano, Sultana anarejelewa kwa majina kama vile kipofu na kinyangarika. Aidha, utafiti wa Muguche (2022) ulidokeza kuwa katika jamii nyingi hasa nchini Kenya, unyanyapaa dhidi ya watu walemavu ni jambo lililokithiri.

### 2.4.2 Maudhui Yanayowasilishwa na Walemavu wa Tabia

Sehemu hii imejadili maudhui mbalimbali yanayowasilishwa na walemavu wa tabia. Wahusika walio na ulemavu wa tabia ni Meja Jabali na Fatima. Maudhui yanayojengwa na wahusika hawa ni ukatili, mauaji, uhalifu, tamaa na utabaka.

#### 2.4.2.1 Ukatili

Maudhui ya ukatili yanadhihirishwa na wahusika walemavu wa tabia katika kipindi cha Sultana. Mhusika anayejulikana kwa jina la Meja Jabali anadhihirisha maudhui haya pale anapomfungia mke wake anayejulikana kama Bi. Ua nyumbani asitoke nje. Meja Jabali alichukua uamuzi huo baada ya mkewe kupatwa na ugonjwa wa kiakili baada ya kujifungua. Hali hiyo ilimfanya mkewe kudhoofika kiafya. Kwa sababu hiyo, Meja Jabali alimuamrisha mfanyakazi wake anayejulikana kama Mwanzele amchunge mkewe asitoke nje na ikiwa angetaka kutoka basi sharti iwe ni kwa idhini yake pekee. Aidha, wakati Bi. Ua anazidiwa na ugonjwa wa kiakili, Meja Jabali anachukua hatua nyingine ambapo anamfunga mke wake miguu na mikono kwa kamba na kisha kumfunga kwenye kitanda. Vilevile, Meja Jabali anachukua hatua ya kumdunga mke wake sindano ya kumfanya alale kwa madai kuwa amechoshwa na kelele zake. Tabia hii ni ya ukatili kwani inaenda kinyume na haki za kimsingi za kibinadamu kama vile uhuru wa kutembea.

Maudhui ya ukatili pia yanajitokeza wakati Meja Jabali anawanyanyasa wafanyikazi wake. Kupitia mmoja wa wafanyikazi wa Meja Jabali anayejulikana kama Mwanzele, tunafahamishwa kuwa Meja Jabali anawadhulumu wafanyakazi wake. Kwa mfano, wakamaji maziwa hawaruhusiwi kunywa chai ya maziwa licha ya kuwa wao ndio

wanaowachunga na kuwakama ng'ombe wa Meja Jabali. Aidha, anaonyesha ukatili wakati ambapo anamchapa mmoja wa wafanyikazi wake anayejulikana kama Maneno kofi baada ya mfanyakazi huyo kukiri kuwa yeye ndiye aliyemleta Sultana kwenye sherehe ambayo Sultana aligonga na kuangusha keki ya sherehe hiyo. Anamwachisha kazi mfanyakazi huyo na kumuamrisha aondoke kwake mara moja. Meja Jabali pia alikataa kumlipa mfanyakazi huyo marupurupu yake licha ya kumfanyia kazi kwa muda mrefu.

Meja Jabali pia anaonyeshwa kuwa katili baada ya kugundulika kuwa alijinyakulia urithi wote kutoka kwa baba yake na kumwacha dadake Sada bila chochote, baada ya baba yao kuaga dunia. Sada aliishi maisha ya ufukara licha ya kuwa babake alikuwa tajiri. Sada anamweleza Jabali Junior kuwa Meja Jabali aligeuza urithi uliokuwa umeandikwa na baba yao na kujiandika kama mrithi wa kipekee wa mali ya baba yao.

Ukatili zaidi unabainishwa na mhusika Fatima. Mhusika huyu anatafuta majangili ambao anawalipa na kuwatuma wakamvamie na kumuua mumewe Buya. Majangili hao walimchapa, kumuumiza na kumlemaza Buya mguu wake kisha wakamfunga kwa karatasi na kumtupa ndani ya pipa wakidhani kuwa ameaga dunia. Wakati huo wote Buya alikuwa amepoteza fahamu. Buya alichukuliwa na lori la takataka na kupelekwa jaani, mahali panapoitwa Mwakifunge bila yeye kujua. Buya alikaa kwenye takataka kwa muda wa siku tatu kabla ya kuokolewa na Maria. Maria anampa malazi, anamlisha, anamvisha na kumuuguza kwa muda kabla ya kumuunganisha na familia yake. Kitendo cha Fatima kutaka kumuua mumewe kinadhihirisha maudhui ya ukatili.

Kwa mujibu wa nadharia ya Maigizo, jukwaa linalotumiwa na waigizaji sharti liwakilishe uhalisia. Katika dunia halisi, walemavu hupitia changamoto kwa sababu ya hali zao. Wright (2006) alibaini kuwa wahusika walemavu hupitia changamoto nyingi wanapopigania haki zao. "Wahusika walemavu hasa wa viungo katika kazi nyingi za fasihi wanaonekana kudharauliwa hasa na wahusika wasio walemavu jambo ambalo ni changamoto iliyo katika dunia halisi" (Wright 2006, uk. 20). Meja Jabali na Fatima ni wahusika wakuu ambao ni walemavu wa tabia katika kipindi cha Sultana. Wahusika hawa wanaonyesha ukosefu wa maadili katika jamii. Mara nyingi, wahusika walemavu wa tabia ndio huonyesha ukatili kwa wahusika wa viungo.

Kwa mujibu wa Traore (1972), maigizo ni vitendo vinavyotokana na uzoefu wa binadamu katika kukabiliana na maisha na vinavyoonyesha uhalisia wa maisha yaliyojaa changamoto na migogoro. Hali hizi halisi humpa mwigizaji fursa ya kutoa mchango wake katika kuwakilisha matatizo yanayowakabili jamii. Aidha, mwigizaji anaweza kutumia uigizaji kama njia ya kukosoa jamii yake, hasa inapokuwa na vitendo vinavyoonyesha athari mbaya.

#### 2.4.2.2 Mauaji

Wahusika katika kipindi cha Sultana wanabainisha maudhui ya mauaji. Mhusika Meja Jabali alimuua babake ili aweze kurithi mali yake. Alifanya hivyo baada ya kugundua kuwa babake hakuwa na nia ya kumrithisha mali yoyote. Mhusika Fatima alikuwepo wakati Meja Jabali alitekeleza unyama huo bali walikubaliana kuwa hangetoboa siri hiyo. Meja Jabali anamweleza Fatima kuwa angempa chochote ilmradi asitoboe siri hiyo kwa mtu yeyote.

Meja Jabali pia anamuua aliyekuwa mfanyakazi wake Maneno. Meja Jabali alifanya hivyo baada ya wanakijiji kwenda kwake kulalamikia kile walichokiita dhuluma dhidi yao. Wanakijiji hao walidai kuwa Meja Jabali alikuwa na mazoea ya kuwanyang'anya mashamba yao na mifugo na kukwepa kuwalipa. Meja Jabali alitoka nje ya nyumba yake akiwa ameshikilia bunduki na kuanza kuwafyatulia waandamanaji hao risasi. Hii ilisababisha kifo cha Maneno ambaye alikuwa mfanyakazi wake wa kitambo aliyekuwa amemfanyia kazi kwa muda mrefu.

Aidha, maudhui ya mauaji yanaendelezwa na Meja Jabali anayemuua Zuu. Zuu alikuwa ameenda kumtafutia Babu dawa ya miti shamba ambapo alipatana na Meja Jabali. Kulizuka vuta nikuvute baina yao. Katika harakati za kutaka kulipiza kisasi dhidi ya mauaji ya babake Maneno yaliyotekelezwa na Meja Jabali, Zuu anachukua jembe kwa lengo la kutaka kumvamia Meja Jabali nalo. Meja Jabali anamgonga kichwani na kumuua Zuu papo hapo. Anamdunga mguuni ili ionekane kana kwamba aliuwawa na sumu ya nyoka iliyomuuma. Fatima na Meja Jabali wanashirikiana kupanga njama ya kumuua Buya ambaye ni mumewe Fatima kwa kutumia majambazi ila hawakufaulu.

Kwa kurejelea nadharia ya Maigizo, jukwaa linalotumiwa na waigizaji sharti liwakilishe uhalisia ili hadhira iweze kutambua na kuelewa kwa urahisi ujumbe unaowasilishwa. Katika kipindi cha Sultana, tukio la mauaji linalohusisha Meja Jabali linaiiga hali halisi ya jamii ambapo baadhi ya watu hutumia ukatili, mauaji na vitisho vya kisheria au kijamii kama njia ya kulinda mali au kushikilia mamlaka. Uigizaji huu unafanikisha lengo la kuwasilisha maudhui kwa wepesi, kwani hadhira inatambua uhusiano kati ya tabia za wahusika na visa vya uhalifu vinavyojitokeza mara kwa mara katika jamii. Hivyo basi,

kupitia wahusika kama Meja Jabali, mtayarishaji hutumia uigizaji kusuta mienendo mibaya inayojitokeza katika maisha halisi na kuhamasisha hadhira kuhusu athari zake kijamii na kimaadili.

Kwa mujibu wa Mahenge (2017), katika jamii kuna watu ambao huenda kinyume na maadili ya jamii. Watu kama hawa huhusishwa na vitendo visivyo vya kawaida kama vile mauaji au unyanyasaji wa watu wengine. Katika kipindi cha Sultana, wahusika kama vile Meja Jabali wanatumia ubabe wao kutekeleza uovu kama vile mauaji kinyume na matarajio ya jamii.

#### 2.4.2.3 Tamaa

Maudhui ya tamaa pia yanabainishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Mhusika Fatima anaonyesha tamaa ya mali kwa kutaka bintiye anayejulikana kama Dida aolewe na mtoto wa Meja Jabali anayejulikana kama Jabali Junior. Juhudi za Fatima kutaka mwanawe aolewe katika familia tajiri zilianza wakati bintiye alipozaliwa. Meja Jabali ambaye ni baba wa kambo wa Jabali Junior pia alikubaliana na mpango huu. Vitendo vya Fatima vinaonyesha kuwa hatosheki na alichonacho. Aidha, anatafuta njia ya mkato ili kupata mali zaidi.

Vilevile, maudhui ya tamaa yanajitokeza wakati ambapo Fatima anataka kuolewa kama mke wa pili wa Meja Jabali ili aweze kupata mali yake. Fatima anajaribu kila awezalo kumshawishi Meja Jabali amuoe lakini anakosa kufaulu. Anapokosa kufaulu, Fatima anamlaghai Meja Jabali kwa kumlewesha wakiwa katika klabu ya burudani. Meja Jabali anakubali kutia sahihi cheti cha ndoa kati yake na Fatima na kubadilishana pete bila yeye kufahamu chochote kutokana na ulevi. Bila shaka, hii ni mbinu ya kutaka mgao wa mali

ya Meja Jabali ambayo alitamani kuwa nayo kwa muda mrefu. Kwa ujanja wake, Fatima alichukua video na picha ya tukio hili wakiwa kwenye klabu kama thibitisho kuwa Meja Jabali alikuwa ametia sahihi cheti cha ndoa kati yao. Licha ya kuwa Fatima si maskini, bado anataka mali zaidi. Hajatosheka na kile alicho nacho. Fatima ni mke wa Buya ambaye ni miongoni mwa watu wachache tajiri kijijini.

Maudhui ya tamaa pia yanajitokeza wakati Meja Jabali anamuua babake Mzee Jabali ili anyakue mali yake. Alimuua wakiwa nyumbani kwao baada ya kutoka katika kambi ya jeshi alipokua akifanya kazi. Sada ambaye pia ni mwanawe Mzee Jabali anakumbuka jinsi alivyompata babake akiwa amelala sakafuni nyumbani kwao akiwa ameaga dunia. Sababu ya Meja Jabali kumuua babake ni kutaka kurithi mali yake yote. Katika wosia wake, Mzee Jabali hakumrithisha Meja Jabali chochote kwa sababu alijua atafuja mali yote. Kwa hivyo, Mzee Jabali alimrithisha Sada mali yake yote. Kwa mujibu wa Sada, babake alimpigia simu akimwambia kuwa kuna dharura nyumbani. Alipofika pale alipata babake ashaaga dunia. Baada ya kutekeleza mauaji ya babake, Meja Jabali alitengeneza stakabathi ghushi na kubadilisha wosia wa babake.

Aidha, maudhui ya tamaa yanajitokeza wakati ambapo Meja Jabali ananunua samaki kutoka kwa wavuvi kwa bei ya chini sana na kuuza samaki hao kwa bei ghali ndio apate kutengeneza faida kubwa zaidi. Licha ya kuwa wavuvi wanalalamikia hali hii, Meja Jabali anawasuta na kudai kuwa hela alizokuwa akiwalipa zilitosha. Aidha, anawaona wavuvi hao kama wasiojua faida ya pesa.

Nadharia ya maigizo inadokeza kuwa uigizaji unafaa kusawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi kiasi kuwa hadhira itaelewa kinachozungumziwa. Ni bayana kuwa maudhui ya

tamaa yamejitokeza kupitia kwa wahusika mbalimbali kama vile Meja Jabali na Fatima ambao licha ya kuwa baadhi ya watu wanaomiliki mali nyingi wanaonekana kuwa na tamaa kiasi kuwa wanawanyang'anya hata wale walio na kidogo. Kulingana na Njoroge (2018, uk. 34), "maigizo katika vyombo vya habari ni picha ya masuala mbalimbali yanayofanyika katika jamii. Televisheni ni chombo muhimu cha kuwasilisha ujumbe katika jamii kupitia kwa programu mbalimbali." Tamaa ni moja kati ya mambo ambayo yamo katika jamii. Katika jamii halisi, kuna watu wenye tamaa ambao huwanyang'anya wanyonge mali yao.

#### 2.4.2.4 Utabaka

Maudhui ya utabaka kati ya maskini na tajiri pia yanadhihirishwa na wahusika katika kipindi cha Sultana. Familia ya Meja Jabali na ya Fatima ni ya tabaka la juu. Maisha yao hayawezi kulinganishwa na wanakijiji ambao wanaishi karibu na wao.

Wanaishi katika nyumba za kifahari, kuendesha magari ya kifahari, wanafanya kazi tajika na hata kuwa na watumishi wa nyumbani. Aidha, watoto wao wanasomea katika shule za kifahari. Meja Jabali alikuwa na cheo cha umeja jeshini. Meja Jabali anasema kuwa anataka kumjulisha Jabali Junior kwa mheshimiwa ili wabadilishane mawazo. Haya yote ni kwa ajili ya kudumisha uhusiano wa familia yake na watu mashuhuri. Katika sherehe ya kufuzu kwa mwanawe Jabali Junior, Meja Jabali anawaalika wageni kutoka familia tajiri pekee. Kitendo hiki kinaonyesha kugawanya watu kitabaka.

Naye Buya ambaye ni mumewe Fatima ni mhandisi na mkandarasi. Buya ni miongoni mwa watu wachache tajiri kijijini. Hii ndio sababu Fatima ambaye ni mkewe Buya anaonyesha utabaka ambapo hataki mwanawe Dida aolewe na mtu wa tabaka la chini,

yaani Kaka ambaye alitoka katika familia maskini. Kwa sababu hii, Fatima anamwita Kaka kijakazi mwenye hafai kumkaribia binti yake. Hii ni licha ya kuwa bintiye Dida alimpenda Kaka hata kama alikuwa anatoka katika familia maskini. Kulingana na Fatima, watu maskini wanafaa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wenzao ambao ni maskini huku tajiri nao wakiwa na uhusiano na tajiri wenzao.

Utabaka unabainika pale ambapo Meja Jabali anawadunisha wanakijiji na kuwaona kama watu wasiofaa. Anawanyang'anya mashamba na kudai kuwa yeye peke yake ndiye anaweza kufanya kazi ya ukulima na ya kuchunga mifugo vyema. Anaonekana akifanya biashara ya kuuza maziwa kijijini ambapo hataki upinzani kutoka kwa mtu yeyote hasa watu maskini wanaomzunguka. Kwa sababu hiyo, Meja Jabali anawadharau watu maskini ambapo anawaona kama wasiofaa kwake. Aidha, anawaona kama watu wazembe wasiojua jinsi ya kujitafutia riziki. Uwepo wa watu maskini na tajiri katika kipindi cha Sultana kunaonyesha utabaka uliopo kati ya maskini na tajiri.

Katika jamii halisi, kuna utabaka wa aina nyingi ukiwemo ule wa kati ya maskini na tajiri. Mtayarishaji wa kipindi cha Sultana amebainisha utabaka huu katika kipindi hiki kupitia wahusika walemavu wa tabia.

Kwa mujibu wa Karimi (2022), wahusika mbalimbali katika kazi za kisanaa kama vile maigizo hutumiwa ili kufanikisha maudhui ya msanii. Karimi anaeleza:

"Katika kazi ya fasihi, wahusika ni watu wanaowakilisha tabia za binadamu katika maisha halisi" (Karimi, 2022, uk. 44).

Wahusika walemavu wa tabia wametumiwa katika kipindi cha Sultana ili kubainisha maudhui ya utabaka katika jamii hasa utabaka kati ya maskini na tajiri. Inabainika katika

kipindi hiki kupitia wahusika walemavu wa tabia kuwa maskini hawafai kuoana na tajiri bali wanafaa kuwa na uhusiano na maskini wenzao.

Smith (2019) alibaini kuwa wahusika walemavu katika filamu mara nyingi hupewa majukumu ya chini ikilinganishwa na wahusika wasio walemavu. Hata hivyo, utafiti wa Smith unaonekana kutofautiana na jinsi ilivyo katika kipindi cha Sultana ambapo wahusika walemavu wanawakilishwa katika majukumu muhimu. Wahusika kama vile Sultana ambaye ni mlemavu wa macho amepatiwa majukumu sawa na wahusika wasio walemavu. Kwa mfano, Sultana ndiye mhusika mkuu katika kipindi cha Sultana na kupitia kwake, dhamira ya mtayarishaji wa kipindi na maudhui mbalimbali yanayowasilishwa katika kipindi yanajitokeza.

Wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana wanaonyeshwa kuwa na sifa ambazo kwa kawaida huhusishwa na wahusika wasio walemavu. Kwa mfano, Sultana ana uwezo wa kutekeleza majukumu ambayo aghalabu hayatekelezwi na watu walio walemavu wa macho katika ulimwengu halisi. Kokani ana uwezo wa kutia fora masomoni licha ya kulemaa ngozi. Naye Buya ana uwezo wa kutumia akili yake ipasavyo ili kufanya maamuzi bora licha ya kuwa mlemavu wa miguu. Majukumu mbalimbali waliyopewa wahusika walemavu wa viungo katika kipindi cha Sultana zinakifanya kipindi hiki kuwa na upekee. Hii ni tofauti na jinsi wahusika walemavu wa viungo wanavyosawiriwa katika vipindi vingine. Kwa mfano, katika kipindi cha Papa Shirandula kilichopeperushwa katika runinga ya Citizen, wahusika walemavu kama vile Mama Nyaguthii ambaye ni mlemavu wa miguu hawajapewa majukumu muhimu katika kipindi hicho. Aidha, katika kipindi cha *Mother-in-Law* pia katika runinga ya Citizen, wahusika walemavu

hawajapatiwa majukumu muhimu. Mhusika Salome katika kipindi hiki ambaye ni mlemavu wa miguu amepewa jukumu kama mhusika msaidizi. Hii ni tofauti na jinsi ilivyo katika kipindi cha Sultana.

### 2.5 Hitimisho

Sura hii imejadili maudhui mbalimbali yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Katika kujadili maudhui, sura hii imeongozwa na mihimili ya nadharia ya Maigizo. Utafiti umeonyesha kuwa kipindi hiki kilikuwa na wahusika walemavu wa viungo na wa tabia. Maudhui mbalimbali yamebainishwa kupitia kwa wahusika hawa. Wahusika walemavu wa viungo katika kipindi hiki ni Sultana ambaye ni mlemavu wa macho, Buya ambaye ni mlemavu wa miguu na Kokani ambaye ni mlemavu wa ngozi. Maudhui yaliyobainishwa na wahusika walemavu wa viungo ni kama vile maudhui ya bidii, mapenzi, ujasiri na unyanyapaa. Aidha, wahusika walemavu wa tabia ambao ni Meja Jabali na Fatima wamedhihirisha maudhui ya ukatili, mauaji, tamaa na utabaka. Kipindi hiki kinawaonyesha walemavu wa viungo kama wanaojiweza wala si wategemezi jinsi wanavyosawiriwa katika sanaa za maigizo au katika dunia halisi. Wahusika walemavu wa tabia wanaonyeshwa kama wanaochangia hali zisizofaa katika jamii.

# SURA YA TATU

# SIFA ZA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA

## 3.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia iliangazia maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kilichopeperushwa katika runinga ya Citizen. Sura hiyo ilibainisha maudhui mbalimbali yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi hicho. Sura hii inaangazia sifa mbalimbali za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana katika runinga ya Citizen nchini Kenya. Sifa za wahusika walemavu wa viungo na zile za walemavu wa tabia zimebainishwa na kuelezwa. Sifa za wahusika walemavu zimeshughulikiwa kwa sababu ni kupitia sifa hizo ambapo dhamira na maudhui ya kipindi yanajitokeza. Hivyo basi, kwa kuangazia sifa mbalimbali za wahusika walemavu, tutabainisha dhamira ya mtayarishaji na ujumbe aliokusudia kupitisha kwa hadhira yake. Katika kubainisha sifa hizo, mhimili wa nadharia ya Maigizo kuwa uigizaji unaomshirikisha mtendaji hai una ufanisi mkubwa kwa kuwa mtendaji huyo ana uwezo wa kufaragua vitendo vyake kwa ajili ya kutosheleza matakwa ya hadhira yake umetumikizwa. Aidha, mawazo ya wataalamu mbalimbali katika sanaa ya maigizo yamesaidia katika kubainisha sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana.

## 3.2 Sifa za Wahusika Walemavu wa Viungo katika Kipindi cha Sultana

Sifa mbalimbali zinabainika kutokana na walemavu wa viungo katika kipindi cha Sultana. Walemavu wa viungo ni binadamu wa kawaida na sifa zao si mahsusi kwao bali ni sifa zinazoweza kuhusishwa na watu wasio walemavu (Mungai, 2007). Walemavu wa viungo katika kipindi hiki ni Sultana aliye mlemavu wa macho, Buya ambaye ni mlemavu

wa miguu na Kokani aliye na ulemavu wa ngozi. Ili kubainisha sifa za wahusika hawa, mtafiti alitazama kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen iliyopeperusha kipindi hicho. Aidha, mtafiti alimhoji mtayarishaji wa kipindi hicho na baadhi ya wahusika walemavu. Vilevile, tunapata sifa za wahusika walemavu kutokana na jinsi wahusika wengine wasio walemavu wanavyozungumza kuhusu ulemavu na walemavu.

### 3.2.1 Sifa za Mhusika Sultana

Sultana ndiye mhusika mkuu katika kipindi cha Sultana. Kuna sifa mbalimbali zinazohusishwa na mhusika huyu. Aidha, sifa zake zinajitokeza kutokana na matendo yake na jinsi wahusika wengine katika kipindi wanavyozungumza kumhusu. Sifa hizo ni kama zifuatazo.

#### 3.2.1.1 Mkakamavu

Kupitia kwa matendo na lugha anayoitumia, Sultana anaonekana kuwa mhusika mwenye ukakamavu. Sifa ya ukakamavu inadhihirika kutokana na kuwa hali yake ya ulemavu au mazingira yake magumu hayajamfanya kupoteza matumaini maishani. Kwa mfano, Sultana anakataa kusaidiwa na ndugu zake katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kujikimu. Sultana anaweka mikakati mbalimbali ili kutimiza ndoto zake maishani na kuishi maisha ya kawaida kama watu wengine. Kwa mfano, mhusika huyu anaonekana kwenye ufuo wa bahari akijitafutia riziki kwa kuokota makombe baharini kisha kuyauza. Kwa kawaida katika jamii, Sultana hangekuwa na matumaini ya kufanikiwa maishani kwa sababu ya hali yake. Angetaka kusaidiwa katika kutekeleza majukumu yake.

Sifa hii pia inajitokeza wakati ambapo Sultana anaonekana akipambana na hali ngumu ya mazingira anamoishi. Mahali anapoishi Sultana pana vichochoro vingi ambavyo

vinaweza kumfanya akose kutembea na kufanya shughuli zake za kujikimu. Kwa mfano, Sultana anatembea kwa muda mrefu na wakati mwingine anapoteza mwelekeo akielekea baharini. Aidha, njia anazopitia zimesheheni aina kadhaa ya vizuizi. Njia hizo hazijawekwa lami au kutengenezwa kuwa laini. Hivyo basi, Sultana anatembea huku akijikwaa mara kwa mara lakini hili halimfanyi kukaa nyumbani na kungoja msaada. Hizi ni baadhi ya changamoto wanazozipitia walemavu wa viungo. Mungai (2007, uk. 167 – 168) anaeleza kuwa:

> "Majukumu wanayotekeleza walemavu ama wasiyoyatekeleza, mambo wanayofanyiwa au kukosa kufanyiwa yanatokana na mielekeo yao wenyewe kuhusu hali zao za ulemavu. Badala ya kujawa na shauku kuhusu hali zao, walemavu wanafaa kutafuta jinsi wanavyoweza kubadilisha mielekeo hasi kuwahusu katika jamii na kutafuta namna ya kujikimu jinsi alivyofanya mwanariadha maarufu nchini Kenya Wanyoike."

Mwanariadha Henry Wanyoike ni Mkenya ambaye ni miongoni mwa wanariadha waliobobea katika ulingo wa riadha duniani. Mwanariadha huyu alipoteza uwezo wake wa kuona akiwa umri wa miaka ishirini na moja. Licha ya kuwa na upofu, Wanyoike hakupoteza azma yake ya kuwa mwanariadha bora duniani. Aliweza kutimiza ndoto yake na kushinda mataji mbalimbali duniani na hata kuajiriwa kuwapa hotuba ya motisha wanafunzi nchini Kenya na mataifa ya kigeni yakiwemo Indonesia na Uingereza.

Katika kipindi cha Sultana, wahusika wengine wasio walemavu wanatamani kuwa na ukakamavu kama Sultana. Kwa mfano, Fatima anatamani bintiye Dida awe mkakamavu kama Sultana. Hili linajitokeza katika onyesho moja ambapo Fatima anajiuliza sababu za

Jabali Junior kumpenda Sultana wala si Dida, bintiye. Anasikika akisema "lakini Sultana hapendi kushindwa licha ya hali yake…". Kauli hii inaonyesha kuwa wahusika wengine wanamwona Sultana kama mkakamavu.

#### 3.2.1.2 Mwepesi wa Hasira

Mhusika Sultana anaonekana kuwa mwenye hasira kwa wahusika wengine sifa inayodhihirika kila wakati anapofanyiwa matendo yasiyomridhisha na aila yake. Sifa hii inadhihirishwa kutokana na tabia zake wakati anapokasirishwa. Kwa mfano, kila anapokasirika, Sultana anaonekana akilia sana na kutoweka nyumbani kwao. Sultana anakasirishwa na tabia za ndugu zake wanaosisitiza kumpangia kile anachostahili kufanya wala si anachokitaka yeye mwenyewe. Mara kwa mara Sultana anatafutwa na ndugu zake wanaohofia usalama wake kwa sababu ya hali yake ya upofu. Sultana anahusisha tabia za ndugu zake na unyanyapaa. Sultana anaona kuwa ndugu zake wanamchukulia kama mtu asiyejiweza na anayefaa kupewa msaada mara kwa mara, jambo ambalo Sultana halitaki. Aidha, huwa vigumu kumshawishi mhusika huyu kurudi nyumbani kwao anapokasirishwa na jamaa zake. Katika kipindi hiki, Sultana ana mazoea ya kusema maneno yanayoonyesha kuwa anajitakia kifo ili aila yake wapate amani. Hii inatokana na hisia alizonazo Sultana kuwa jamaa wake hawamthamini na hivyo basi kifo chake kitawapatia amani. Kauli anazotoa Sultana zinaonyesha kuwa hapendi unyanyapaa anaoonyeshwa na ndugu wake wa karibu. Kisaikolojia Sultana anajihisi kuwa mzigo kwa familia yake.

Aidha, Sultana anaonekana akipasua zawadi aliyoletewa na Kokani wakati alipokuja kumwomba Sultana posa. Sultana alipasua zawadi hiyo baada ya kukasirishwa na tabia

ya Kokani ya kutomjulisha mapema kuwa angeleta posa. Ni bayana pia kuwa Sultana hakuwa anataka uhusiano wa kimapenzi na Kokani. Hata hivyo, Sultana hakumjulisha Kokani moja kwa moja kuwa hakuwa anataka uhusiano wa kimapenzi naye. Badala yake anamkasirikia Kokani na hata kuonekana kumkwepa au kukataa zawadi anazomletea kwa kisingizio kuwa hakumjulisha kuwa angemnunulia na kumletea zawadi hizo. Aidha, katika mahojiano na mtayarishaji wa kipindi, ilibainika kuwa Sultana ni mwepesi wa hasira. Mtayarishaji wa kipindi alikuwa na haya ya kusema katika dondoo lifuatalo:

> Sultana anonekana kukasirika kwa haraka. Tulimpa sifa hii maksudi kwa sababu ya hali yake ya upofu. Aghalabu, Sultana anakumbana na changamoto nyingi katika shughuli zake za kila siku. Katika jamii, watu walio na ulemavu wanaonekana kukerwa na tabia ya watu wasio na ulemavu kutoheshimu hali zao. Sultana anakumbana na watu wanaomkosea heshima kwa sababu ya hali yake jambo linalomfanya kukasirika haraka (Data ya nyanjani, 2025).

Kupitia kwenye dondoo hili, inabainika kuwa mtayarishaji wa kipindi alikuwa na mtazamo kuwa walemavu wa viungo hukerwa na unyanyapaa hivyo basi mara nyingi wao huonekana wakipandwa na mori kwa haraka. Hili linajitokeza kupitia kauli anazotoa Sultana wakati amekasirika. Kwa mfano, katika onyesho moja, Sultana anasema "kila wakati mnaniona kama mzigo kwenu, heri nife niwaondokee…". Sultana anatoa kauli hizi mara kwa mara akiwa amekasirishwa na ndugu zake. Kafka (1990) anaeleza kuwa wakati mwingine walemavu wa viungo hukosa kujithamini kutokana na unyanyapaa wanaopitia. "Kuna athari nyingi za kisaikolojia zinazotokana na ulemavu. Athari mbaya

zaidi ni kutojikubali na kutojithamini. Kwa kukosa kujithamini, mlemavu hujitwika mgizo wa kujidharau mwenyewe" (Kafka, 1990, uk. 90).

**3.2.1.3 Muwajibikaji**

Sifa ya uwajibikaji inajitokeza kutokana na matendo na maneno anayotumia mhusika Sultana. Kwanza, Sultana anapenda familia yake. Sifa hii inajitokeza wakati ambapo Sultana anaonekana akiwashughulikia ndugu zake katika kuandaa chakula na kuwasaidia katika kazi nyingine za nyumbani kama vile kuwafulia nguo, kuosha vyombo vya jikoni na kufagia nyumba bila malalamishi yoyote kuwa angetaka wajifanyie kazi hizo. Sultana anaonekana akifanya kazi hizo kwa hiari, tena kwa furaha kuwa anatoa msaada kwa familia yake licha ya kuwa na upofu. Ndugu zake Sultana walimchunga asije akapatwa na mabaya kwa sababu walimwona kama msichana mwenye upendo kwao.

Aidha, Sultana anaonyesha sifa ya kujali maslahi yake ya kiakili wakati ambapo anaonekana kukerwa na tabia ya Kokani aliyekuwa anataka urafiki wa kimapenzi naye. Kokani alikuwa na mazoea ya kumfungia Sultana chumbani mwake kwa kisingizio kuwa Sultana angefanyiwa matendo maovu na wanaume wengine kwa sababu ya upofu wake kwa kumbaka au hata kumuua. Sultana alikatiza uhusiano wake na Kokani na kumwonya asimkaribie tena. Sultana anatafuta mapenzi kwa mtu ambaye angeelewa hali yake na kumthamini jinsi alivyo. Hii ilipelekea Sultana kupatana na Jabali Junior na kuanza uhusiano wa kimapenzi naye. Ni kutokana na mapenzi baina ya Sultana na Jabali Junior ambapo Jabali Junior anamsaidia Sultana kuona tena baada ya kumtafutia daktari wa macho. Sultana alifanyiwa upasuaji wa macho ambapo hali yake ya upofu iliweza kurekebishwa kwa gharama ya juu sana. Jabali Junior aligharamia uponyaji huo. Haya

yote ni kwa sababu ya mapenzi kati yao. Kutokana na jinsi alivyompenda Jabali Junior, Sultana alikubali posa yake na kuonyesha kufurahia kufunga ndoa rasmi naye. Katika mahojiano na mtayarishaji wa kipindi, ilibainika kuwa upendo ni moja kati ya sifa kuu za mhusika Sultana. Mtayarishaji wa kipindi alisema haya kwenye dondoo lifuatalo:

> Sultana ndiye mhusika mkuu katika kipindi hiki. Sifa zake ni muhimu kwa sababu ndizo zinazodhihirisha lengo la kipindi. Mhusika huyu ana upofu lakini anapendana na mmoja kati ya wahusika wanaotoka kwenye familia tajiri zaidi katika kipindi hiki. Nia ya kufanya hivi ni kuondoa dhana na mazoea katika jamii kuwa walemavu wa aina yoyote hawawezi kupendwa na watu wasio walemavu hasa matajiri (Data ya nyanjani, 2025).

Kulingana na dondoo hili, Sultana ni mmoja kati ya wahusika wakuu katika kipindi hiki. Hivyo basi, sifa zake zina mchango mkubwa katika kuendeleza maudhui ya kipindi. Katika mahojiano kupitia simu na Sultana, ilibainika kuwa alikuwa na jukumu muhimu katika kufanikisha dhamira ya mtayarishaji, hivyo basi sifa zake zilitiliwa maanani. Hili linajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Ni kweli kuwa mimi nilikuwa mhusika mkuu katika kipindi cha Sultana. Hiyo ndiyo maana pia nilipatiwa jina la kipindi. Kukasirika kwangu kwa ghafla na mara kwa mara kulipangwa ili kuakisi uhalisia uliopo katika jamii. Ni kweli kuwa katika hali halisi walemavu hupitia changamoto nyingi ikilinganishwa na watu wasio walemavu. Changamoto hizi hasa ile ya unyanyapa huwafanya walemavu kukasirikia si tu watu bali hata ulimwengu unaowazunguka. Yaani wanakasirikia kila kitu. Kipindi cha Sultana kilichukua mwelekeo tofauti kidogo ambapo

kiliwapa wahusika walemavu sifa za kijasiri ambazo kwa kawaida hupewa wahusika wasio walemavu (Data ya nyanjani, 2025).

Katika dondoo hili, Sultana amefafanua kuwa hasira zake za mara kwa mara ziliundwa kimakusudi ili kuakisi uhalisia wa changamoto zinazowakumba walemavu katika jamii. Hali hii inalingana na mhimili wa nadharia ya maigizo, kuwa uigizaji unaomshirikisha mtendaji hai humpa nafasi ya kufaragua vitendo vyake kwa ubunifu ili kuyalinganisha na matarajio ya hadhira.

Kwa mujibu wa Muguche (2022), aghalabu wahusika walemavu husawiriwa kama wanyonge. Kwa maana hiyo, wahusika walemavu katika kazi za sanaa aghalabu hudokeza sifa zinazowafanya wao kuonekana wanyonge. Kwa kawaida, sifa kama vile ya ukakamavu hupewa watu wasio na ulemavu. Hii ni tofauti na jinsi ilivyo katika kipindi cha Sultana ambapo mhusika Sultana ambaye ni mlemavu wa macho anapewa sifa ya ukakamavu. Hii ni kinyume na matarajio katika jamii nyingi hasa nchini Kenya. Naye Njoroge (2018) anadai kuwa kusawiriwa kwa wahusika walemavu kwenye vyombo vya habari kunaweza kuwa na athari chanya au hasi kuwahusu. Iwapo wahusika watasawiriwa kama wakakamavu basi kuna uwezekano mkubwa jamii husika kuwa na mtazamo chanya kuwahusu. Njoroge (k.t) anaendelea kueleza kuwa kuwasawiri wahusika walemavu kwa njia hasi kama vile kuwa na hasira kunaweza kuzua mtazamo hasi katika jamii husika. Aidha, uponyaji wa Sultana unaonyesha kuwa hali ya ulemavu ni telezi. Mungai (2007, uk. 166) anafafanua kuwa “ulemavu unaweza kusababishwa na jambo lolote au kutokea wakati wowote kwa mtu yeyote.” Aidha, ulemavu pia unaweza

kutoweka jinsi ilivyomfanyikia Sultana ambaye hali yake ya ulemavu ilitoweka baada ya kutibiwa.

### 3.2.2 Sifa za Mhusika Kokani

Kokani ni mmoja kati ya walemavu wa viungo katika kipindi cha Sultana. Ni mhusika aliye na ulemavu wa ngozi. Zifuatazo ni sifa za mhusika huyu.

#### 3.2.2.1 Mbinafsi

Binadamu yeyote mlemavu au asiye na ulemavu anaweza kuwa mbinafsi. Kulingana na Kamusi ya TUKI toleo la tatu (2013), ubinafsi ni hali ya mtu kujipenda mwenyewe na kujifikiria zaidi kiasi kuwa anakosa kutambua mahitaji ya watu wengine. Licha ya kuwa mlemavu wa ngozi, Kokani ni binadamu wa kawaida kama wale wasio walemavu ambaye anaweza kuwa na sifa mbalimbali. Sifa ya ubinafsi inabainika kutokana na hulka za Kokani. Kwa mfano, mhusika huyu hataki Sultana awe na uhusiano wa kimapenzi na mtu mwingine bali yeye tu. Mara kwa mara anaonekana kughadhabika anapomwona Sultana na mtu mwingine. Ili kumzuia Sultana kukutana na kuchumbiwa na mtu mwingine, Kokani anapanga na Bi. Salama kuwa Sultana awe akienda kwake kwa ajili ya masomo ya kimsingi na ya ziada. Hata hivyo, Kokani ana nia nyingine tofauti ambayo ni kumleta Sultana karibu naye ili amshawishi kimapenzi. Kokani anaonekana akimlewesha Sultana na hata kumfungia chumbani kwake ili asitoke nje wala kurudi nyumbani kwao. Kokani anamfungia Sultana chumbani mwake na kwenda katika shughuli zake za kikazi na matembezi. Sultana anabaki chumbani akijiongelesha huku akiteta na kukasirikia hali hii. Tabia hii inaonyesha kuwa Kokani hajali fikra au maslahi ya Sultana bali anayapa mahitaji yake pekee kipaumbele. Aidha, Sultana anaonekana akimweleza Bi. Salama

kuwa Kokani wakati mwingine huwa mkali kana kwamba anammiliki kama mali yake binafsi. Kokani anamwambia Sultana kuwa hamtii, kumaanisha kuwa anamsikiliza mwanamume mwingine ambaye Kokani anasema kuwa ni lazima amkomeshe. Mwanamume huyo ni Jabali Junior ambaye Sultana anaonekana kumpenda kwa dhati. Ili kuvunja uhusiano kati ya Sultana na Jabali Junior, Kokani anajaribu kumshawishi Sultana arudishe nguo alizonunuliwa na Jabali Junior. Hii ilikuwa njama ya Kokani ya kuwakosanisha Sultana na Jabali Junior ili yeye apate nafasi ya kuwa na Sultana. Aidha, Kokani anafurahia posa kati ya Jabali Junior na Dida ili Jabali Junior akae mbali na Sultana.

**3.2.2.2 Mpweke**

Kokani hapendi kutangamana na watu wengine. Anapenda maisha ya upweke. Haonekani akitangamana na watu jinsi ilivyo na wahusika wengine. Mhusika huyu hana rafiki wa karibu ambaye anaweza kumweleza mawazo yake. Anaonekana kuwa na wakati mgumu kutengeneza urafiki. Kwa mfano, katika kutafuta uhusiano na Sultana, Kokani anamtumia Bi. Salama ili amwongeleshe Sultana kwa niaba yake. Katika mazungumzo yake na Bi. Salama, Kokani anaonekana kusitasita kumweleza kile anachotaka kwa Sultana. Anatumia maneno machache mno kumweleza kuwa angetaka uhusiano wa kimapenzi na Sultana. Anatangamana na Bi. Salama kwa muda mchache na anaonekana kuficha uso wake. Anazungumza na Bi. Salama huku akiangalia upande mwingine. Bi. Salama anamjulisha Sultana kuwa Kokani angependa kumpa masomo ya kimsingi ili Sultana asije akagundua nia ya Kokani. Sultana anapomtembelea Kokani yeye hana habari kuwa Kokani alikuwa na nia tofauti na kile alichokuwa ameambiwa na Bi. Salama. Aidha, Kokani hakumwambia Sultana moja kwa moja nia yake mahsusi ya kumtaka nyumbani

kwake bali alimwachia Sultana jukumu la kutafakari na kung'amua nia hiyo. Kisa hiki kinamwonyesha Kokani kama mpungufu wa maarifa na ujuzi wa kijamii unaomfanya mtu kutangamana na watu wengine.

Aidha, sifa ya upweke inajitokeza wakati Kokani anawakwepa wafanyikazi wenzake. Kokani ni daktari lakini hapendi kufanya kazi na wahudumu wenzake kama vile Nesi. Badala yake, Kokani anaonekana kufanya kazi wakati ambapo madaktari wengine wameondoka hospitalini. Katika harakati za kuwatibu wagonjwa, Kokani anakosa kupiga gumzo na wao. Anawatibu kisha kuondoka haraka haraka na kujifungia katika chumba cha madaktari au hata kuelekea nyumbani kwake. Sifa hii inaonekana kuchangiwa na hali yake ya ulemavu wa ngozi. Hivyo basi, kwa kuogopa unyanyapaa, Kokani hapendi kuonyesha uso wake kwa watu wengine. Anavalia nguo iliyo na kofia anayotumia kuficha uso wake. Anafunua uso wake akiwa nyumbani kwake ambapo anajitazama kwenye kioo mara kwa mara kwa imani kuwa ngozi yake itapona na kuwa kama ya watu wengine.

Wahusika wengine katika kipindi cha Sultana pia wanamwona  Kokani kama mpweke. Kwa mfano, katika onyesho moja, Bi. Salama anasikika akimwambia Sultana kuwa Kokani hana marafiki wengi kwa sababu hapendi mambo mengi. Lakini hii si sababu mahsusi ya Kokani kupenda kuwa mpweke. Kokani anapenda upweke kwa sababu hataki watu wengine waone ulemavu wake wa ngozi.

Akizungumzia sifa za mhusika Kokani, mtayarishaji wa kipindi alikiri kuwa mhusika huyu amepatiwa sifa ya kujitenga na watu wengine katika jamii. Mtayarishaji alikuwa na haya ya kusema kwenye dondoo lifuatalo:

> Kokani ni mhusika asiye na mahusiano ya kawaida na wanajamii wengine. Yeye hupenda kujifanyia shughuli zake bila kuitisha usaidizi wa mtu mwingine. Hata akiwa na suala linalomsumbua ni adimu yeye kujieleza. Katika jamii, walemavu wa viungo huwa na tabia kama ya Kokani kwa kuogopa unyanyapaa (Data ya nyanjani, 2025).

Ni dhahiri kupitia dondoo hili kuwa Kokani hapendi kutangamana na watu wengine katika jamii. Kwa kurejelea mhimili wa nadharia ya maigizo kuwa uigizaji unafaa kusawiri uhalisia wa maisha kwa wepesi kiasi kuwa hadhira itaelewa kinachozungumziwa, ni dhahiri kuwa mtayarishaji wa kipindi cha Sultana alitaka kusawiri hali halisi ya maisha kupitia kipindi hiki. Uhalisia huo ni kuwa wakati mwingine walemavu wa viungo hujitenga na wanajamii wengine na hata kujifungia katika makazi yao kwa sababu ya kuogopa unyanyapaa (Kafka, 1990, uk. 90). Kwa mujibu wa Mutugu (2019), wahusika walemavu hutumiwa kuwasilisha maudhui na dhamira ya mwandishi. Hivyo basi, wahusika hutwikwa sifa mbalimbali zinazowabainisha ili kuwasilisha maudhui. Aidha, hali hii inaakisi maelezo ya mhimili wa nadharia ya Maigizo kuwa uigizaji unaomshirikisha mtendaji hai humpa nafasi ya kufaragua vitendo vyake kwa ubunifu ili kuyalinganisha na matarajio ya hadhira.

### 3.2.3 Sifa za Mhusika Buya

Buya ni mhusika mlemavu wa miguu katika kipindi cha Sultana. Mhusika huyu ana sifa mbalimbali zinazombainisha. Sifa za Buya ni kama zifuatavyo:

#### 3.2.3.1 Mvumilivu

Licha ya kuwa katika ndoa yenye dhuluma na Fatima, Buya alivumilia kukaa katika ndoa hiyo. Katika kipindi hiki, Buya anakejeliwa na kutusiwa na mkewe Fatima kwa muda mrefu. Kuna kipindi ambacho Buya alifilisika na hivyo kushindwa kulipa mikopo yake ya benki. Katika harakati za kutaka kurejesha pesa walizomkopesha Buya, benki moja ilitumia dalali kwa nia ya kutwaa na kupiga mnada mali ya Buya. Dalali wanafika nyumbani kwa Buya wakiwa na barua mkononi na kumjulisha kuwa wametumwa kutwaa nyumba yake na gari lake. Mkewe, Fatima anamkejeli huku akimuuliza yeye ni mwanamume wa aina gani anayeshindwa kulipa mkopo. Anavumilia madhila haya na kuwa na matumaini kuwa shwari itarejea. Alimwomba meneja wa benki ampe muda wa kulipa mkopo wake lakini hakufaulu kuongezewa muda. Alikosa wa kumsaidia hata wale aliowasaidia wakati alikuwa na pesa. Anasikika akisema kuwa asante ya punda ni mateke.

Baada ya kutimuliwa nyumbani kwake, mkewe alimtoroka. Naye Buya aliishi bila makao na hata kulala kwenye mapipa ya kutupa taka baada ya kuumizwa na majambazi waliotumwa na Fatima kumuangamiza. Baadaye aliokolewa na Maria aliyempeleka kwenye makao yake ambayo yalikuwa duni. Hata hivyo, Buya ambaye alikuwa amezoea maisha ya kifahari alilazimika kuvumilia hali jinsi ilivyokuwa nyumbani kwa Maria. Buya analala sakafuni na kula chakula duni na wakati mwingine kukosa chakula kabisa. Licha ya kupitia masaibu haya yote, Buya anaonyesha kuwa mvumilivu. Haya yote yanaonyesha kuwa mlemavu anaweza kuishi maisha ya kawaida kama mtu yeyote.

#### 3.2.3.2 Mwenye Hekima

Buya ni mwenye hekima. Aghalabu, anaonekana kumwelekeza binti yake Dida dhidi ya kupea pesa kipaumbele katika ndoa. Mamake Dida ambaye ni mkewe Buya alitaka bintiye aolewe katika familia tajiri ya Meja Jabali. Hii ni licha ya kuwa Dida hakuwa anampenda Jabali Junior aliyetoka katika familia tajiri ya Meja Jabali. Buya anatofautiana na mkewe Fatima anayeonekana kulazimisha ndoa kati ya bintiye Dida na Jabali Junior. Buya anasema kuwa ndoa sharti ijengwe katika msingi wa mapenzi wala si pesa. Anasema kuwa atahakikisha bintiye, Dida, ameolewa na mtu anayempenda yeye wala si kulazimishwa kuolewa na mtu yeyote kwa sababu ya pesa. Buya anamshauri Dida asifuate ushauri wa watu wasiomjali akiwemo mama yake kwani mwishowe watakuwa wa kwanza kumcheka wakati ndoa yake itakapoporomoka.

Katika tukio jingine, Buya anaamua kumpa mkewe Fatima talaka baada ya wao kukosa kuafikiana kuimarisha ndoa yao.  Japo Fatima hakubaliani na talaka kati yake na mumewe, Buya anashikilia msimamo wake na kusema kuwa hilo ni jambo la busara kufanya badala ya kuishi katika ndoa ya mateso. Aidha, Buya anajizuia kujibizana na mkewe licha ya kutusiwa na kudharauliwa kila wakati. Anapandwa na mori lakini anajizuia kufanya vitendo ambavyo vinaweza kumfanya kujuta baadaye kama vile kumchapa mkewe.

Kutokana na sifa za Buya, ni bayana kuwa mlemavu anaweza kuishi maisha kama mtu yeyote asiye na ulemavu. Kwa mfano, anaweza kuoa, kuajiriwa, kuchukua mikopo na kulipa. Hili ni funzo kuwa unyanyapaa dhidi ya walemavu hauna nafasi katika jamii.

Njoroge (2018) anaeleza kuwa uwasilishaji wa wahusika walemavu katika vipindi vya televisheni unaweza kuwa wa mchanganyiko. "Wahusika hawa wanaweza kuwasilishwa kama walio na uwezo au nguvu ya kufanya jambo fulani au kama wategemezi." (Njoroge, 2018, uk.33). Mhusika Buya amewasilishwa kama mwenye uwezo wa kiakili licha ya kuwa mlemavu. Kwa mfano, Buya anaonyeshwa kama mtu mwenye hekima. Aidha, Buya anaonyeshwa kama mtu mvumilivu. Si mtu wa kukata tamaa licha ya kukumbana na changamoto nyingi katika maisha yake. Anadhihirishwa kama mtu anayefanya maamuzi bora.

### 3.3 Sifa za Walemavu wa Tabia

Walemavu wa tabia katika kipindi cha Sultana ni watatu. Hawa ni pamoja na Meja Jabali, Fatima na Kaka. Mtafiti alitazama kipindi cha Sultana katika runinga ya Citizen na kumhoji mtayarishaji wa kipindi hiki pamoja na baadhi ya wahusika ili kubaini sifa za wahusika hawa. Sifa za wahusika hawa ndizo zinazowabainisha kama walemavu wa tabia.

#### 3.3.1 Sifa za Meja Jabali

Meja Jabali ni mmoja kati ya wahusika wakuu walio na ulemavu wa tabia katika kipindi cha Sultana. Sifa zake ni kama zifuatazo.

##### 3.3.1.1 Mwenye Taasubi ya Kiume

Meja Jabali ana taasubi ya kiume. Sifa hii inajitokeza mwanzoni mwa kipindi ambapo Meja Jabali anadai kuwa mkewe atajifungua mtoto wa kiume. Hii ni licha ya kuwa hakuwa amefahamishwa na daktari kuwa mkewe atajifungua mtoto wa jinsia gani. Aidha, Meja Jabali anasikika akisema kuwa mtoto wa kiume ndiye mtoto anayeweza kumfanya

kuheshimiwa na kuonekana kama fahari. Mkewe alijifungua mtoto wa kike ambaye ni Sultana lakini akabadilishiwa na kupewa mtoto wa kiume aliyemwita Jabali Junior. Watoto hawa walizaliwa wakati mmoja lakini mama ya mtoto wa kiume aliaga dunia baada ya kujifungua. Njama ya kumbadilishia mtoto ilifanywa na kijakazi wa Meja Jabali aliyejulikana kama Asiya akishirikiana na Bi. Salama ambaye alikua mkunga.

Kuwa na mtoto wa kiume kulimpa Meja Jabali furaha kubwa iliyomfanya kufanya uamuzi wa kuandaa sherehe kubwa ya kuzaliwa kwa mwanawe. Meja Jabali hakujua kuwa mtoto aliyedhani kuwa wake hakuwa wake kibayolojia. Mkewe, Bi. Ua pia hakuwa na uhakika kuwa mtoto huyo alikuwa wake jambo lililomfanya kukosa amani. Kila wakati alishuku kuwa mtoto wake alikuwa wa kike wala si wa kiume. Meja Jabali alimpa jina mtoto wake aliyebadilishiwa Jabali Junior na kusema kuwa mtoto huyo atakuwa na tabia kama zake na ndiye atakayerithi mali yake. Katika mahojiano na Meja Jabali yaliyofanyika kupitia kwa njia ya simu, mhusika huyo alisema kuwa alipewa jukumu la kuigiza masuala ambayo yanaenda kinyume na matarajio ya jamii. Hata hivyo, masuala hayo yapo katika jamii hivyo basi ilikuwa muhimu kuyashughulikia katika kipindi ili kuhamasisha jamii dhidi ya mambo hayo. Meja Jabali alikuwa na haya ya kusema katika dondoo lifuatalo:

> Jukumu langu katika kipindi lilikuwa kuigiza kama mtu ambaye anafanya mambo kinyume na matarajio katika jamii. Katika jamii kuna kila aina ya watu. Kuna watu walio na tabia tunazoweza kusema ni njema na kuna wale walio na tabia mbaya. Mimi ni kati ya wahusika wanaoakisi watu walio na tabia zisizokubalika katika jamii. Tabia kama vile kuwanyang’anya watu wengine mali yao kulinipa

> sifa ya mhusika mbaya. Lakini haimaanishi kuwa mimi ni mhalifu katika maisha yangu ya kawaida. Yale ni maigizo tu (Data ya nyanjani, 2025).

Kupitia dondoo hili, inabainika kuwa Meja Jabali alipatiwa jukumu la kuigiza kama mhusika mwenye tabia zisizokubalika katika jamii, yaani mhusika mlemavu wa tabia. Hivyo basi, sifa zake nyingi zinafuata mkondo wa kumsawiri kama mhusika anayekosa maadili ya jamii anayotoka. Sifa hizo ni kama kuwa katili au mtu anayeshabikia jinsia ya kiume huku akiwabagua watu wa jinsia ya kike.

**3.3.1.2 Katili**

Meja Jabali ana sifa ya ukatili. Sifa hii inajitokeza kutokana na vitendo vyake mbalimbali vya kikatili dhidi ya wahusika asiokubaliana nao. Katika tukio moja, Meja Jabali anampata Sultana shambani mwake akichuma matunda. Wafanyakazi wa Meja Jabali ambao ni Kaka na Mwanzele walikuwa wamemruhusu Sultana kuchuma matunda. Meja Jabali anamsingizia Sultana kuwa ni mwizi wa mbuzi na ng'ombe wake na kumpa adhabu ya kufagia zizi lote la ng'ombe. Jitihada za Sultana kujitetea kuwa alikuwa ameruhusiwa kuchuma matunda ziliambulia patupu. Kaka na Mwanzele walijaribu kumweleza Meja Jabali ukweli kuwa Sultana si mwizi lakini pia wao hawakufaulu. Meja Jabali hakuripoti kwenye kituo chochote cha polisi kuwa Sultana amemwibia matunda yake wala kumshtaki afunguliwe mashtaka ya wizi.

Aidha, Meja Jabali anawatuma majangili kumvamia Kokani nyumbani kwake baada ya Kokani kukosana na mtoto wake ambaye ni Jabali Junior. Kokani anavamiwa kwa kuchapwa na kujeruhiwa na majangili hao. Jabali Junior hakuwa na habari kuwa babake alikuwa amewatuma watu wamvamie Kokani. Meja Jabali anajipiga kifua na kusema

kuwa mtu yeyote akicheza na familia yake sharti ampe adhabu. Anachukulia sheria mikononi mwake licha ya kuwa kuna vituo vya sheria.

Pia, Meja Jabali anaangamiza familia ya mfanyakazi wake wa muda mrefu aliyejulikana kama Maneno. Kwanza, Meja Jabali anamuua Maneno kwa kumfyatulia risasi. Maneno alikuwa kati ya waandamanaji waliokuwa wakipinga dhuluma dhidi yao kutoka kwa Meja Jabali. Kisha Meja Jabali anamuua mtoto wa Maneno aliyejulikana kama Zuu. Hii ni baada ya Meja Jabali na Zuu kukutana msituni ambapo Zuu alikua akimtafutia Babu dawa ya kienyeji, kisha vurugu ikatokea baina yao. Meja Jabali anamzidi Zuu nguvu na kumuua. Kisha anamdunga mguu ili ionekane kuwa Zuu alikufa kutokana na sumu ya nyoka. Katika mahojiano na mtayarishaji wa kipindi, ilibainika kuwa Meja Jabali ni mhusika mkuu mwenye ulemavu wa tabia katika kipindi hiki. Mtayarishaji wa kipindi alikuwa na haya ya kusema:

> Meja Jabali ni mhusika mkuu katika kipindi cha Sultana aliye na tabia zinazoenda kinyume na matakwa ya jamii. Ni kweli kuwa Meja Jabali ni katili. Hata mali aliyonayo hakupata kwa njia halali bali alijinyakulia mali hiyo kwa kumuua baba yake. Pia, anashiriki katika vitendo vya kuwanyang'anya watu mali yao ili ajitajirishe zaidi huku wengine wakiendelea kuwa maskini (Data ya nyanjani, 2025).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa sifa alizopewa Meja Jabali ni za kufanikisha maudhui ya kipindi, hali inayokubaliana na maelezo ya mhimili wa nadharia ya Maigizo kuwa uigizaji unaomshirikisha mtendaji hai una ufanisi mkubwa kwa kuwa mtendaji huyo ana uwezo wa kufaragua vitendo vyake kwa ajili ya kutosheleza matakwa ya hadhira yake.

Kwa mujibu wa Traore (1972), maigizo hujengwa katika migogoro inayosheheni uhalisia wa kimaisha. Aidha, mhimili wa nadharia ya Maigizo kuwa jukwaa linalotumiwa na waigizaji sharti liwakilishe uhalisia, Meja Jabali anasawiriwa kuakisi uhalisia uliopo katika jamii. Katika jamii kuna watu walio na sifa kama za Meja Jabali. Meja Jabali ana mivutano na wahusika mbalimbali katika kipindi cha Sultana. Katika maisha halisi kuna mivutano mbalimbali kati ya watu. Katika kipindi cha Sultana, mivutano hii ndio inayodhihirisha dhamira ya mtayarishaji wa kipindi hiki na kufanikisha maudhui.

### 3.3.2 Sifa za Mhusika Fatima

Fatima ni mmoja kati ya wahusika walemavu wa tabia. Ana sifa mbalimbali zinazobainisha ulemavu wake wa tabia. Sifa hizo ni kama zifuatazo:

#### 3.3.2.1 Mdanganyifu

Fatima anaonyeshwa kuwa mhusika mdanganyifu. Katika tukio moja, mhusika huyu anadanganya familia ya Meja Jabali kuwa bintiye Dida ana mimba aliyopajikwa na Jabali Junior, mwanawe Meja Jabali. Hii ilikuwa njama ya kutaka kumshawishi Jabali Junior kumuoa Dida na kuachana na Sultana ambaye alimpenda kwa dhati. Baada ya Jabali Junior kusema kuwa sharti wafanyiwe vipimo vya uzazi ili kubaini kama ni kweli Dida ana mimba, Bi Fatima anamshawishi Dida adanganye kuwa amepoteza ujauzito huo.

Fatima pia anaficha barua ya maagano kati ya Sultana na daktari wa macho ili Sultana asitibiwe macho. Anapoulizwa anadanganya kuwa hajui chochote kuhusu barua hiyo. Fatima pia anamnyang’anya Sultana mkufu wa thamani kutoka shingoni. Inapokisiwa kuwa ni yeye yuko na mkufu huo, anaupeleka kwa Jabali Junior na kumdanganya kuwa

aliupata kwenye begi lake na hajui ni nani aliuweka pale. Ili kujitoa lawama, anawasingizia Sada na Bi.Ua.

Katika tukio jingine, Fatima anahojiwa na polisi kuhusu kuvamiwa kwa Buya na wahuni. Fatima anadanganya kuwa Buya alikua akishiriki katika shughuli haramu na pengine wahuni aliojishughulisha nao ndio walimvamia wakiwa na nia ya kumuua. Hata hivyo, Fatima ndiye aliyekuwa amewatuma wahuni hao kumvamia Buya.

### 3.3.2.2 Mwenye Tamaa

Fatima anaonekana kuwa mwenye tamaa katika kipindi cha Sultana. Katika tukio moja, Fatima ambaye ni mke wa Buya anataka pia kuwa mke wa Meja Jabali. Anapanga njama ya kumlazimisha Meja Jabali kumuoa na kuachana na Bi.Ua. Meja Jabali ni mume wa Bi.Ua. Hii ni baada ya mipango yake na Meja Jabali ya kuwaoza Jabali Junior na Dida kugonga mwamba. Fatima anatoroka kwake na kuenda kuishi kwa Meja Jabali. Nia ya kutaka ndoa na Meja Jabali ni kujinyakulia mali ya Meja Jabali. Hii ni licha ya kuwa Fatima hakuwa maskini. Ana tamaa ya kutaka mali zaidi hata kama atawaacha wengine na umaskini.

Vilevile, Fatima anamchochea Meja Jabali dhidi ya mkewe, Bi. Ua na kusababisha mateso yake kutoka kwa Meja Jabali. Kwa mfano, Fatima ndiye aliyemshauri Meja Jabali amfungie mkewe kwenye banda la mbwa, licha ya kuwa afya yake ya kiakili ilikuwa imezorota. Fatima alifanya hivyo ndio apate nafasi ya kumlaghai Meja Jabali mali yake.

Katika tukio jingine, Fatima anamkejeli Bi. Ua kwa kudai kuwa hivi karibuni atakuwa malkia katika nyumba ya Meja Jabali na kwamba Bi. Ua atakufa maskini. Kiini cha Fatima kumwangamiza Bi. Ua ni tamaa ya kuwa mke wa Meja Jabali. Tukio hili

linaonyesha wazi kuwa Fatima hakuridhika na ndoa yake na alitaka kuharibu ndoa kati ya Meja Jabali na Bi. Ua ili atimize matakwa yake binafsi.

Kupitia mahojiano na mtayarishaji wa kipindi, ilibainika kuwa wahusika walipewa sifa mahsusi ili kufanikisha maudhui ya kipindi. Mtayarishaji alieleza kuwa Fatima ni mmoja wa wahusika wenye tabia zisizokubalika katika jamii, na alipewa sifa hizo ili kuakisi hali halisi ya maisha ambapo watu hutumia uongo, njia za mikato na hata mauaji ili kufanikisha tamaa zao za mali. Hili linajitokeza katika dondoo lifuatalo:

> Fatima ni mmoja kati ya wahusika walio na tabia zisizokubalika katika jamii. Alipewa sifa hizi ili kuakisi hali halisi katika jamii. Katika jamii kuna watu walio na mienendo kama ya Fatima. Kuna watu hutumia uongo na njia za mikato ili wapate mali. Hata kuna watu wanaoshiriki katika mauaji kwa ajili ya mali. Hii inaletwa na tamaa wanazokuwa nazo binadamu (Data ya nyanjani, 2025).

Dondoo hili linaashiria kuwa wahusika katika kipindi cha Sultana wamepewa sifa za pekee zinazowawezesha kutimiza majukumu yao katika kuwasilisha maudhui. Mutugu (2019) anaeleza kuwa taswira za wahusika walemavu wa tabia hutumika kufanikisha maudhui kwa njia yenye mvuto wa kisanaa.

Kwa hivyo, uwasilishaji wa Fatima kama mdanganyifu na mwenye tamaa ya mali ni utekelezaji wa mhimili wa nadharia ya maigizo unaosisitiza kuwa uigizaji sharti uwe wa ubunifu na utumie mbinu mbalimbali kama vile kuundwa kwa sifa mahsusi za wahusika kwa ajili ya kutosheleza matakwa ya hadhira.

### 3.3.3 Sifa za Mhusika Kaka

Kaka ni miongoni mwa wahusika wanaosawiriwa kama wahusika walemavu wa tabia katika kipindi cha Sultana. Zifuatazo ni sifa za mhusika huyu.

#### 3.3.3.1 Mkaidi

Kaka anajitokeza kama mhusika mkaidi katika kipindi cha Sultana. Sifa hii inajitokeza kupitia matukio mbalimbali katika kipindi hiki. Kwa mfano, Bi. Salama ambaye ni mlezi wa Sultana anamkanya Kaka dhidi ya kumtembeza Sultana. Hata hivyo, Kaka anafanya kinyume na jinsi anavyoagizwa. Anamtaka Sultana kimapenzi. Sultana naye hamtaki kwa sababu tayari ana mahusiano ya kimapenzi na Jabali Junior. Kaka anajifanya kutembea baharini ilmradi akutane na Sultana ambaye ana mazoea ya kwenda baharini kutafuta makombe. Kaka pia humpeleka Sultana nyumbani kwa Meja Jabali kula matunda.

Katika tukio jingine, Kaka anaonyesha kuwa mkaidi wakati anampeleka Sultana kwenye sherehe nyumbani kwa Meja Jabali kinyume na masharti ya Meja Jabali kuwa shehere zake zinahudhuriwa na watu walioalikwa pekee. Kaka alikuwa anajua masharti haya kwa sababu alikuwa mfanyakazi wa Meja Jabali lakini aliyapuuza.

Aidha, Kaka anadhihirisha ukaidi wakati ambapo anafika kazini kwa Meja Jabali akiwa amechelewa ama wakati mwingine kukosa kufika kabisa. Anaonywa mara nyingi dhidi ya tabia hii lakini habadilishi mwenendo wake. Hii inasababisha ugomvi wa mara kwa mara baina yake na babake anayejulikana kama Mwanzele. Aidha, Kaka anamkaidi Jabali Junior ambaye ni mtoto wa mwajiri wake anapomwomba amtayarishie boti la kutumia. Hata hivyo, sifa hii haijitokezi kwa mhusika huyu pekee bali pia inajitokeza kwa baadhi ya wahudumu katika maisha ya kawaida.

#### 3.3.3.2 Mchochezi

Kaka anaonyesha kuwa mchochezi. Katika tukio moja, Kaka anamwambia Jabali Junior kuwa Dida hampendi ndio maana havai pete yake. Dida na Jabali Junior walikuwa wachumba. Hata hivyo, huu si ukweli kwani pete aliyokuwa amevalia Dida ilianguka na kuzama kwenye sinki alipokuwa akiosha vyombo. Alijaribu kuitoa pete hiyo lakini akashindwa na kuiacha hapo. Kaka alijua kilichofanyika lakini akaamua kumdanganya Jabali Junior kwa matumaini kuwa watakosana na Dida ili apate fursa ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Dida. Jambo hili lilisababisha ugomvi kati ya Dida na Jabali Junior.

Aidha, uchochezi wa Kaka unaonekana wakati anamwambia Sultana kuwa Kokani ni mnafiki na kuwa hampendi. Hakuwa anataka kumwona Sultana akiwa na Kokani au hata kumtembelea. Nia ya Kaka ni kuwakosanisha ili apate nafasi ya kuwa na Sultana, kwani alikua na hisia za kimapenzi naye.

Kwa mujibu wa Karimi (2022), wahusika walemavu hufanikisha maudhui na kufaulisha dhamira katika kazi za maigizo. Sifa alizonazo Kaka za ukaidi na uchochezi ziliteuliwa maksudi na mtayarishaji wa kipindi ili kufanikisha maudhui ya kipindi. Sifa za Kaka zinathibitisha maelezo ya mhimili wa nadharia ya Maigizo kuwa mtendaji katika kazi za maigizo ana uwezo wa kufaragua vitendo vyake kwa ajili ya kutosheleza matakwa ya hadhira yake. Aidha, Goodland (1971) anaeleza kuwa maigizo yana lengo la kuelimisha na kuonya jamii kuhusu masuala mbalimbali katika jamii. Katika kipindi cha Sultana, sifa za ukaidi na uchochezi zimewasilishwa ili kuonyesha kuwa kuna watu walio na sifa kama hizi katika jamii. Mtayarishaji pia anaonyesha kuwa sifa kama hizi hazifai.

### 3.3.4 Tathmini ya Sifa za Wahusika

Kipindi cha Sultana kinaonyesha kuwa walemavu wa viungo ni kama binadamu wengine wasio walemavu. Hivyo basi, walemavu wanaweza kufanya chochote kama mazingira na miundo msingi ya jamii itawawezesha. Kwa mfano, wanaweza kutia bidii masomoni na kufuzu katika taaluma mbalimbali sawa na watu wasio walemavu. Hivyo basi, sifa zao kama za watu wasio walemavu tunaokabiliana nao maishani. Sifa hizo zinaweza kuwa nzuri au hasi.

Aidha, walemavu wanaweza kukabiliana na hali ngumu za maisha kama vile mazingira magumu jinsi wanavyofanya watu wasio walemavu. Kwa upande mwingine, walemavu wa tabia wanaweza kusaidiwa kubadilisha tabia kupitia vituo mbalimbali vya kurekebishia tabia ili waweze kuwa na tabia faafu.

Kupitia kipindi hiki, pia inajitokeza kuwa ulemavu si kutotekeleza. Walemavu wanaoshindwa kutekeleza pengine wamekosa nafasi au hawajawezeshwa na miundo msingi ya jamii ili waweze kutekeleza.

Pia, kupitia kipindi cha Sultana inadhihirika kuwa unyanyapaa hauna mantiki. Ni bayana kuwa ulemavu unaweza kuathiri kwa namna tofauti mahusiano katika jamii na shughuli mbalimbali. Walemavu hupitia changamoto mbalimbali katika maisha yao ya kila siku. Hata hivyo, walemavu ni kama watu wengine wasio walemavu na hivyo basi unyanyapaa dhidi yao hauna msingi. Walemavu waruhusiwe kama wanajamii wengine kuishi maisha ya kawaida.

## 3.4 Hitimisho

Sura hii imeangazia na kubainisha sifa mbalimbali za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kilichopeperushwa katika runinga ya Citizen. Ili kubainisha sifa za wahusika, sura hii imeongozwa na mhimili wa nadharia ya Maigizo kuwa uigizaji unaomshirikisha mtendaji hai una ufanisi mkubwa kwa kuwa mtendaji huyo ana uwezo wa kufaragua vitendo vyake kwa ajili ya kutosheleza matakwa ya hadhira yake. Aidha, maelezo ya wataalamu mbalimbali yalitumikizwa katika kuchambua sifa za wahusika hao. Vilevile, data ya nyanjani iliyopatikana kutokana na mahojiano na mtayarishaji wa kipindi na baadhi ya wahusika yalitumika. Utafiti umebainisha sifa mbalimbali za wahusika walemavu wa viungo na wale wa tabia. Sifa zilizobainishwa kwa wahusika walemavu wa viungo ni kama vile mhusika Sultana aliye mkakamavu, mwepesi wa hasira na muwajibikaji. Kokani alibainika kuwa na sifa za ubinafsi na upweke ilhali Buya alibainika kuwa na sifa za uvumilivu na hekima. Nao wahusika walemavu wa tabia walibainisha sifa mbalimbali. Meja Jabali alidhihirishwa kuwa na sifa za kuwa na taasubi ya kiume na kuwa katili. Naye Fatima alionekana kuwa mdanganyifu na mwenye tamaa. Mwisho, Kaka alionekana kuwa mkaidi na mchochezi. Wahusika hawa wamepatiwa sifa hizi kimakusudi ili kufaulisha dhamira ya mtayarishaji wa kipindi na vilevile kufanikisha maudhui mbalimbali katika kipindi cha Sultana.

# SURA YA NNE

# MBINU ZA MAIGIZO ZINAZOTUMIWA NA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA

## 4.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilibainisha sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Miongoni mwa mihimili ya maigizo ni kuwa maigizo sharti yafanywe kwa ubunifu kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuvutia hadhira. Kila uigizaji unafaa kuishawishi hadhira kuuzingatia na ni kwa njia hiyo pekee utakavyoweza kufanikisha mawasiliano. Sura hii inafafanua mbinu za maigizo zinazotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kilichopeperushwa katika runinga ya Citizen nchini Kenya. Katika kufafanua mbinu hizo, sura hii itaongozwa na mihimili ya nadharia ya Maigizo. Vilevile, maelezo ya wataalamu mbalimbali katika fasihi simulizi hasa kipera cha maigizo yamesaidia katika ufafanuzi wa mbinu hizo za maigizo. Pia, data kutoka nyanjani iliyohusisha mahojiano baina ya mtafiti, mtayarishaji wa kipindi na wahusika katika kipindi cha Sultana ilichanganuliwa na matokeo yake kuwasilishwa.

## 4.2 Mbinu za Maigizo

Wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana wametumia mbinu mbalimbali za maigizo katika kufaulisha dhamira na kufanikisha maudhui ya kipindi. Mbinu za maigizo walizotumia ni kama vile kufananisha, ishara za mwili, mazungumzo na mielekeo ya wahusika. Mbinu hizi ni kama zilivyojadiliwa katika sehemu zifuatazo. Stanislavski na Benedetti (2009) wanaeleza mbinu mbalimbali za kuigiza ambapo wanasema kuwa katika uigizaji, mwigizaji ni mwanafalsafa na pia mchungaji wa hisia. Mwigizaji hujiuliza

maswali kama vile mimi ni nani? Niko wapi? Ni lini? Nataka nini? Nitapataje ninachokitaka? Ni upungufu gani ninaostahili kupunguza? Miongoni mwa maswali mengine. Ni kupitia maswali kama haya ambapo mwigizaji hupata kufahamu mbinu anazofaa kutumia ili kufaulisha dhamira ya kipindi na kufanikisha maudhui. Mbinu walizotumia waigizaji walemavu katika kipindi cha Sultana zimefafanuliwa katika sehemu zifuatazo.

### 4.2.1 Kufananisha

Schechner (1988, uk. 31) anaeleza kuwa kuigiza ni sanaa ya kufananisha. Hii inamaanisha kuwa mwigizaji hufanya mambo jinsi ambavyo mambo hayo yanavyofanywa na mtu mwingine. Kwa mfano, mwigizaji anaweza kumithilisha jambo fulani linavyotendwa au jinsi jambo hilo lilivyo. “Mwigizaji anaweza kuiga ulemavu, ugonjwa, tabia, taaluma kama vile ualimu, udaktari au vitendo halisia vya mtu fulani” (Mutegi, 2010: 2). Kuigiza humfanya mwigizaji kuonekana kama mtendaji halisi wa mambo anayoyaigiza. Wahusika walemavu na wasio walemavu wametumia mbinu ya kufananisha ili kufanikisha maudhui mbalimbali katika kipindi cha Sultana. Wahusika wote katika kipindi cha Sultana wakiwemo walemavu wa viungo na wa tabia wanashiriki katika kuigiza masuala mbalimbali yanayotendeka katika ulimwengu halisi. Maigizo ya wahusika hawa yanatumika katika kufaulisha maudhui mbalimbali kama vile unyanyapaa, bidii, utabaka, ukatili na ujasiri katika kipindi hiki.

Sultana anajifananisha na mlemavu wa macho. Hili linajitokeza kutokana na jinsi macho yake yanavyoonekana na matendo yake. Macho ya Sultana yanaonekana meupe kwa kukosa irisi na pupili, sehemu muhimu za macho ambazo humwezesha binadamu kuona.

Kupitia vitendo vyake, Sultana anaonekana kama mlemavu wa macho. Sultana anaonekana kutumia vifaa vya kuigiza vinavyomfanya aonekane kama mtu aliyepofuka. Ametia vifaa hivyo kwenye macho yake yanayoonekana kana kwamba yamepofuka. Kitendo hiki ni cha kujifananisha na mtu aliyepofuka katika hali halisi. Aidha, wakati mwingine Sultana anaonekana akitumia fimbo ya kutembelea ili imsaidie katika matembezi yake kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hata hivyo, Sultana si mlemavu wa macho katika maisha halisi. Katika ulimwengu halisi, kuna watu ambao ni walemavu wa macho. Sultana pia anaigiza kama mlemavu wa macho asiyetegemea watu wengine kukidhi mahitaji yake. Katika maonyesho kadhaa, Sultana anaonekana akiwa baharini akitafuta makombe anayoyauza kwa watengenezaji wa mapambo ya vito. Kitendo hiki kinamwonyesha Sultana kama mtu mwenye bidii licha ya kuwa na ulemavu wa macho. Ili kufananisha matendo yake na yale ya ulimwengu halisi, Sultana anazama katika wadhifa anaoigiza na kuonekana kama aliyepofuka. Katika mahojiano na Sultana, mhusika huyu alidokeza kuwa yeye si mlemavu wa macho katika maisha yake ya kawaida. Sultana alikuwa na haya ya kusema katika dondoo lifuatalo:

> Mimi si kipofu katika hali yangu ya kawaida. Kuigiza kama mtu aliyepofuka ni jukumu nililopatiwa na mtayarishaji wa kipindi. Halikuwa jambo rahisi kuigiza kama mlemavu. Nilichukua muda mwingi mno kujitayarisha kwa sababu kama mhusika mkuu katika kipindi, nilihitajika kuonekana kama mtu asiye na uwezo wa kuona (Data ya nyanjani, 2025).

Kupitia dondoo hili tunapata kujua kuwa Sultana si mlemavu wa macho katika ulimwengu halisi. Ili kufanikisha uigizaji wake, Sultana hutumia mbinu ya kuzama

kisaikolojia katika nafasi ya mhusika anayemwigiza. Vilevile, Sultana anaonekana akitumia ubunifu ili kujifananisha na mlemavu halisi. Ubunifu huo unamwezesha kuzama katika ulimwengu wa ulemavu na kufanya mambo ambayo kwa kawaida yangefanywa na mlemavu halisi wa macho. Hili linajitokeza kutokana na jinsi anavyoigiza kana kwamba yeye ni mlemavu halisi wa macho. Hata hivyo, Sultana anatekeleza tu jukumu alilopatiwa katika kipindi la kuigiza kama mlemavu wa macho. Kuigiza kwake kama mlemavu kunafaulisha dhamira ya ulemavu katika kipindi cha Sultana.

Buya anajifananisha na mlemavu wa miguu katika ulimwengu halisi. Buya anaonekana akiwa na mguu uliolemaa na vilevile anashiriki katika vitendo vinavyomwonyesha kama mlemavu. Anawekewa miguu bandikizi ya magurudumu ili aweze kutembea kama aliyelemaa. Vilevile, anatumia fimbo ya kutembelea inayomsaidia katika matembezi yake. Buya alipata ulemavu baada ya kushambuliwa na kujeruhiwa na majangili waliotumwa na mkewe, Fatima. Buya haachi nyuma fimbo yake ya kutembelea kila anapotoka nyumbani kwake kuelekea kazini au katika shughuli zake nyingine. Hili linaonyesha kuwa Buya amejitayarisha kisaikolojia ambapo anazama katika jukumu analoigiza. Buya pia anatumia miondoko ya mwili ili kuonekana kana kwamba mguu wake umelemaa, hivyo basi kujifananisha na watu walemavu katika dunia halisi. Kwa mfano, katika matembezi yake, Buya anachechemea. Katika ulimwengu halisi, kuna walemavu wa miguu ambao Buya anajifananisha nao. Kuna wale wanaotumia miguu bandia na wale wanaotumia fimbo za kutembelea ambazo huwasaidia kutembea kutoka eneo moja hadi jingine. Vilevile, walemavu wa miguu katika ulimwengu halisi aghalabu hutembea kwa kuchechemea. Hivyo basi, Buya anaiga watu ambao katika ulimwengu

wao halisi wana ulemavu wa miguu. Kuigiza kama mlemavu wa miguu kunafaulisha dhamira ya ulemavu katika kipindi hiki.

Kokani anajifananisha na walemavu wa ngozi katika ulimwengu halisi. Hili linaonekana katika hali yake ya ngozi. Ngozi katika uso wake inaonekana kama iliyojikunjakunja kuashiria kuwa alipata hali hiyo ya ulemavu kwa kuchomeka. Kokani anajitahidi kuficha uso wake kila anapokutana na watu ili wasiuone ulemavu wake. Hata kazini huwa hapendi kuonyesha uso wake kwa wafanyikazi wenzake au wagonjwa anaowatibu. Anajitazama kwenye kioo na kushangaa jinsi uso wake ulivyolemaa. Hata hivyo, Kokani si mlemavu wa ngozi katika ulimwengu halisi. Ametumia kifaa cha kuigiza kinachomfanya kuonekana kama mlemavu halisi wa ngozi. Ili kufanikiwa katika kujifananisha na walemavu halisi, Kokani anaonekana akijitayarisha kihisia kana kwamba yeye ni mlemavu. Aidha, Kokani anaonyesha kuwa na shime ya kuigiza kupitia vitendo vyake jukwaani. Mhusika huyu haonekani kama anayeigiza bali anaonekana kuwa mwenye ulemavu wa ngozi, wadhifa anaojifananisha nao. Katika dunia halisi kuna walemavu wa ngozi ambao Kokani anawaiga. Kuigiza kwa Kokani kunatumika katika kufaulisha dhamira ya ulemavu. Vilevile, Kokani anadhihirisha bidii katika masomo yake hadi kufaulu kuwa daktari. Matendo yake yanabainisha kuwa watu walemavu na wasio walemavu wanaweza kutia bidii maishani na wakafaulu katika shughuli zao.

Meja Jabali anaiga walemavu wa tabia katika jamii. Hili linajitokeza katika matendo yake na vilevile lugha anayoitumia. Mhusika huyu anaonekana akitumia mbinu ya kupiga chuku. Haya yanajitokeza katika maonyesho mbalimbali ya kipindi. Katika onyesho moja, Meja Jabali anaonekana akimuua baba yake ili aweze kunyakua mali yake. Katika

onyesho jingine, Meja Jabali anamuua mfanyakazi wake wa muda mrefu aliyejulikana kama Maneno kwa risasi. Vilevile, Meja Jabali anatumia bunduki yake kuwashambulia wanakijiji walioenda kwake kulalamika dhidi ya dhuluma alizokuwa akiwatendea. Meja Jabali anatumia lugha ya kuwadunisha watu wengine. Kwa mfano, anatumia neno vinyangarika kuwarejelea wanakijiji wenzake. Katika ulimwengu wa kawaida, kuna watu wenye tabia zinazoigizwa na Meja Jabali. Chuku inajitokeza pale ambapo mhusika huyu anaonekana akirudia matendo maovu. Huku ni kushadidia maudhui ya ukatili yanayowasilishwa na mhusika huyu. Katika mahojiano na Meja Jabali, ilijitokeza kuwa yeye alikuwa anaigiza masuala haya tu katika kipindi cha Sultana. Meja Jabali alikuwa na haya ya kusema katika dondoo lifuatalo:

> Kusema kweli katika jamii zetu kuna watu wanaoshiriki katika kuwatendea watu wengine mambo maovu. Kuna wauaji, wadanyanyifu, wanyang'anyi, wafisadi na kadhalika. Jukumu langu lilikuwa tu kuigiza tabia hizi ili kukipatia kipindi uhalisia kwani haya ni masuala yanayofanyika katika jamii zetu halisi. Mimi si muuaji au katili katika maisha yangu halisi (Data ya nyanjani, 2025).

Kupitia dondoo hili inadhihirika kuwa Meja Jabali si muuaji au katili katika maisha yake halisi. Haya ni majukumu aliyopatiwa katika kipindi cha Sultana ambayo aliweza kuyaigiza kwa ustadi. Kuigiza masuala haya kwa ubunifu kupitia utondoti wa matendo na hisia zake kunafaulisha maudhui ya ukatili na mauaji katika kipindi hiki, jambo linalodhihirisha kuwa wahusika hutumia mbinu za maigizo ili kuishawishi na kuiburudisha hadhira.

Kulingana na Mutugu (2019:133), mbinu mbalimbali hutumika katika kazi za kifasihi ili kuwasilisha maudhui. Mbinu hizo hujumuisha matumizi ya wahusika au hali zao za kipekee. Kwa mfano, Mutugu anataja mhusika Mzee Gae mwenye ulemavu wa akili katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* (1980) kama mbinu ya kuwasilisha maudhui. Kadhalika, wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana wametumia ubunifu wa kimaigizo unaojumuisha hali za kisaikolojia, matayarisho ya kihisia, miondoko ya mwili na chuku ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui mbalimbali. Mbinu hizi zimefanikisha kuibua maudhui ya bidii, ujasiri, mapenzi na unyanyapaa kupitia wahusika walemavu wa viungo, na vilevile maudhui ya mauaji, ukatili, tamaa na utabaka kupitia wahusika walemavu wa tabia. Hali hii inaendana na mhimili wa nadharia ya maigizo unaosisitiza kuwa uigizaji unapaswa kufanywa kwa ubunifu na kutumia mbinu mbalimbali ili kuvutia na kushawishi hadhira.

### 4.2.2 Ishara za Mwili

Ishara za mwili ni ishara zinazotumiwa na mtu na huambatanishwa na mazungumzo au sauti ili kutimiza lengo fulani (Bezemer na Mavers, 2011). Ishara hizi ni kama vile kurusha mikono au miguu, kutingiza kichwa au viungo vingine vya mwili kama mabega, kukodoa au kufunga macho, kukunja viganja vya mikono miongoni mwa ishara nyingine. Vilevile, mwonekano wa sura unaashiria aina fulani ya hisia. Katiba ya Kenya 2010 imetambua matumizi ya lugha za ishara kwa manufaa ya walemavu ambao hawawezi kuongea. Katika kipindi cha Sultana, wahusika wanaonekana wakitumia ishara mbalimbali za mwili kama mbinu ya kufanikisha maudhui. Wahusika walemavu wa viungo wakiwemo Sultana, Buya na Kokani wanatumia ishara za mwili katika kuwasilisha maudhui. Licha ya kuwa wahusika hawa wanatumia ishara hizi kwa wingi,

hili halimaanishi kuwa ishara hizi hutumiwa na walemavu pekee. Watu wasio walemavu pia wanaweza kutumia ishara hizi katika mawasiliano yao.

Sultana anatumia mikono yake sana katika kupitisha ujumbe wake kwa wahusika wengine. Mara kwa mara anaonekana akitumia mikono yake kuashiria kuwa anataka kwenda mahali au kufuata njia fulani. Akiwa nyumbani kwao anatumia mikono kuashiria mahali ambapo bahari inapatikana ambapo ni kusini ya wanapoishi. Aidha, Sultana anatumia mikono yake kuashiria yanapopatikana makao ya Meja Jabali. Licha ya kuwa haoni, Sultana anaelewa vyema mahali ambapo anaishi. Anaeleza kwa urahisi kwa kutumia ishara za mwili. Aidha, Sultana anatumia mikono yake wakati ambapo anakosa kukubaliana na hali au jambo fulani. Kwa mfano, Sultana anatikisa kiganja cha mkono wake na kutikisa kichwa chake ili kumjulisha Kokani kuwa hakubaliani naye. Huu ni wakati ambapo Kokani alitaka kumfungia Sultana katika chumba chake ili asije akatoka nje na kutangamana na wanaume wengine. Mbinu hii imetumika kama moja ya njia za mawasiliano katika kipindi hiki. Kupitia mahojiano na Sultana, ilibainika kuwa aghalabu alitumia ishara za mwili katika kufanikisha mawasiliano na wahusika wengine na kuweka wazi msimamo wake kuhusu mambo fulani. Sultana alikuwa na haya ya kusema katika dondoo lifuatalo:

> Hali yangu ya kuwa na upofu ilihitaji kutumia ishara za mikono kwa kiasi kikubwa ili kuashiria nilichokuwa nakitaka. Lakini sikutumia mikono peke yake bali pia kupitia mabadiliko ya sura yangu ni rahisi kujua hali yangu na msimamo wangu kuhusu jambo au hali fulani. Matumizi ya ishara yalienda sambamba na vitendo vyangu na yale nilikuwa nikisema (Data ya nyanjani, 2025).

Dondoo lililowasilishwa linaonyesha kuwa Sultana alitumia ishara za mwili huku akitumia ishara za mikono yake kwa kiasi kikubwa katika mawasiliano yake na wengine.

Buya anatumia ishara za mwili kudhihirisha hisia zake. Kwa mfano, Buya anakunja uso wake kuonyesha kughadhabishwa kwake na mkewe, Fatima wakati ambapo Fatima alitaka binti yao aolewe katika familia tajiri. Buya anakunja sura yake na kurusha mikono yake kuonyesha kughadhabishwa na maamuzi ya mkewe. Aidha, Buya anatumia mikono yake kuonyesha kuwa yeye ni mlemavu wa miguu. Anaeleza kwa lugha ya ishara ambapo anaunyoshea mguu wake kidole cha mkono kuonyesha kuwa anatumia mguu bandikizi. Anafanya hivyo wakati ambapo rafiki zake wanamtazama na kushangaa kumwona akitumia fimbo ya kutembelea.

Kokani huwa hazungumzi mara nyingi. Yeye hutumia ishara za mwili kupitisha ujumbe wake kwa wahusika wengine. Mara nyingi anaonekana akiwaita watu kwa kutumia ishara ya mkono. Kwa mfano, katika onyesho moja, Kokani anaonekana akimwita Bi. Salama kwa ishara ya mkono. Aidha, anawasalimia watu kwa kuwapungia mkono. Kokani hapendi kutangamana na watu kwa ukaribu hivyo basi anawasalimia kutoka mbali kwa kuwapungia mkono. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa hataki watu waone ulemavu wake wa ngozi. Kokani anaonekana kuogopa unyanyapaa wanaopitia walemavu wa ngozi. Matumizi ya ishara za mwili na mhusika huyu kunafanikisha maudhui ya unyanyapaa katika kipindi cha Sultana. Kokani anaogopa kuulizwa na watu kilichomtendekea au kukejeliwa kwa sababu ya hali yake.

Wahusika walemavu wa tabia pia wanatumia ishara za mwili katika kufaulisha dhamira na kufanikisha maudhui mbalimbali. Meja Jabali hupitisha ujumbe wake kupitia

mwonekano wa sura yake. Kwa mfano, katika onyesho moja, Meja Jabali anaonyesha sura ya tabasamu na kutikisa kichwa kuonyesha kuridhishwa na kitendo chake cha kumuua babake na kurithi mali yake kwa njia haramu. Ishara hii inaonyesha kuwa Meja Jabali ni katili. Katika onyesho jingine, Meja Jabali anaonyesha sura ya kicheko wakati anawakejeli wanaompinga. Meja Jabali anacheka sana wakati anapojulishwa na ndugu yake kuwa yeye ndiye mrithi halali wa mali aliyonayo na hivyo basi ajitayarishe kumkabidhi mali hiyo na kuenda jela kwa kosa la ulaghai. Meja Jabali anauchukulia ujumbe wa nduguye kimzaha na kucheka. Sura ya kicheko inamwonyesha Meja Jabali kama mtu anayefurahia maovu anayowatendea wengine. Meja Jabali pia huonyesha kununa na kukunja viganja vyake vya mkono wakati ambapo amekerwa na mambo fulani kama vile watu anaowadhulumu wanapodai haki zao. Hili linadhihirika wakati wanakijiji walienda nyumbani kwake kuandamana kupinga dhuluma dhidi yao. Meja Jabali anaonekana akikunja sura yake kuonyesha kughadhabishwa kwake na jambo hilo.

Fatima naye anaonyeshwa akitikisa viganja vya mikono yake na kuonyesha sura ya kukasirika kila mara anapokosa kukubaliana na mtu yeyote au kughadhabishwa na jambo fulani. Hili linajitokeza zaidi anapokosa kukubaliana na mumewe, Buya. Katika hali hiyo, Fatima hutikisa viganja kwa nguvu na kutikisa kichwa chake, ishara inayomwonyesha Buya kuwa katu hakubaliani na msimamo wake wa kumzuia bintiye Dida kuolewa katika familia ya Meja Jabali. Fatima anamkazia mumewe macho bila kusema lolote, jambo linaloashiria ghadhabu na tamaa ya kutaka bintiye aolewe kwa mali badala ya mapenzi ya dhati. Ishara hizi za mwili zinamwonyesha kama mkaidi na mwenye tamaa, na zinasaidia kuibua maudhui ya tamaa na migongano ya kifamilia.

Karimi (2022:88) anaeleza kuwa katika kazi za uandishi na usimulizi, wahusika hutumika kuendeleza mbinu za kifasihi kama vile maswali ya balagha, matumizi ya kinaya na kejeli. Katika kipindi cha Sultana, wahusika walemavu hutumia ishara mbalimbali za mwili, kama vile mwonekano wa sura na miondoko ya mikono, ili kupitisha ujumbe na kufanikisha maudhui kama vile ukatili na tamaa. Hali hii inalingana na mhimili wa nadharia ya maigizo unaosisitiza kuwa uigizaji sharti uwe wa ubunifu na kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa, kama vile ishara za mwili, sura za uso na miondoko ili kuwasilisha maudhui kwa ufanisi na kuvutia hadhira.

### 4.2.3 Mazungumzo

Mtunzi wa kazi za kisanaa huwa na masuala fulani anayotaka kuwasilisha kwa hadhira yake (Chemutai, 2016: 45). Ili kuyafanya masuala hayo kuwa na athari anayotarajia, mtayarishaji wa kazi za kisanaa hutumia mbinu fulani kuwasilisha masuala hayo. Moja ya mbinu hizo ni kutumia maneno. Mbinu hii inahusisha uteuzi wa msamiati na matumizi ya semi za lugha (Chemutai, 2016:45). Wahusika katika kipindi cha Sultana wanatumia maneno ili kuwasilisha maudhui mbalimbali. Usemi ni "tamko au kauli inayotolewa na mtu na yaweza kuwa neno moja, kirai, sentensi au zaidi" (Massamba, 1994: 55). Hivyo basi, usemi ni kauli inayotolewa na mtu na inaweza kutolewa baada au kabla ya mtu mwingine kuongea. Kwa upande mwingine, mazungumzo ni utaratibu wa maongezi baina ya pande mbili (Kiunga, 2016: 35). Hii inamaanisha kuwa mazungumzo ni kauli zinazotolewa na pande mbili huku kila pande ikiwa na wakati wake wa kutoa kauli. Mazungumzo hufanyika baina ya watu wawili au zaidi. Mtindo wa lugha unaohusisha uteuzi wa msamiati wa aina fulani katika usemi na mazungumzo ni moja kati ya mbinu zilizotumiwa sana na wahusika mbalimbali katika kipindi cha Sultana katika kuwasilisha

ujumbe na kufanikisha maudhui. Wahusika wote walemavu na wasio walemavu katika kipindi cha Sultana wanatumia mbinu ya mazungumzo ambapo wanateua msamiati wao kimakusudi kama njia kuu ya mawasiliano baina yao na kuwasilisha ujumbe.

Sultana anatumia maneno katika kupinga unyanyapaa. Katika kauli zake Sultana anatumia msamiati mahususi ili aweze kueleweka ipasavyo. Kwa mfano, akiwa baharini anakutana na vijana ambao wanamcheka kwa sababu ya upofu wake. Sultana anawaambia kuwa si kupenda kwake kuwa haoni na kuwa ni vibaya kumcheka mtu aliye na ulemavu. Sultana anaonekana kuteua na kutumia msamiati maalum unaoonyesha kuwa unyanyapaa dhidi ya walemavu wa viungo haufai. Anatumia maneno kama vile "si kupenda kwa mtu kuwa na upofu, usinicheke kwa sababu sioni, kuwa na heshima kwa kila mtu." Sultana pia anamweleza Jabali Junior ambaye ni mpenzi wake jinsi alivyopata ulemavu wake na kumweleza kuwa angependa kuona siku moja. Ni kupitia mazungumzo hayo ambapo Jabali Junior alimtafutia Sultana daktari wa macho ambaye aliweza kumtibu na hatimaye Sultana akapata uwezo wa kuona. Sultana anaonekana kuteua maneno yake kwa makini. Wakati anaelezea kuhusu ulemavu wake anatumia msamiati unaoonyesha kuwa kwa yakini yeye ni mlemavu wa macho. Kwa mfano, anasema kuwa "ni kweli mimi sioni, natumia hisia kutembea na kufika niendako." Vilevile, anatumia maneno yanayoonyesha kuwa unyanyapaa dhidi ya walemavu wa viungo haufai. Kwa mfano, anasema 'heshimu watu wote, usinidharau kwa sababu sioni.' Aidha, anatumia maneno ya heshima anapofanya mazungumzo na watu. Kwa mfano, licha ya Meja Jabali kumdharau na kumwita kinyangarika, Sultana anamuamkua kwa heshima. Maneno anayotumia Sultana ni mbinu anayoitumia katika kipindi hiki.

Buya anatumia mbinu ya mazungumzo katika mawasiliano yake na wahusika wengine katika kipindi cha Sultana. Buya ni mlemavu wa miguu. Ili kueleza kuhusu hali yake ya ulemavu, Buya anatumia msamiati maalum katika kauli zake. Kwa mfano, kupitia njia ya mazungumzo, Buya anamweleza Maria kuwa alipata kulemaa mguu wake baada ya kutumiwa majangili na mkewe, Fatima. Anatumia maneno kama vile "nilijeruhiwa, nilipachikwa mguu bandia, nilinunua fimbo ndio niweze kutembea kwa urahisi" ili kuielezea hali yake ya ulemavu. Hii ilikuwa baada ya Buya kukosana na mkewe ambaye aliwatuma majangili wakamuue. Majangili hao walimchapa na kumfungia Buya ndani ya pipa la taka wakidhani kuwa wamemuua. Buya aliokolewa na Maria ambaye alimpeleka kwake na kumpa huduma ya kwanza. Akiwa kwa Maria ndipo alisimulia masaibu yaliyompata kupitia kwa njia ya mazungumzo. Ni kupitia mazungumzo hayo ambapo Fatima anaonyeshwa kama mtu katili. Aidha, Buya anatumia lugha ya heshima katika mazungumzo yake. Licha ya kukosana na mkewe, Buya hatumii lugha ya kumwonyesha madharau au kumzushia hadhi. Bado anamrejelea mkewe akitumia maneno kama vile "mke wangu mpendwa, ni vizuri watu kuishi kwa kuelewana, heshima haina kikomo." Kauli zake Buya zinamwonyesha kama mtu mwenye hekima na busara.

Meja Jabali anaonyesha kuwadharau watu wengine kupitia maneno anayotumia. Hili linadhihirika kupitia kauli anazotoa katika mazungumzo baina yake na wahusika wengine. Kauli anazotumia zinawadunisha watu wengine. Lugha anayotumia Meja Jabali inaonyesha kuwakebehi maskini na walemavu hasa wa viungo. Kwa mfano, katika mazungumzo yake na mfanyakazi wake anayejulikana kama Kaka, Meja Jabali anadhihirisha kuwa na madharau. Katika mazungumzo hayo, Meja Jabali anamuuliza Kaka kwa nini alimruhusu kinyangarika kuingia katika boma lake. Anayerejelewa kama

kinyangarika na Meja Jabali ni Sultana. Neno kinyangarika ni la kumzushia hadhi Sultana kutokana na hali yake ya upofu. Meja Jabali anamwona Sultana kama mtu asiye na umuhimu wowote duniani. Aidha, Meja Jabali anawarejelea wanakijiji wenzake kama vinyangarika na wategemezi. Katika onyesho moja, Meja Jabali anatumia kauli kama vile vikaragosi hawa, vinyangarika hawa, watumwa kuwarejelea watu wengine. Maneno anayotumia yanaonyesha kutowathamini watu wengine.

Katika mahojiano na mtayarishaji wa kipindi cha Sultana, ilibainika kuwa Kutenda kwa kutumia maneno ni njia ya kimsingi inayotumiwa na wahusika katika kufanikisha maudhui ya kipindi. Mtayarishaji huyu alikuwa na haya ya kusema kupitia dondoo lifuatalo:

> Kutenda kwa kutumia maneno ni njia muhimu ya mawasiliano inayotumika katika kipindi cha Sultana. Hulka za wahusika aghalabu zinajitokeza kupitia kwa kile wanachokifanya au kile wanachokitenda. Wanayosema wahusika katika kipindi huchukuliwa kuwa na uzito kwa sababu hapo ndipo tunapopata maudhui ya kipindi. Kama mtu ni mbaya utamjua kupitia jinsi anavyozungumza na maneno anayotumia. Kwa mfano, Fatima anatumia maneno ambayo katika ulimwengu halisi tunayaita matusi (Data ya nyanjani, 2025).

Dondoo hili linaonyesha kuwa maneno wanayosema wahusika katika kipindi cha Sultana yana uzito mkubwa katika kujenga hulka zao. Tabia za wahusika hujitokeza kupitia lugha wanayotumia katika mawasiliano baina yao, ambapo wengine hutumia lugha ya heshima, ilhali wengine hutumia misemo ya kejeli na dharau. Msamiati anaotumia Meja Jabali unamwonyesha kama mlemavu wa tabia kwa kuwa maneno yake hufichua ukatili na

ukosefu wa utu. Kisaikolojia, walemavu wa akili mara nyingi hukosa uwezo wa kutafakari taathira ya lugha yao kwa wengine, hali inayokisiwa katika namna wahusika fulani wanavyotumia semi zao.

Chemutai (2016) anaeleza kuwa mtindo ni njia ya kipekee inayotumiwa na mwandishi au mtayarishaji wa sanaa ya maonyesho kujieleza, na hujitokeza kupitia uteuzi wa msamiati na matumizi ya semi. Mahenge (2017) anaongeza kuwa katika jamii halisi, mara nyingi walemavu hupewa majina ya kuwakebehi, jambo linalojitokeza pia katika kipindi cha Sultana kupitia maneno kama "kinyangarika" na "kikaragosi", ambayo hudhalilisha si tu walemavu wa viungo bali hata wasio walemavu. Naye Madumulla (2009) anasema kuwa wahusika hutumiwa na msanii kufanya mazungumzo yanayolenga masuala fulani ili kupitisha ujumbe. Msamiati unaotumiwa na wahusika katika kipindi hiki umeteuliwa kimakusudi ili kufikisha ujumbe na kufanikisha maudhui ya ukatili, dharau na unyanyapaa. Hali hii inadhihirisha utekelezaji wa mhimili wa nadharia ya maigizo, unaosisitiza kuwa uigizaji unapaswa kuwa wa ubunifu kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile uteuzi makini wa lugha na semi, ili kuibua maudhui na kuvutia hadhira.

### 4.2.4 Hisia na Mielekeo ya Wahusika

Mwelekeo ni mbinu inayojitokeza kulingana na jinsi wahusika walemavu wanavyoyatekeleza majukumu yao katika kipindi. Wahusika hawa wanaweza kuwa na mielekeo chanya au hasi kuhusu walemavu kutokana na vitendo vyao katika kipindi. Kwa mujibu wa Muguche (2022), walemavu hupitia changamoto mbalimbali katika jamii kama vile unyanyapaa. Muguche alionyesha kuwa nchini Kenya walemavu wa viungo

hupitia changamoto za kimazingira kutokana na hali zao. Kipindi cha Sultana kinaonyesha mielekeo ya wahusika kuhusu walemavu wa viungo na wale wa tabia.

#### 4.2.4.1 Hisia na Mielekeo ya Wahusika Walemavu wa Viungo

Maudhui mbalimbali yanayodhihirishwa kupitia kwa wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana yanaonyesha mielekeo mbalimbali ya wahusika hawa katika kipindi hiki. Kwa mfano, maudhui ya bidii, mapenzi, ujasiri na unyanyapaa yanaonyesha mwelekeo chanya wa wahusika walemavu wa kipindi hiki kuhusu ulemavu na walemavu kwa ujumla. Katika uigizaji wao, wahusika katika kipindi cha Sultana wanaonekana kuwa wenye bidii licha ya hali zao. Hili linaonyesha kuwa wahusika walemavu wa viungo wanawasilishwa kama wasio wahitaji tu ama wategemezi tofauti na matarajio ya jamii kuwa walemavu wa viungo ni wategemezi au wahitaji (Smith, 2019). Wahusika katika kipindi cha Sultana wanaonyesha kuwa walemavu na wasio walemavu wanaweza kuwa na bidii. Aidha, wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana wanajitokeza kama watu jasiri sawa na watu wasio walemavu. Licha ya kulemaa, wahusika hao pia wanaonekana kuwa na hisia za kupenda au kupendwa na watu wengine. Wahusika hawa wanaonyesha kuwa hakuna hisia au masuala yaliyotengewa walemavu na wasio walemavu. Walemavu wanaweza kuwa na bidii, ujasiri au upendo kinyume na matarajio ya jamii kuwa walemavu ni wategemezi, wanyonge au wasio na hisia za kupenda. Mwelekeo huu chanya kuhusu wahusika walemavu unajitokeza kutokana na jinsi wanavyosawiriwa na kutekeleza majukumu yao mbalimbali. Hili lilijitokeza katika mahojiano na mtayarishaji wa kipindi katika dondoo lifuatalo:

Kwa kawaida katika jamii, wahusika walemavu huchukuliwa kuwa dhaifu. Hata hivyo, kipindi hiki kililenga kubadilisha mwelekeo huo kwa kuwasawiri wahusika walemavu kama jasiri, wenye bidii na watu wasiotegemea wale wasio walemavu katika kukidhi mahitaji yao. Kwa mfano, Sultana anasawiriwa kama mhusika asiyeogopa hali ambazo kwa kawaida zingemwogopesha kama vile kwenda baharini bila msaidizi. Kokani ni daktari wa kutibu watu wagonjwa licha ya kuwa mlemavu wa ngozi (Data ya nyanjani, 2025).

Aidha, wahusika katika kipindi cha Sultana wanaonyesha mielekeo yao kuhusu unyanyapaa unaowakumba walemavu wa viungo katika ulimwengu halisi. Vitendo vyao vinaonyesha kuwa unyanyapaa dhidi ya walemavu haufai. Hili linajitokeza wakati wahusika walemavu wa tabia na wanaowadhulumu walemavu wa viungo wanaonyeshwa kama walio na tabia zisizofaa. Kwa mfano, Fatima ambaye anamwita Sultana kipofu anaonyeshwa kama mlemavu wa tabia. Aidha, Meja Jabali ambaye anamwita Sultana kinyangarika anaonyeshwa kama mhusika mwenye ulemavu wa tabia. Meja Jabali anaonyeshwa kama mwenye ukatili, muuaji na mwenye tamaa kutokana na vitendo vyake dhidi ya wahusika walemavu wa viungo.

#### 4.2.4.2 Mielekeo ya Wahusika Walemavu wa Tabia

Mwelekeo wa kipindi cha Sultana kuhusu wahusika walemavu wa tabia ni kuwa wahusika hao wanafaa kurekebisha tabia zao wao wenyewe au kwa kusaidiwa. Hili linaweza kufanywa kwa kuhusisha vituo mbalimbali vya kurekebishia tabia. Aidha, wahusika walemavu katika kipindi hiki wana mwelekeo kuwa tabia za uharibifu zinafaa kukomeshwa na wale walio na tabia kama hizo wanafaa kutiwa mbaroni na kufunguliwa

mashtaka na kisha kufungiwa korokoroni kama njia mojawapo wa kuwasaidia katika kurekebisha tabia zao. Hili linadhihirishwa na wahusika walemavu wa tabia kwenye kipindi wakati ambapo majangili waliotumwa na Fatima kumteka nyara Dida wanakamatwa na polisi baada ya Buya kuwaripoti katika kituo cha polisi. Meja Jabali aliwadhulumu na kuwatelekeza jamaa zake, akiwemo Sada ambaye ni dadake, mkewe Bi. Ua na wanakijiji kwa ujumla. Meja Jabali ananyang'anywa mali yote aliyomiliki kama vile magari, nyumba na hisa katika kampuni mbalimbali na akaunti zake zote kufungwa kupitia wakili wa Sada. Meja Jabali alikuwa amepata mali aliyokuwa nayo kwa njia ya ulaghai. Hii ni mali alioritishwa Sada na marehemu babake, lakini Meja Jabali alibadilisha wosia wa babake na kumiliki mali hii peke yake.

Aidha, wahusika walemavu wa tabia katika kipindi hiki wanaonyesha kuwa ulemavu wa tabia haufai katika jamii. Tabia kama vile unyanyapaa dhidi ya walemavu wa viungo, ukatili, ulaghai na tamaa zinaonekana kukemewa na wahusika katika kipindi hiki. Wahusika walemavu wa tabia wanaonekana kuishi maisha ya wasiwasi. Kwa mfano, Meja Jabali alishirikiana na Fatima kufanya uhalifu wa kuwavamia wengine kama vile kumuumiza Babu kwa kumbana ulimi na vidole vya mguu na kumlaghai Buya shilingi milioni mbili baada ya kumteka nyara Dida. Mwishowe, wawili hawa wanaishia kuishi maisha ya ombaomba baada ya kufukuzwa mle chumbani na Sada ambaye ndiye alikuwa mrithi halali wa mali ya babake. Meja Jabali na Fatima hawana malazi, mavazi na hata chakula. Wawili hawa wanafaulu kutorokea mafichoni kwa muda lakini polisi wanawasaka kwa udi na uvumba. Baadaye wanakamatwa kwa shutuma ya ulaghai. Njama yao ya kutorokea taifa la kigeni ili kuepuka kukamatwa inatibuka. Meja Jabali akiwa mafichoni anampigia inspekta simu ili amsaidie lakini hapewi msaada wowote.

Licha ya uhusiano wake na watu maarufu wenye vyeo vya juu serikalini, wakati huu wanakosa kumpa sikio. Mtayarishaji wa kipindi alikuwa na haya ya kusema kupitia mahojiano kwenye dondoo lifuatalo:

> Wahusika kama Meja Jabali wamesawiriwa kama watu walio na tabia zisizokubalika katika jamii. Nia ya kuwa na wahusika kama vile Meja Jabali ni kuonyesha uhalisia ulioko katika jamii kupitia kwa maigizo. Katika jamii zetu wapo wahusika walio na tabia za kuudhi kama vile Meja Jabali. Kusuta tabia zao kupitia maigizo ni moja kati ya njia za kusema kuwa tabia hizo hazifai na zinapaswa kukomeshwa (Data ya nyanjani, 2025).

Dondoo hili linadhihirisha wazi mwelekeo wa mtayarishaji wa kipindi kuhusu walemavu wa tabia. Vilevile, mielekeo ya wahusika walemavu inajitokeza kwani wao ndio wanaotumika kuonyesha kuwa ukatili, ulaghai, uharibifu na tamaa ni mambo yasiyokubalika na yanayopaswa kukomeshwa katika ulimwengu halisi. Kwa mtazamo wa kijamii, walemavu wa tabia huakisi watu wenye mienendo inayopingana na maadili ya jamii, na kupitia kipindi cha Sultana, mtayarishaji anaonekana kusuta tabia hizo kwa njia bunifu, ikiwemo kuwaonyesha wahusika kama watu walio na wasiwasi kutokana na matendo yao mabaya.

Kwa mujibu wa Rono (2013:30), wahusika hubeba na kuwasilisha ujumbe katika kazi za fasihi, na hivyo maudhui katika sanaa ya maonyesho hujitokeza kulingana na mielekeo ya wahusika ambayo huonyeshwa kupitia hisia zao. Wahusika wanaweza kudhihirisha hisia chanya au hasi kuhusu suala fulani. Katika kipindi cha Sultana, wahusika walemavu wa viungo hudhihirisha hisia zinazojenga mtazamo chanya kuhusu walemavu katika

jamii, ilhali walemavu wa tabia huibua hisia hasi zinazodhihirisha upinzani dhidi ya mienendo mibaya. Uwasilishaji huu wa hisia kupitia mbinu za kimaigizo unaendana na mhimili wa nadharia ya Maigizo, unaosisitiza kuwa uigizaji lazima uwe wa ubunifu na utumie mbinu mbalimbali kama vile hisia, mienendo na hali za wahusika ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui na kushawishi hadhira.

**4.3 Hitimisho**

Sura hii imechambua mbinu mbalimbali za maigizo zilizotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Jumla ya mbinu nne zimechambuliwa zikiwemo kufananisha, ishara za mwili, mazungumzo na mielekeo ya wahusika. Wahusika wametumia mbinu ya kufananisha ambapo wanatenda au kuigiza mambo ambayo yanafanyika katika ulimwengu halisi. Aidha, ishara za mwili zimetumika kama njia moja ya kupitisha ujumbe. Vilevile, wahusika wametumia mbinu ya mazungumzo kama vile uteuzi wa msamiati mahususi katika kuwasilisha ujumbe na kuhakikisha kuwa ujumbe wao unaeleweka kwa ufasaha. Mwisho, hisia za wahusika zinaonyesha mielekeo yao kuhusu suala la ulemavu na walemavu katika jamii.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeangazia mbinu mbalimbali za maigizo zilizotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kilichopeperushwa katika runinga ya Citizen. Sura hii inawasilisha yaliyoangaziwa katika sura nne zilizotangulia kwa muhtasari, matokeo ya utafiti kulingana na malengo na maswali ya utafiti na vilevile mapendekezo ya utafiti.

### 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Dhamira kuu ya utafiti huu ilikuwa kutathmini maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen nchini Kenya. Kipindi hiki kilipeperushwa kati ya Machi, 2022 na Julai, 2023 ikiwa ni takribani mwaka mmoja na miezi minne. Jumla ya sura tano zilijenga utafiti huu. Sura ya kwanza ilijenga msingi wa utafiti ambapo iliangazia vipengele kama vile usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka. Aidha sura hiyo imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada ambapo masuala ya ulemavu kwa jumla na masuala ya walemavu katika vyombo vya habari yameangaziwa. Vipengele vingine vilivyoangaziwa katika sura ya kwanza ni misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilishughulikia lengo la kwanza la utafiti ambalo ni kujadili maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Data iliyotumika ni ya nyanjani na ile ya maktabani. Mihimili ya nadharia ya Maigizo na maelezo ya wataalamu mbalimbali yalitumika katika kujadili maudhui

mbalimbali yanayowasilishwa na wahusika walemavu wa viungo na wa tabia katika kipindi cha Sultana yalibainishwa na kujadiliwa. Utafiti uliangazia walemavu wa viungo na wa tabia. Walemavu wa viungo katika kipindi cha Sultana ni watatu, ambao ni Sultana, Buya na Kokani. Aidha, wahusika walemavu wa tabia ni watatu, nao ni Meja Jabali, Fatima na Kaka.

Sura ya tatu ilishughulikia lengo la pili la utafiti ambalo lilikuwa kubainisha sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Data ya nyanjani na ya maktabani ilihusishwa katika kubainisha sifa hizo. Mihimili ya nadharia ya Maigizo ilitumika huku pia maelezo ya wataalam mbalimbali yakitumika katika kubainisha sifa hizo. Utafiti ulibainisha sifa mbalimbali zilizodhihirishwa na walemavu wa viungo na wa tabia katika kipindi hiki.

Sura ya nne ilishughulikia lengo la tatu la utafiti ambalo ni kufafanua mbinu za maigizo zinazotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Sura hii pia ilitumikiza data ya nyanjani na ile ya maktabani katika kufafanua mbinu mbalimbali zilizotumiwa na wahusika walemavu wa viungo na wa tabia. Aidha, maelezo ya wataalamu mbalimbali na mihimili ya nadharia ya Maigizo ilitumika katika kufafanua mbinu walizotumia wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Lengo la kwanza lilidhamiria kujadili maudhui yanayowasilishwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Baada ya kuchanganua data ya nyanjani na maktabani, maudhui mbalimbali yaliyowasilishwa katika kipindi cha Sultana yalibainishwa na kujadiliwa. Maudhui yaliyotokana na wahusika walemavu wa viungo ni pamoja na

maudhui ya bidii, mapenzi, ujasiri na unyanyapaa. Maudhui ya bidii yamedhihirishwa na wahusika wote walemavu wa viungo ambao ni Sultana aliye mlemavu wa macho, Buya aliye mlemavu wa miguu na Kokani aliye mlemavu wa ngozi. Sultana anajitafutia riziki bila kutegemea mtu yeyote, Buya anafanya bidii na kumiliki mali licha ya kulemaa miguu huku Kokani akitia bidii katika masomo yake na kuwa daktari wa kutibu wagonjwa. Aidha, utafiti ulibaini kuwa wahusika walemavu, kama ilivyo kwa wahusika wasio walemavu, wanaweza kupenda na kupendwa. Sultana anapendana na kufanya harusi ya kifahari na Jabali Junior. Maudhui ya ujasiri yanadhihirishwa na Sultana anayeenda baharini bila kuhitaji usaidizi wowote na Kokani anayepigania haki za wanakijiji wao. Aidha, maudhui ya unyanyapaa yanadhihirishwa na Kokani anayeogopa kutangamana na watu wakiwemo wagonjwa anaowatibu hospitalini na wafanyikazi wenzake. Sultana pia anakumbana na watu wanaomkejeli kwa sababu ya hali yake ya upofu.

Wahusika walemavu wa tabia wametumika kuwasilisha maudhui ya ukatili, mauaji, tamaa na utabaka. Maudhui ya ukatili yanadhihirishwa na Meja Jabali anayewanyanyasa wafanyikazi wake kwa kutowalipa mishahara yao, kuwachapa na kuwanyima chakula. Fatima naye anamtafutia mumewe majangili wanaomcharaza na kumjeruhi. Meja Jabali anashiriki katika mauaji ya watu mbalimbali akiwemo babake, mfanyakazi wake na mtoto wa mfanyakazi wake. Aidha, kupitia kwa Meja Jabali, maudhui ya tamaa yanajitokeza ambapo mhusika huyu anamuua babake kwa ajili ya mali. Naye Fatima anataka mtoto wake aolewe katika familia tajiri ndio apate mali zaidi. Hii ni licha ya kuwa Fatima hakuwa maskini.

Sura ya tatu ilichambua lengo la pili ambalo lilikuwa kubainisha sifa za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Utafiti ulibainisha sifa mbalimbali za wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana zikiwemo sifa za wahusika walemavu wa viungo na wale wa tabia. Sifa za Sultana ambaye ni mlemavu wa macho ni pamoja na kuwa mkakamavu, mwepesi wa hasira na muwajibikaji. Kokani ambaye ni mhusika mlemavu wa ngozi anaonyesha kuwa mbinafsi na mpweke. Naye Buya aliye mlemavu wa miguu anadhihirisha kuwa mvumilivu na mwenye heshima. Meja Jabali aliye mlemavu wa tabia ni mwenye taasubi ya kiume na katili. Fatima aliye mlemavu wa tabia ni mdanganyifu na mwenye tamaa. Aidha, Kaka ambaye ana ulemavu wa tabia anaonyesha kuwa mkaidi na mchochezi. Sifa za wahusika walemavu katika kipindi hiki zinafaulisha maudhui mbalimbali yanayowasilishwa na kipindi hiki.

Aidha, sura ya nne ilichambua mbinu za maigizo zinazotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Baada ya uchanganuzi wa data ya nyanjani na ile ya maktabani, utafiti ulibainisha mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Mbinu hizo ni kama vile kufananisha, ishara za mwili, mazungumzo na mielekeo ya wahusika. Wahusika wote waliigiza masuala mbalimbali jambo linalodhihirika kupitia matendo yao kama vile Sultana kuigiza kama mlemavu wa macho, Buya kuigiza kama mlemavu wa miguu na Kokani kuigiza kama mlemavu wa ngozi. Aidha, Meja Jabali, Fatima na Kaka waliigiza kama watu walio na upungufu wa maadili. Wahusika pia wanatumia ishara za mwili kama vile mwonekano wa sura na ishara za mikono katika kupitisha ujumbe. Kadhalika, wahusika wanatenda kwa kutumia maneno ili ujumbe wao ueleweke kwa njia iliyo bayana. Sultana anatumia maneno yanayodhihirisha kuwa yeye ni mlemavu wa macho huku Buya akitumia maneno

yanayomwonyesha kama mtu aliye na hekima na busara. Aidha, Meja Jabali anatumia maneno yanayomwonyesha kama katili, muuaji na mkosa heshima huku msamiati wa Fatima ukimwonyesha kama mwenye tamaa, katili na mdanganyifu. Vilevile, wahusika wanaonyesha mielekeo yao kuhusu suala la ulemavu na walemavu kwa jumla. Maudhui yanayowasilishwa kupitia kwa wahusika Sultana, Buya na Kokani yanaonyesha kusuta unyanyapaa dhidi ya walemavu wa viungo. Maudhui ya bidii, mapenzi na ujasiri yanaonyesha kuwa walemavu wa viungo wana uwezo wa kufaulu katika masuala mbalimbali katika jamii sawia na watu wasio walemavu.

### 5.4 Changamoto za Utafiti

Changamoto mbalimbali zilikumba utafiti huu. Changamoto kubwa ilikuwa ya kufanya mahojiano na watayarishaji na wahusika wa kipindi cha Sultana kulingana na ratiba ya mahojiano. Tatizo hili lilitokana na wahojiwa kubanwa na shughuli zao mbalimbali. Tatizo hili lilitatuliwa kwa kufuata ratiba ya wahojiwa katika kupanga vikao vya mahojiano.

Changamoto nyingine ilikuwa ya kupakua data kutoka kwa majarida mbalimbali mtandaoni. Mengi ya majarida ya mtandaoni yalihitaji kujisajili na kulipa kiwango kikubwa cha ada ya usajili. Changamoto hii ilitatuliwa kwa kutumia majarida yanayopatikana bila ada, maktaba za chuo kikuu zenye usajili rasmi, pamoja na msaada wa wakufunzi waliotoa mwongozo wa kupata vyanzo mbadala visivyo na vizuizi vya kifedha.

## 5.5 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umetathmini maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana. Kipindi hiki kina upekee kwani kimewapa wahusika walemavu nafasi ya kipekee kama wahusika wakuu na vilevile kuwapa sifa zinazowatambulisha kama watu wa kawaida wanaoweza kuwa na sifa chanya au hasi, jambo ambalo ni nadra katika vipindi vingine. Wahusika walemavu wa viungo wameonyeshwa kama watu wanaoweza kuwa na sifa chanya kama vile bidii, ujasiri, ukakamavu, hekima na uvumilivu. Hivyo basi, utafiti huu utawafaa mno watafiti, wasomaji na wasomi wengine wa baadaye katika uwanja wa fasihi simulizi hasa katika maigizo.

Aidha, utafiti huu umeonyesha kuwa unyanyapaa dhidi ya walemavu hauna mantiki. Ulemavu unaweza kumpata mtu yeyote na wakati wowote kupitia njia mbalimbali kama vile ajali. Hivyo basi, utafiti huu utawanufaisha wasomaji kuwa na mielekeo chanya kuhusu ulemavu na walemavu.

## 5.6 Mapendekezo ya Utafiti

### 5.6.1 Mapendekezo kwa Wadau Mbalimbali

Utafiti huu unatoa mapendekezo yafuatayo kwa wadau mbalimbali katika sekta ya filamu nchini Kenya:

Kwanza, utafiti unapendekeza vyombo vya habari na televisheni kuandaa na kutekeleza sera za ndani zinazohakikisha uwakilishi jumuishi wa watu wenye ulemavu, huku zikitoa nafasi kwa waigizaji wenye ulemavu kushiriki moja kwa moja katika uigizaji na utayarishaji wa vipindi. Pili, serikali na watunga sera wanahimizwa kutumia matokeo ya

utafiti huu kama rejeleo la kuimarisha sera na miongozo ya maudhui ya vyombo vya habari ili kuhakikisha zinazingatia misingi ya usawa, ujumuishi na haki za watu wenye ulemavu. Tatu, mashirika ya kijamii pamoja na yale yanayoshughulika na masuala ya ulemavu yanashauriwa kushirikiana na sekta ya burudani kwa kutoa mafunzo, ushauri na mrejesho wa kitaalamu kuhusu namna ya kuwasilisha ulemavu kwa njia chanya, yenye heshima na kuelimisha jamii.

### 5.6.2 Mapendekezo kwa Tafiti za Baadaye

Utafiti umetoa mapendekezo yafuatayo kwa tafiti za baadaye:

Utafiti huu ulitathmini maigizo ya wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana kwenye runinga ya Citizen. Kuna haja ya utafiti mwingine kufanywa ili kuangazia wahusika wengine kama vile wahusika wakongwe na wale wasio walemavu katika vipindi vya televisheni.

Aidha, utafiti huu ulihusisha mtayarishaji wa kipindi cha Sultana na wahusika walemavu katika kipindi hicho. Hivyo basi, kuna haja ya utafiti mwingine kufanywa ili kushirikisha watazamaji wa kipindi hicho hasa watazamaji ambao ni walemavu katika maisha halisi kwa sababu mtazamo wao kuhusu ulemavu katika jamii ni muhimu. Aidha, utafiti uling'amua kuwa wahusika walemavu si walemavu katika dunia halisi. Kuna haja ya utafiti zaidi kufanywa kuangazia changamoto wanazopitia waigizaji ambao ni walemavu katika maisha yao halisi.

Utafiti huu umechangia kwa kutoa mtazamo wa kipekee kuhusu namna ambavyo wahusika walemavu wanawakilishwa katika kipindi cha Sultana. Kwa kuwa utafiti ulihusu kipindi hiki pekee, umefungua mwanya wa uelewa ambao tafiti zijazo zinaweza

kuendeleza kwa kuchunguza vipindi vingine vya televisheni vinavyohusisha wahusika walemavu. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yanatoa msingi muhimu wa kulinganisha na kupanua uelewa kuhusu uwasilishaji wa walemavu katika vyombo vya habari nchini Kenya na kwingineko. Aidha matokeo ya utafiti yatakua na mchango mkubwa wa kuhamasisha wanajamii juu ya vipawa vya walemavu na jinsi vinaweza kutumika katika kujenga uwezo wao wa kushiriki katika ujenzi wa jamii.

## 5.7 Hitimisho

Sura hii imewasilisha muhtasari wa yaliyoangaziwa katika sura nne zilizotangulia. Aidha, matokeo ya utafiti kulingana na malengo na maswali ya utafiti yamewasilishwa katika sura hii. Imebainika kuwa wahusika walemavu wa viungo katika kipindi cha Sultana wamewasilisha maudhui mbalimbali yakiwemo maudhui ya bidii, mapenzi, ujasiri na unyanyapaa. Wahusika walemavu wa tabia wamewasilisha maudhui ya ukatili, mauaji, tamaa na utabaka. Vilevile, sura imejadili sifa za wahusika walemavu ambazo ni ukakamavu, wepesi wa hasira, uwajibikaji, ubinafsi, upweke, uvumilivu, kuwa na hekima, kuwa na taasubi ya kiume, tamaa, udanganyifu, ukaidi na uchochezi. Aidha sura hii imeonyesha mbinu mbalimbali zilizotumiwa na wahusika walemavu katika kipindi cha Sultana zikiwa ni kufananisha, ishara za mwili, Mazungumzo na mielekeo ya wahusika. Sura hii pia imeangazia changamoto mbalimbali alizokumbana nazo mtafiti katika harakati za kutafuta data. Mchango wa utafiti huu pia umejadiliwa. Mwisho, sura hii imetoa mapendekezo ya tafiti nyingine kufanywa ili kuziba pengo ambalo halikuangaziwa katika utafiti huu.

**MAREJELEO**


Babbie, E. (2016). *The basics of social research*. Cengage Learning.

Barnes, C. (1992). *Disability imagery and the media: An exploration of the principles for media representations of disabled people*. Ryburn Publishing.

Bezemer, J., & Mavers, D. (2011). Multimodal transcription as academic practice: A social semiotic perspective. *International Journal of Social Research Methodology, 14*(3), 191–206. https://doi.org/10.1080/13645579.2011.563619

Briggs, C. L., & Bauman, R. (1992). Genre, intertextuality, and social power. *Journal of Linguistic Anthropology, 2*(2), 131–172. https://doi.org/10.1525/jlin.1992.2.2.131

Buliba, G., na wenzake. (2014). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Serengeti Educational Publisher Limited.

Chemutai, M. J. (2016). *Mtindo katika hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili* (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta).

Cohen, E., Ite, U., van der Geest, S., & Adegoke, T. A. (2007). Research ethics in ethnography/anthropology. *Social Science & Medicine, 65*(12), 2248–2259. https://doi.org/10.1016/j.socscimed.2007.08.002

Creswell, J. W. (2013). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (4th ed.). Sage Publications.

Devlieger, P. J. (1999). Frames of reference in African proverbs on disability. *International Journal of Disability, Development and Education, 46*(4), 439–451. https://doi.org/10.1080/103491299100597

Dimbu, S. (2021). *Uchanganuzi makinifu wa diskosi katika vikatuni vya Shujaaz* (Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Chuka).

Fine, E. (1994). *The Folklore Text: The Performance to Print*. Indiana University Press: Bloomington.

Foley, J. M. (1995). *The Singer of Tales in Performance.* Indiana University Press: Bloomington.

Gao, H., & Njeri, W. (2020). Challenges and Opportunities for Disabled Actors in Television: A Case Study. Communication Studies Journal, 9(3), 275-291.

Gao, H., & Njeri, W. (2020). Collaborative Efforts for Inclusive Representation: The Role of Disability Organizations in Television. Disability & Media, 8(2), 145-160.

Hakim, C. (1982). Secondary analysis and the relationship between official and academic social research. *Sociology*, *16*(1), 12-28.

Kafka F. (1990). The damaged self. In *The Body Silent* (pp. 249-260). Routledge.

Karimi, S. K. (2022). *Nafasi ya Wahusika Wendawazimu Katika Riwaya Teule: Kidagaa Kimemwozea na Mkamadume* (Haijachapishwa) Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.

King'ei, G. K. na Kisovi, C. N. (2005). Msingi wa Fasihi Simulizi. Kenya Literature Bureau.

Kiunga, T. M. (2016). *Maana ya Usemi na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii Hususani Facebook na Twitter* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Kobia, J (2004): 'Taswira ya mwanamke katika rnethali (njuno) za Kimeru' M. Phil Thesis Moi University

Kombo, D. K., & Tromp, D. L. (2006). Proposal and thesis writing: An introduction. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2004). Research Methodology: Methods and Techniques. New Age International.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Mture Educational Publications.

Mahenge, E. G. (2017). Msigano wa Majina ya 'Walemavu' katika Jamii ya Wazungumzaji Kiswahili: Mifano kutoka Tanzania. Kioo cha Lugha, 11 (1).

Massamba, D. P. B. (1994). Historia ya Kiswahili. *Jarida la Kichaa*, 1, 34 – 42.

Mathooko, P., et al. (2012). Literature review on media portrayal of people with disabilities in Kenya. *International Journal of Humanities and Social Science, 2*(8), 223–228.

Matti, G. N. (1996). *Sanaa za maonyesho za Kiafrika Sajadi: Mfano wa tohara ya Watharaka* (M.Phil. thesis, Moi University).

Mawira, S. (2020). Disability and marginalization: An examination of media representations. *African Journal of Communication, 38*(2), 147–162.

Mbarouk, J. S. (1998). *Matumizi ya lugha katika nyimbo za watoto* (Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Zanzibar, haijachapishwa).

McCombes, S. (2019, November 5). *Descriptive research: Definition, types, methods & examples*. Scribbr. https://www.scribbr.com/methodology/descriptive-research/

Mchepange, S. O., & Mahenge, E. G. (2022). Methali za Kiswahili zihusuzo ulemavu: Mitazamo na athari zake katika jamii. *Swahili Forum, 29*, 114–133. https://doi.org/10.25158/vol29

Mohamed, S. A. (1980). *Dunia mti mkavu*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Muguche, A. L. (2022). *Ulinganishaji wa ujifunzaji stadi za Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu, Kenya* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta).

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi: Sasa Sema Publishers.

Mutegi, L. (2010). *Maigizo katika fasihi simulizi: Mfano wa Kirarire katika nyimbo za tohara za Wameru* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, haijachapishwa).

Mutugu, B. N. (2019). Taswira za Ulemavu Kama Mtindo Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu, K., & Chimerah, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu* (Vol. 1). Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, P. (2018). Disability Representation in African Television: A Critical Analysis. African Journal of Cultural Studies, 36(1), 29-46.

Robinson, D. (1980). *Performative linguistics: Speaking and translating as doing things with words*. Routledge.

Rono, P. (2013). Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemuozea. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Schechner, R (1988). Performance Theory London and New York: Routledge.

Senkoro, F. E. (1982). *Fasihi*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Shule, V. (2017). Filamu za Kiswahili nchini Tanzania: Athari za' Kauli' za Wasambazaji-Wauzaji kwa Wasanii na Jamii. *Kioo cha Lugha*, *12*(1).

Smith, L. (2019). Representations of Disability on Television: A Critical Review. Journal of Media Studies, 8(2), 145-160.

Stanislavski, K., & Benedetti, J. (2009). *An actor's work on a role*. Routledge.

Traore, A. (1972). Theatre in Black Africa and Madagascar.

TUKI. (2013). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Tatu. Nairobi: OUP.

Turner, V.W. (1969): The Ritual Process. London: Routledge and Kegan Press

Wa-Mungai, M. (2007). “Bodily contrariness”: Some preliminary questions on disability and leadership. In J. Barkan, M. Katumanga, & P. Njogu (Eds.), *Good governance and development: Toward quality leadership in Kenya* (pp. 163–182). Nairobi: Twaweza Communications.

Wa Thiong’o, N. (1986). *Petals of blood*. Nairobi: East African Publishers.

Wa Thiong’o, N. (1986). *Decolonising the mind*. London: Heinemann.

Wa Thiong’o, N. (2006). *Wizard of the crow*. New York: Random House.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Nairobi: Focus Publications.

Wanjala, F. S. (2011). *Kitovu cha fasihi simulizi: Kwa shule, vyuo na ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wright, P. (2006). *A language of the body: Images of disability in the works of D. H. Lawrence* (Doctoral dissertation, Washington State University).

Yovo, P. N. (2021). *Uchunguzi wa jinsi masuala ibuka yalivyoigizwa katika ngonjera za Kiswahili katika tamasha za drama za kitaifa nchini Kenya (2010–2017)* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, haijachapishwa).

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A

## MWONGOZO WA MAHOJIANO KWA MTAYARISHAJI WA KIPINDI CHA SULTANA

## KITANGULIZI

I. Ulitumikiza wahusika walemavu wangapi kwenye kipindi cha Sultana?

II. Kwa nini uliamua kutumia wahusika hawa?

III. Ni changamoto zipi zilizopo katika kutumia wahusika walio na ulemavu?

IV. Ni mafunzo yapi ulitarajia watazamaji wayapate kutokana na uigizaji wa wahusika walemavu?

V. Uliwaumbia tabia zipi wahusika hawa walemavu?

VI. Kwa nini?

VII. Je, ni jinsi gani wahusika walemavu wamewasilisha uigizaji wao kwa watazamaji?

## KIAMBATISHO B

## MWONGOZO WA MAHOJIANO KWA WAHUSIKA WA KIPINDI CHA SULTANA

## KITANGULIZI

I. Unaigiza kama nani kwenye kipindi cha Sultana?

II. Je, unawezaje kuigiza uhusika uliyopewa?

III. Ni mbinu zipi za maigizo unazotumia kufanikisha jukumu la kuigiza unalopewa?

IV. Ni changamoto zipi unazokumbana nazo wakati wa kuigiza?

V. Ni nini suluhisho ya changamoto hizo?

## KIAMBATISHO CHA C: BARUA YA SHULE YA MASOMO YA VIWANGO VYA JUU

**KENYATTA UNIVERSITY**
**GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 810901 Ext. 4150**

**Internal Memo**

---

**FROM:** Executive Dean, Graduate School

**DATE:** 27th January, 2025,

**TO:** **Getate K. Caroline**
**C/o Kiswahili & African Languages Dept.**

**REF: C50/OL/CTY/32347/2016**

**SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL**

---

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 15th January, 2025 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, **" Tathmini Maigizo ya Wahusika Walemavu Katika Kipindi Cha Sultanana Kwenye Runinga ya Citizen Nchini Kenya ."**

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Also, please ensure that you publish article(s) from your project before submitting it to Graduate School for examination as per the Commission for University Education and Kenyatta University guidelines.

Thank you.

**ELIJAH MUTUA**
**FOR: EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL**

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Dr. Richard Wafula
C/o Department of Kiswahili & African Languages
Kenyatta University

EM/k

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

**Our Ref: C50/OL/CTY/32347/2016**

**DATE: 27th January,** 2025

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR GETATE K. CAROLINE - REG. NO. C50/OL/CTY/32347/2016**

I write to introduce **Getate K. Caroline** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the **Department of Kiswahili & African Languages.**

**Getate** intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, **"Tathmini Maigizo ya Wahusika Walemavu Katika Kipindi Cha Sultanana Kwenye Runinga ya Citizen Nchini Kenya."**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

**PROF. ELIUD NJAGI**
**EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL**

*EM/kc*

*Transforming Higher Education… Enhancing Lives*
Kenyatta University is ISO 9001:2015 Certified

Page 1 of 1

## KIAMBATISHO CHA D: IDHINI YA KUFANYA UTAFITI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **526043**

Date of Issue: **14/February/2025**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Ms.. Getate Kemunto Caroline of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev. 2014) in Nairobi on the topic: TATHMINI YA MAIGIZO YA WAHUSIKA WALEMAVU KATIKA KIPINDI CHA SULTANA KWENYE RUNINGA YA CITIZEN NCHINI KENYA for the period ending : 14/February/2026.**

License No: **NACOSTI/P/25/416032**

**526043**

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**
Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

**CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE**

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to.
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
   i. Endanger national security
   ii. Adversely affect the lives of Kenyans
   iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
   iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
   v. Adversely affect the environment
   vi. Adversely affect the rights of communities
   vii. Endanger public safety and national cohesion
   viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. Neither the license nor any rights thereunder are transferable.
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke